# UHAKIKI WA TAMTHILIA YA WATOTO KAMA ZAO LA MICHEZO YA UTOTONI

na

**BWIRE THEDIUS OJIAMBO**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (MASTER OF ARTS) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**Septemba, 2004**

University of NAIROBI Library
0404777 5

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

..................................................

BWIRE THEDIUS OJIAMBO

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa na sisi tulioteuliwa na chuo kuisimamia

..................................................

Dkt. MWENDA MBATIAH

..................................................

Dkt. KINEENE WA MUTISO

# YALIYOMO

TABARUKU........................................................................................ v
SHUKRANI........................................................................................ vii
MUHTASARI........................................................................................ viii

**SURA YA KWANZA**
1.1 UTANGULIZI........................................................................ 1
1.2 TATIZO LA UTAFITI........................................................... 2
1.3 KUSUDI LA UTAFITI........................................................... 3
1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII.................................... 4
1.5 MIPAKA YA UTAFITI........................................................... 4
1.6 NADHARIA TETE................................................................. 6
1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII.............................. 7
1.8 MSINGI WA NADHARIA....................................................... 9
1.9 NJIA ZA UTAFITI................................................................. 11
1.9.1 UCHUNGUZI WA NYANJANI............................................... 12
1.9.2 HOJAJI ................................................................................. 12
TANBIHI................................................................................... 12

**SURA YA PILI**
HALI YA MICHEZO YA UTOTONI NCHINI
2.1 UTANGULIZI......................................................................... 15
2.2 MICHEZO YA UTOTONI....................................................... 15
2.3 USHIRIKI WA WATOTO KATIKA MICHEZO YA UTOTONI......... 16
2.3.1 MASUALA YA KINYUMBANI............................................... 18
2.3.2 MASUALA YA SHULENI..................................................... 19
2.3.3 MASUALA YA HOSPITALINI............................................... 19
2.3.4 MASUALA YA MIJINI.......................................................... 20
2.3.5 MASUALA YA KIBUNILIZI.................................................. 20
2.4 VIAMBAJENGO VYA MICHEZO YA UTOTONI.......................... 21
2.4.1 PLOTI................................................................................. 21
2.4.2 MAUDHUI........................................................................... 22
2.4.3 WAHUSIKA......................................................................... 23
2.4.4 MANDHARI......................................................................... 24
2.4.4.1 MALEBA KATIKA MICHEZO YA UTOTONI........................... 24
2.4.4.2 JUKWAA KATIKA MICHEZO YA UTOTONI............................ 25
2.5 DHIMA YA MICHEZO YA UTOTONI MAISHANI MWA WATOTO. 26
TANBIHI................................................................................... 30

**SURA YA TATU**
MAUDHUI KATIKA DRAMA YA WATOTO
3.1 UTANGULIZI......................................................................... 31
3.2 TAMASHA ZA DRAMA ZA SHULE NA VYUO.......................... 33

3.2.1 MAUDHUI YA *TUZO AZIZI*........................................ 35
3.2.2 MAUDHUI YA *MAJUTO*........................................ 37
3.2.3 MAUDHUI YA *MONALISA*........................................ 39
3.2.4 MAUDHUI YA *VISOSAUTI*........................................ 41
3.3 KIMALIZIO........................................ 43
TANBIHI........................................ 44

**SURA YA NNE**
WAHUSIKA NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA DRAMA YA WATOTO
4.1 UTANGULIZI........................................ 45
4.2.1 *TUZO AZIZI*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA....... 46
4.2.2 *MAJUTO*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA............ 51
4.2.3 *MONALISA*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA......... 55
4.2.4 *VISOSAUTI*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA......... 60
4.4 KIMALIZIO........................................ 66
TANBIHI........................................ 67

**SURA YA TANO**
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO
5.1 HITIMISHO........................................ 68
5.2 MAPENDEKEZO........................................ 70
MAREJELEO........................................ 72

KIAMBATISHO 1A (HOJAJI KWA WATOTO)........................................ i
KIAMBATISHO 1B (HOJAJI KWA WATUNZI/WALIMU)........................ iv
KIAMBATISHO 2a........................................ vi
KIAMBATISHO 2b........................................ ix
KIAMBATISHO 2c........................................ xi
KIAMBATISHO 2d........................................ xiii
KIAMBATISHO 3a........................................ xv
KIAMBATISHO 3b........................................ xxxiv
KIAMBATISHO 3c........................................ xlvii
KIAMBATISHO 3d........................................ xvl

## TABARUKU

Tasnifu hii ni tabaruku kwako Zephaniah Otinga Nyonje uliyetuaga tarehe 12 Mei, 2004 ukiwa umetimiza miaka tisini na minne. Babu, mapenzi yako kwa watoto hayakuwa na kifani.

**SHUKRANI**

Hii ni kazi ambayo imechukua subira na ustahimilivu mwingi. Nawashukuru enyi mliojenga kivuko tisti kilichonivusha hadi ng'ambo ya pili. Ninatambua ugumu wa kuwataja nyote; kwa wale ambao sitaweza kuwataja, eleweni ugumu wa wajibu huu na kisha jumuikeni na wale nitakaoweza kuwakumbuka kwa sasa.

Mwanzo kabisa, ninapenda kuwashukuru jazila wasimamizi wangu Dkt. Mwenda Mbatiah na Dkt. Kineene wa Mutiso kwa mawaidha yenu ainati na kwa kujitolea bila kuchoka wala kunung'unika kuutumia muda wenu kuisoma na kuielekeza kazi hii.

Shukrani za kipekee na zimwendee msimamizi wangu mwasisi mwalimu Timothy Arege ambaye sasa ni mhadhiri katika chuo kikuu cha Catholic University of East Africa. Ahsante kwa himizo zako za mara kwa mara na kuutenga muda wako kunisikiza na kunipa ushauri pindi nilipokuhitaji.

Sina budi kukupa shukrani zangu za udhati wa moyo wangu ewe Dkt. Ezekiel Alembi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuniamini na kunipa uhuru wa kutumia maktaba yako ya kibinafsi. Zipokeeni ahsante zangu wahadhiri Richard Mgullu, Dkt. Kithaka wa Mberia, Dkt. Alfred Buregeya na Prof. Abdulaziz.

Ni furaha yangu kuishukuru kwa dhati aila ya Mzee Ojiambo Mataya hususan ndugu zangu Evans Manana, Mary Nyongesa China, Henry Ojiambo, Godfrey Ojiambo, Patrick Omondi, Ben Ojiambo na Rael Mutola. AbaDoris, lau si kwa msaada wenu pamoja na shinikizo zenu nisingekamilisha safari hii. Popote mlipo, Mama Doris na mpendwa Mathew 'Gaddafi', sijazisau shime na kani mlizonishushia mara kwa

mara bahari hii yenye mawimbi ilipozidi kuchafuka. Japo sasa hali yenu siijui, moyoni mwangu mliacha alama.

Nisingeweza kutimiza ndoto yangu pasi na ushirika wa walimu na wanafunzi wa shule za msingi zifuatazo: *Precious Gift* – Nairobi, *Nyali*-Mombasa, *Mtakatifu Anna* – Mumias na shule ya malazi ya *Maseno*. Mlinipa matini za kutafiti pamoja na kukubali kuhojiwa. Kitendo chenu ni fadhila kubwa kwangu.

Nachukua fursa hii kuwashukuru walimu na ambao pia ni marafiki zangu wakubwa, waliojitolea kuogelea bahari hii ya drama ya watoto Ndg. Otieno Isaiah, Ndg. Athuman Mohamed Amani, Ndg. Khamis Kanganji, Ndg. Mohamed Tawa, Ndg. Wenceslause Masinde, Ndg. Otieno Nyangla na Ndg. Gabriel Onyango Jura. Bila tamthilia zenu, katu nisingefanikiwa.

Aidha nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioabiri pamoja katika harakati za kuukweya mlima huu wa usomi. Hawa ni Osoro Mogere, Jerono, P., Muthoni Chiuri na Permenus Nzuki. Daima sitasahau wema, ushirika, ushauri na maliwazo yenu ya mara kwa mara.

Naona fahari kubwa kukushukuru wewe Doris Kilonzi kwa kuichapa tasnifu hii kwa ufarisi na maarifa yasiyo kifani. Rabana akurehemu.

Mwisho, na hawa ndio muhimu kuliko wote, vijana wangu Daryl 'Mama' Omoche, Nilcon 'Mzee' Asomba na Wesley 'Gaddafi' Wesonga pamoja na mama yao, Anna kwa mapenzi na utulivu wa nafsi walionionyesha kila wakati nilipozama na kuibuka ndani ya bahari ya vitabu.

**Ahsanteni**

**MUHTASARI.**

Kazi hii inashughulikia tamthilia ya watoto kama zao la michezo au maigizo ya utotoni. Kuna sura tano katika tasnifu hii. Kuna tanbihi mwishoni mwa sura ya kwanza, ya pili, ya tatu na ya nne. Baada ya sura ya tano, kuna orodha ya vitabu vya marejeleo na mwishoni kabisa, viambatisho.

Sura ya kwanza inatanguliza kazi nzima. Katika sura hii, tumeonyesha tatizo la utafiti, kusudi la utafiti, sababu za kuchagua mada hii, mipaka ya utafiti na msingi wa nadharia. Utafiti huu umeongozwa na kanuni za nadharia ya semiotiki ambayo inajishughulisha na ishara na maana ya ishara hizo katika kazi ya kifasihi. Aidha kumeonyeshwa mbinu za utafiti tulizozitumia.

Sura ya pili inashughulikia hali ya michezo au maigizo ya utotoni nchini. Hapa, tumeonyesha ushiriki wa watoto katika michezo ya utotoni, viambajengo vya michezo hiyo na hatimaye tumetoa ufafanuzi kuhusu dhima ya michezo hii maishani mwa watoto.

Sura ya tatu imesheheni uhakiki wa maudhui muhimu katika tamthilia nne teule zilizowasilishwa na watoto wa shule za msingi katika tamasha za drama za mwaka 2002. Tamthilia hizo ni *Tuzo Azizi, Majuto, Monalisa* na *Vososauti.* Tumeonyesha kuwa maudhui yanayoshughulikiwa na tamthilia hizo yana mshabaha na maudhui yanayoshughulikiwa katika michezo ya utotoni. Pia tumemulika ukweli kwamba fasiri ya baadhi ya watunzi ya maudhui hayo haijalingana na urazini wa watoto-lengwa bali i katika mawanda ya watu wazima.

Katika sura ya nne, tumejishughulisha na uchanganuzi wa wahusika pamoja na matumizi yao ya lugha katika tamthilia hizo teule.

Tumebainisha kuwa vipengele hivi vya fani; yaani usawiri wa wahusika na matumizi yao ya lugha, vyote havilingani na urazini wa watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na mitatu.

Sura ya tano ni hitimisho. Katika sura hii, tumetoa maoni yetu kuhusu maswala tuliyoyashughulikia katika tasnifu hii pamoja na kupendekeza njia za kuiboresha drama ya watoto. Aidha, tumetoa mapendekezo ya kufanywa kwa utafiti zaidi.

# SURA YA KWANZA.

## 1.1 UTANGULIZI

Drama ni utanzu wa fasihi ambayo kimsingi hudhamiriwa kuigizwa mbele ya hadhira. Uigizaji huu hufanywa na viumbe ambao aghalabu hutumia lugha. Viumbe hawa huiga mambo yanayopatikana na jinsi yanavyoonekana katika jamii. Lugha ya viumbe hawa kadhalika huingiliana kwa kiasi kikubwa na lugha ya jamii inayohusika.

Maigizo yanapoandikwa, matokeo yake ni tamthilia. Tamthilia inapowasilishwa jukwaani na kuigizwa, inakuwa kitengo cha sanaa ya utendaji.

Maelezo haya yamelandana kwa kiasi kikubwa na sifa za drama ya watoto. Drama ya watoto ni aina kuu na muhimu ya sanaa ya utendaji ya watoto. Chimbuko la drama hii ni michezo ya utotoni au maigizo ya watoto, wenyewe kwa wenyewe. Maigizo haya hufungamana na utamaduni, uchumi na siasa ya jamii inayohusika. Isitoshe, maigizo haya huwasaidia watoto waweze kujifunza mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii yao pamoja na kuzifanyia hali anuwai za maisha yao majaribio (Slade 1973). Kupitia drama, mtoto hupata nafasi ya 'kubaki' mtoto huku akijiburudisha na kujielimisha kwa njia ya kipekee.

Drama ya kileo ya watoto hata hivyo haijapewa uzingativu wa kutosha kama ilivyopewa ile drama ya watu wazima. Ingawa tungo za drama ya watoto hujishughulisha na maswala ambayo watoto wa kisasa hukumbana nayo siku baada ya siku, watunzi wengi wameushindilia utanzu huu hisia za kiutu uzima.

Tasnifu hii imeshughulikia tamthilia zinazosomwa na kuigizwa na watoto ili kuchanganua kama tamthilia hizo zipo katika mawanda ya watoto-lengwa.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI.

Utafiti wetu unahusu uchambuzi wa maudhui na kwa kiasi fani katika drama ya watoto. Uchanganuzi huu utatuwezesha kukadiria kama maudhui katika aina hii ya drama ni yale mambo yanayopatikana katika jamii wanamoishi watoto. Kadhalika, tutatalii usahili wa vipengele vya fani vinavyotumika kuyawasilishia maudhui hayo tukiwa na azima ya kukadiria kama kweli vipengele hivyo viko katika mawanda ya watoto-lengwa.

Kama tulivyodokeza katika utangulizi, drama ya watoto ni zao la michezo ya utotoni. Kwa hivyo, ni lazima drama ya watoto ya kisasa ifumbate matakwa ya watoto kama ilivyo katika michezo hii ya watoto. Drama ya watoto inapaswa kuwa na jambo ilisemalo na jambo hilo litokane na mazingira ya watoto na aidha likuzwe kwa njia ambayo watoto hao wanaitambua.

Kusudi la drama ni kuigizwa jukwaani. Ufanifu wa drama ya watoto kwa hivyo unapaswa kupimwa kwa kuzingatia msingi huu. Kwa vile wahusika huwa nguzo kuu na muhimu ya kukuzia dhamira na kuendelezea maudhui mbalimbali, wahusika ambao wanateuliwa katika drama ya watoto ni lazima wawe wanatambuliwa na watoto wenyewe kwa wenyewe. Yaani, wahusika hao pamoja na maleba ambayo wanayatumia vipatikane katika michezo ya utotoni. Waaidha, lugha watakayoitumia iwe inatambulika katika ulimwengu huo wa watoto.

Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko tumbi kutoka kwa wakereketwa wa drama ya watoto kuhusu tamthilia ambazo husomwa na kuigizwa na

watoto. Alembi katika *"Children are not Miniature Adults" Some Reflections on Primary Schools' Category Scripts' of The Kenya Schools' and Colleges' Drama Festivals* (uk.1), makala aliyowasilisha katika warsha ya watunzi wa drama[1], analalamika kuwa walimu wa drama hawajamwelewa mtoto ni nani. Kutomwelewa huku kumesababisha utata mkubwa kwa sababu watunzi hawa aghalabu wamemtungia mtoto tamthilia ambazo hazimfai. Anaendelea kushauri watunzi hao, kwa utuvu na utuo, waupenye ulimwengu wa mtoto kwa mboni zake mtoto na wala sio zile za kiutu uzima.

Kwa mtazamo mwingine, kwa vile maudhui na fani ni sura mbili za sarafu moja na ni muhali kuzitenga (Senkoro. 1982:1), wandishi, katika harakati zao za utunzi wa tamthilia za watoto, ni bora wamtungiaye aathiri mtungo huo kimaudhui na kifani.

Tatizo letu basi ni kuchanganua tamthilia ambazo watoto huzisoma na kuziigiza hii ikiwa njia ya kuchunguza kama kweli maudhui yanayoshughulikiwa na kadhalika fani itumiwayo kuyawasilishia, vyote vipo katika mawanda ya hao watoto.

## 1.3 KUSUDI LA UTAFITI

Madhumuni yetu ni:

i Kufafanua michezo au maigizo ya utotoni kama awamu mojawapo ya maendeleo ya drama ya watoto.

ii Kuchambua maudhui na fani katika drama ya watoto na kutathmini kama vipengele hivyo viko katika mawanda ya watoto-lengwa.

iii Kuileta drama ya watoto katika jukwaa la kiusomi na kutalii njia za kuiboresha.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII.

Tumechagua kushughulikia drama ya watoto ya kisasa kimaudhui na kifani kwa sababu swala hili bado halijafanyiwa utafiti. Utafiti wetu umelenga kujaza pengo hili.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni ile hamu ya kutaka kuvumbua masuala yanayozingatiwa na watoto katika maigizo au michezo ya utotoni na kadhalika mbinu wanazotumia kuigizia ili kuiwezesha drama ya watoto kupata sifa ambazo zitaweza kuwavutia viumbe hawa ambao wako katika kipindi nyeti na teketeke cha ukuzi.

Utafiti huu una umuhimu wa kipekee kwa vile baada ya kumulika kwa kina udhaifu uliopo katika drama ya watoto ya kileo, papo hapo utatoa changamoto ya utunzi bora wa tamthilia za watoto.

## 1.5 MIPAKA YA UTAFITI

Mpaka leo, tamasha za shule na vyuo ambazo huandaliwa kila mwaka na Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi ndilo jukwaa la kipekee wapewalo watoto walio chini ya miaka kumi na mitatu kuiwasilishia michezo yao ya kuigiza. Mashindano haya huanzia mashinani hadi kiwango cha kitaifa. Utafiti wetu kwa hivyo, umejikita katika zile tamthilia zilizoigizwa katika kiwango cha mkoa na kile cha kitaifa.

Tumechanganua tamthilia nne. Kila moja kutoka mkoa mmoja mmoja kati ya mikoa minane ya Kenya. Tamthilia hizo ziliwasilishwa katika tamasha za mwaka 2002 kama tunavyoonyesha hapa chini.

| Tamthilia | Mkoa |
| --- | --- |
| i. *'Tuzo Azizi'* ya Isaiah Otieno | Nairobi |
| ii. *'Majuto'* ya Amani Athumani | Pwani |
| iii. *'Monalisa'* ya Masinde W.K.E. Wenceslause | Magharibi |
| iv. *'Visosauti'* ya Otieno Nyangla na Masinde W.K.E. Wenceslause | Nyanza |

Tulitamani kufikia mikoa yote minane nchini lakini fedha hazikuturuhusu ndiposa tukachagua kuzuru fainali za mikoa minne; mkoa wa Nairobi, wa Pwani, wa Magharibi na huo wa Nyanza.

Katika uteuzi wa tamthilia hizi na kadhalika walengwa wa kuchunguzwa wakiziigiza jukwaani pamoja na wale wa kuhojiwa, tumeongozwa na imani ya Jackson (1980) kwamba, tamthilia za watoto ni zile ambazo husomwa na kuigizwa na watoto wenye umri hadi miaka kumi na mitatu.

Ili kuuwekea utafiti wetu msingi tisti, timechunguza kwa kifupi michezo au maigizo ya utotoni kama awamu mojawapo ya maendeleo ya drama ya watoto. Tunaongozwa na imani kuwa michezo ya utotoni ndilo jukwaa la kipekee ambalo huwapatia watoto fursa ya kujitungia michezo ya kuigiza na kadhalika kuiigiza michezo hiyo bila usimamizi au mwelekezo wa watu wazima. Maigizo haya ya utotoni yalituwezesha kuupenya ulimwengu wa watoto kwa mboni zao na kuchunguza masuala yanayopatikana katika ulimwengu huo pamoja na fani wanayoitumia kuyawasilishia.

Hatukushughulikia vipengele vyote vya fani katika tahakiki yetu hii. Tumechanganua wahusika na matumizi yao ya lugha pekee. Kuhusu

wahusika, tumeangaza uteuzi na kadhalika usawiri wao tukiwa na azima ya kuonyesha kama kweli viumbe wanaopatikana katika drama ya watoto ya leo wanatambulikana katika ulimwengu wa watoto.

Kwa vile fasihi ni kazi ya sanaa inayowasilisha maudhui yake kwa kutumia lugha ya maneno, tumeichambua lugha ambayo wahusika hawa wanaitumia. Sababu ni kwamba, mawasiliano yatakamilika tu ikiwa wanaowasiliana watayaelewa na kuyatambua maneno wanayoyatumia. Yaani, ni muhimu mazungumzo yanayokuzwa katika drama za watoto yakaribiane sana na uhalisi wa jinsi watoto wanavyotumia lugha katika maigizo au michezo yao ya utotoni.

Labda itahofiwa kuwa ushughulikiaji wa vipengele viwili pekee vya fani na kupuuza vile vingine umedhoofisha kazi hii. Ukweli ni kwamba, umeiimarisha. Utanzu wa fani ni mpana sana. Unajumlisha vipengele kama vile: muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika na mandhari. Kushughulikia wahusika na matumizi yao ya lugha pekee bila shaka kumetupa muda wa kutosha kuchambua tamthilia zinazoigizwa katika drama ya watoto kwa kina.

## 1.6 NADHARIA TETE.

Nadharia tete za kimsingi katika utafiti huu ni:

i Ingawa maudhui katika tamthilia za drama ya watoto yamejengeka kwenye matukio yanayohusiana na mazingira ya watoto-lengwa, maudhui hayo hayako katika mawanda yao.

ii Usawiri wa wahusika katika drama ya watoto pamoja na lugha wanayoitumia havipo katika mawanda ya watoto-lengwa.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII.

Ingawa kuna chambuzi nyingi zishughulikiazo tamthilia ambazo zimekwisha chapishwa, kazi zinazoshughulikia drama ya watoto ni chache mno.

Alembi (khj) analalamika kwamba waandishi wamtungiaye mtoto tamthilia kamwe hawamwelewi mtoto huyo. Kutomwelewa huko kumesababisha hali ya mtoto kuigiza michezo iliyo juu ya ung'amuzi wake. Makala haya hata hivyo, hayachambui tamthilia hizo. Kadhalika, ingawa makala hayo yanatoa mchango mkubwa kwa utafiti wetu, Alembi hakutumia mikakati ya kitaalamu katika kuufikia huo uamuzi wake. Uchambuzi wetu, kwa kutumia mikakati ya kitaalamu, utachanganua tamthilia zinazoigizwa katika drama ya watoto katika tamasha za shule na vyuo ili kumulika udhaifu wazo kimaudhui na kadhalika kifani.

Kabui (1997) amefanya utafiti kuhusu hadhi ya thieta ya watoto jijini Nairobi. Aligundua kwamba, thieta za Nairobi hazilengi watoto. Watoto hujihusisha tu katika drama shuleni mwao wakati wa tamasha za shule na vyuo au katika hafla za siku ya wazazi. Hata hivyo, kiploti, michezo wanayoiigiza imepita kiwango chao cha ung'amuzi. Utafiti huu haukujishughulisha na maudhui na hapo kupuuza umuhimu wa thieta kama chombo cha kufunzia watoto maadili. Waama, utafiti huu ulimega sehemu kubwa sana. Utafiti wetu umebobea tathmini ya maudhui na kadhalika fani. Isitoshe, tumejikita katika tamthilia zinazoigizwa na watoto katika tamasha za shule na vyuo peke yake na hapo kuufanyia utanzu huu uchambuzi wa kina.

Katika makala yake, *Fasihi Simulizi na Uandishi Katika Shule Za Msingi* (1978)[2] Kamera anasisitiza umuhimu wa fasihi ya watoto. Anasema kwamba watoto wana uwezo sio tu wa kufurahia bali pia wa kushirikishwa katika utunzi wa fasihi yao. Ni wazi kutokana na mawazo haya kwamba, Kamera alipoandika makala haya hakukuwa na fasihi

'nzuri' kwa watoto nchini Tanzania. Hii pia ndiyo tuhuma yetu kuhusu tamthilia wanazoigiza watoto humu nchini. Utafiti wetu kwa hivyo, umepiga hatua zaidi. Umelenga drama ya watoto nchini kwa kumulika udhaifu wa tamthilia zinazoigizwa na watoto kisha tumeweza kuwashirikishwa watoto katika kupendekeza jinsi ya kuziboresha tamthilia hizo.

Mpesha (1995) katika utafiti wake kuhusu fasihi ya watoto nchini Tanzania, alikusanya maoni ya kila nui kutoka kwa watoto kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi wanayotungiwa. Lakini anakiri kwamba, katika utanzu wa drama ya watoto, hakukuwa na kazi yoyote iliyokuwa imechapishwa katika Kiswahili wala watoto hao hawakuwa wakishirikishwa katika mashindano ya drama kama ilivyo humu nchini. Tasnifu yetu imepiga hatua zaidi, kwa sababu tumechambua tamthilia zinazoigizwa katika drama ya watoto kwa utondoti na kutoa peupe udhaifu wazo. Hatua hii, bila shaka, itatoa changamoto zinazohitajika kukuzia utunzi wa tamthilia mwafaka kwa watoto nchini.

Kiango (1980) anadai kwamba chimbuko la maigizo ya watoto tuyaonayo leo ni michezo ya utotoni[3]. Madai yake haya hayasaidii vya kutosha kuchochea utunzi wa tamthilia mwafaka kwa watoto. Utafiti wetu umeangazia watunzi chipukizi wa tamthilia za watoto 'ulimwengu wa watoto' ambamo maudhui yafaa yaibukie. Isitoshe, haja ya kutumia fani sahili kama ilivyo katika michezo ya utotoni imesisitizwa.

Lewis katika Fox (1976) na Siks (1977) wamejadili maudhui katika drama ya watoto. Wanadai kuwa kila hirimu ya watoto ina mtazamo tofauti wa maisha. Kwa hivyo, utungo ni lazima uzingatie maudhui yenye kuivutia hirimu hiyo. Siks anapendekeza drama bunilizi ya kifantasia au kinjozi kwa watoto wa miaka sita; hadithi mbabe kwa watoto wa miaka minane hadi kumi na mmoja. Nao watoto wa miaka kumi na miwili, kwa vile ni wadhanifu mno, anapendekeza kuwa watavutiwa zaidi na drama yenye wahusika walio na nguvu ajabu, ujasiri pamoja na uwajibikaji na

ambao wataweza kutatua matatizo makubwa makubwa. Uainishaji huo wa kimaudhui kwa hirimu mbalimbali umetufaa kiasi kwa vile unathibitisha ukweli kwamba drama ya watoto ni lazima ibobee raghba za watoto.

Wamitila (2002) ameshughulikia uhakiki wa tamthilia kwa kina. Ingawa ametaja vitengo vya uhakiki kijumla, maelezo yake yametufaa jazila kuchanganua tamthilia za drama ya watoto.

## 1.8 MSINGI WA NADHARIA.

Uhakiki wetu wa tamthilia zinazoigizwa katika drama ya watoto umeongozwa na kanuni za nadharia ya semiotiki. Baadhi ya wahakiki huiita nadharia ya umatini kwa sababu ya mwelekeo wake wa kupendelea neno "matini" kuielezea kazi ya kifasihi badala ya neno "kazi".

Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa na miaka ya 1970 ambapo mwelekeo mkubwa wa kuuasi umuundo ulikuwa umeshika kani. Hivi leo, nadharia hii inahusishwa zaidi na wahakiki kama Umberto Eco, A.J. Greimas, T. Todorov na Roland Barthes (Elam 1980). Kwa maoni yetu, mawazo ya Barthes ndiyo yaliyoacha athari kubwa na kuiwekea misingi mikuu nadharia hii ya semiotiki.

Nadharia hii inashughulikia ishara na uashiriaji katika kazi ya kifasihi. Inamulika jinsi kazi za kifasihi zinavyowasiliana na wasomaji; yaani jinsi msomaji wa matini fulani ya kifasihi anavyoifasiri kazi anayoisoma. Waaidha, semiotiki humulika usomaji wetu wa kazi za kifasihi na kujiuliza kwa nini kazi hizo zina maana zilizo nazo kwa wasomaji wake.

Kwa vile semiotiki inajishughulisha na ishara na uashiriaji na kwa vile Alembi anadai kuwa mtoto si mtu mzima mdogo,[4] ni wazi kwamba,

ulimwengu wa mtoto unatofautiana kwa kiwango fulani na ule wa mtu mzima. Wakati huu ndipo mtoto ameanza kubobea katika maisha. Kwake, mambo mengi ya ulimwenguni ndipo anayaona kwa mara ya kwanza. Kwa hivyo, huenda ikawa yeye huyaona mambo mengi kwa wakati mmoja. Mengi ya mambo hayo, yamkini, huenda watu wazima wameyaona kwa muda mrefu mpaka wameyazoea na sasa kwao ni mambo ya kawaida.

Mpaka hapa, ni wazi kwamba ishara na uashiriaji katika ulimwengu wa mtoto unatofautiana kwa kiwango fulani na vile ilivyo katika ulimwengu wa mtu mzima. Kuuelewa ulimwengu wa mtoto basi, inabidi kuelewa maana ya ishara anazotumia kuashiria. Kwa vile ishara na uashiriaji katika drama ya watoto kwa kiasi kikubwa huonekana kupitia kwa wahusika pamoja na lugha wanayoitumia, nadharia hii imetufaa katika uhakiki wa wahusika pamoja na matumizi yao ya lugha. Vipengee hivi vya fani tumevichambua huku tukivizingatia kama ishara ambazo watoto hutumia kuwasiliana.

Barthes (Elam 1980) alizua dhana msimbo ambapo alipendekeza njia bora ya kuisoma matini ya kifasihi. Mhakiki huyu anaamini kuwa matini ya kifasihi lazima ivunjwevunjwe kwa vitengo vidogo vodogo vya kiusomaji vyenye urefu sawa alivyoviita *leksia*. Kila *leksia* hapa itadhihirisha misimbo fulani ambayo itakuwa muhimu katika kuifasiri matini hiyo.

Utafiti wetu umefaidika kutokana na mawazo haya kwa sababu, ili mtoto aweze kuelewa maudhui ya tamthilia, tunaamini kwamba ni lazima maudhui hayo yawasilishwe kwa vipimo vidogovidogo kama vile apewavyo dawa mgonjwa.

Wamitila (2002) anaendelea kuthibitisha kuwa, Barthes alitambua aina tano kuu za misimbo ya usomaji. Msimbo wa matukio unahusu mtiririko wa matukio kiathari au kisababishi. Pili, kuna msimbo unaohusu

taharuki ambao aliuita msimbo wa kihemenitiki. Aliamini kuwa taharuki ni lazima ifumbatwe kwenye anwani ya kazi ya kifasihi. Tatu ni msimbo unaohusiana na jinsi msomaji anavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Msimbo huu aliuita wa kiseme. Msimbo wa nne ni wa kiishara ambao unahusishwa na jinsi wasomaji wanavyovumbua maana za ishara katika kazi za fasihi. Tano, kuna msimbo wa kirejelezi. Msimbo huu huipa kazi fulani nguzo za kitamaduni kwani urejelezi huu huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji. Msomaji anaposema anaelewa akisemacho mwandishi huwa anasema hivi kutokana na viashirii vya msimbo huu.

Mawazo haya ya Barthes ni muhimu. Msimbo wa kiseme umetusaidia kuchanganua jinsi mtoto anayeisoma tamthilia atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Nao msimbo wa ki-ishara na ule wa kirejelezi imetuwezesha kuvumbua maana ya ishara ambazo hupatikana katika ulimwengu wa mtoto huku tukiwa na imani kwamba ulimwengu huo una utamaduni wake ambao uko tofauti na ule wa ulimwengu wa mtu mzima.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI.

Data tuliyoitumia katika utafiti huu tuliipata nyanjani na pia maktabani.

Maktabani, tumezidurusu tamthilia nne zilizoigizwa katika tamasha za drama ya shule na vyuo katika kitengo cha mkoa (Taz. 1.5). Hali kadhalika, tumesoma vitabu na makala mbalimbali ambayo yanahusu drama ya watoto na uchambuzi wa tamthilia kwa jumla. Kazi hizi zimetusaidia kukadiria kitaalamu kama tamthilia walizosoma na kuziigiza hao watoto zilikuwa katika mawanda yao.

Nyanjani, tulitumia vifaa vifuatavyo kukusanyia data ya utafiti wetu:-

i. Uchunguzi wa nyanjani.

ii. Hojaji

### 1.9.1 Uchunguzi wa Nyanjani.

Tulitazama maigizo ya utotoni katika shule za msingi teule. Shule hizo ni shule ya *Precious Gift* kutoka mkoa wa Nairobi, ya *Nyali* mkoani Pwani; ya *Mtakatifu Anna-Mumias* kutoka mkoa wa Magharibi na hatimaye shule ya msingi ya *Maseno* kutoka mkoani Nyanza. Madhumuni yetu yalikuwa kuchunguza masuala yaliyoshughulikiwa katika maigizo hayo, uteuzi wa wahusika na lugha waliyoitumia wahusika hao.

Tamthilia tulizohakiki (Taz.1.5) vile vile zilichunguzwa zikiigizwa jukwaani katika mashindano ya shule na vyuo. Tulitazama maigizo ya tamthilia hizo ili tuweze kutathmini kama maudhui yazo yalikuwa yametolewa kutoka kwenye mazingira ya watoto kama tulivyoshuhudia katika maigizo ya utotoni. Aidha, tulitupia uteuzi wa wahusika na lugha waliyoitumia jicho-chunguzi ili kitathmini kama vipengee hivyo vya fani viko katika mawanda ya watoto-lengwa.

### 1.9.2 Hojaji.

Seti mbili za hojaji zilitumika:

a) ***Hojaji ya Wanafunzi*** (Kiambatisho 1A).

Sampuli ya watoto waliohojiwa ni wale walioigiza tamthilia ambazo tumezitaja (1.5). Tuliwateua kwa vile wao ndio waliozisoma na kuziigiza tamthilia hizo. Tulitumia hojaji yenye maswali wazi na tuliwahoji wanafunzi ishirini kutoka kila shule. Hii ni idadi wakilishi kwa vile kila

shule iliwakilishwa na waigizaji wasiozidi thelathini na watano. Wanafunzi hawa walikuwa na umri kati ya miaka sita na kumi na mitatu. Katika hojaji hii tumedhamiria kushawishi ujumbe kuhusu:

i Kiwango cha ushiriki wa watoto katika uigizaji wao, wenyewe kwa wenyewe.

ii Athari ya tamthilia wazisomazo na kuziigiza katika maisha yao.

iii Maoni ya watoto kuhusu jinsi ya kuboresha drama yao.

b) ***Hojaji ya Watunzi/Walimu*** (kiambatisho 1B)

Tuliwahoji walimu na wanasanaa waliotunga na kuwasilisha tamthilia ambazo tumezihakiki kwa uigizaji. Katika hojaji hii, tunalenga ujumbe ufuataο:-

i Tajiriba ya mtunzi katika utunzi wa tamthilia za watoto.

ii Masuala ajishughulishayo nayo katika utunzi wake.

Iii Matatizo ambayo humkabili katika harakati zake za kuwatungia watoto tamthilia.

iv Maoni yake kuhusu jinsi ya kuboresha drama ya watoto.

**TANBIHI.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Taz E. Alembi (2003) | - | Makala haya hayajachapishwa. |
| 2. | Taz. Kamera (1978) | - | Makala haya yaliwasilishwa katika kongomano la *Mwaka* Wa *Vijana 1979* |
| 3. | Taz. Omari, C.K. na Mvungi, M (1980) | - | *"Maendeleo ya Michezo ya Kuigiza"* Makala katika *Urithi wa Utamaduni Wetu.* |
| 4. | Kama hapo juu | - | Uk. 1 |

# SURA YA PILI

## HALI YA MICHEZO YA UTOTONI NCHINI.

### 2.1 UTANGULIZI.

Sura hii itashughulikia michezo au maigizo ya utotoni kama awamu mojawapo ya maendeleo ya drama ya watoto. Uchunguzi wetu umeongozwa na imani kwamba, michezo ya utotoni ina uamilifu mkubwa maishani mwa watoto na ili watunzi wa drama ya watoto waweze kuwatungia watoto tamthilia zilizo katika mawanda yao ya ung'amuzi, ni bora watunzi hao waelewe umbo na kadhalika muundo wa michezo ya utotoni.

Sehemu hii kwa hivyo, itashughulikia kwa kina ushiriki wa watoto katika michezo ya utotoni, viambajengo vya michezo hii na hatimaye kutoa ufafanuzi kuhusu dhima ya michezo au maigizo haya maishani mwa watoto.

### 2.2 MICHEZO YA UTOTONI.

Maigizo ya utotoni ni mojawapo ya michezo muhimu maishani mwa watoto. Michezo hii huigizwa na watoto wenye umri kati ya miaka miwili na nusu na miaka kumi na miwili. Siafu D. Kiango anafafanua kwamba:

> Wengi wetu tulipokuwa watoto wadogo tuliingia katika ulimwengu wa michezo hata bila kujua kwamba tulikuwa tunafanya michezo ya kuigiza. Jambo tu ambalo tulifahamu ni kwamba *tulikuwa tunaigiza maisha ya kila siku ambayo tulikuwa tunayaona.*
>
> *(msisitizo wetu)*

Maoni haya ni ithibati kwamba chimbuko la drama ya watoto ni michezo ya utotoni. Watoto, kupitia kwa michezo hii, hupata fursa ya kumithili

nafsi mbalimbali katika ulimwengu wao dhanifu. Msingi wa umithilinafsi huo huwa umejikita katika uigaji wa hali anuwai za maisha ya kila siku. Kwa mfano, watoto wataigiza maisha ya nyumbani au ya shuleni kulingana na jinsi wanavyoyaona. Katika kuiga maisha ya nyumbani, watoto wataishi katika hali ya kinyumba ambapo kuna bwana, mke na watoto. Waaidha, wataweza kuiga wahusika bunilizi au dhahania kutoka katika mazingira ya leo yaliyoghoshi vitimbi.

Kulingana na Gross katika Courtney (1974), 'azma pekee ya utotoni ni kupata fursa ya kucheza'. Mtoto kwa hivyo, hujidaia nafasi ya kumithili hali anuwai azionazo katika mazingira yake wala hangojei kupewa nafasi hiyo. Kama ambavyo mwana wa kuku hafunzwi kuchakura, mtoto hafunzwi kuigiza. Satua ya kuigiza alizaliwa nayo.

Msimamo wetu huu umetiwa kani na Victor D' Amilo katika (Siks 1958:7) anaposema kuwa 'kila mtoto amejaliwa kipaji kisicho dhahiri cha usanii-tendi'. Maoni haya ni ithibati zaidi kwamba katika michezo yao ya utotoni, wafanyacho watoto ni kuteka mbinu za uigizaji kutoka kwenye bwawa la hekima walilojaaliwa na kuzitumia kutafsiria hisia zao au kumithilia maisha ya kila siku jinsi wanavyoyaona. Hii ndiyo sababu Davies (1983) anadai kwamba kila mtoto azaliwapo huwa amemiliki mbinu muhimu na za kimsingi zinazohitajika katika drama.

## 2.3 USHIRIKI WA WATOTO KATIKA MICHEZO YA UTOTONI.

Ili kukadiria kiwango cha ushiriki wa watoto katika maigizo au michezo ya utotoni, watoto wapatao themanini kutoka shule nne tofauti za msingi walihojiwa. Kila moja ya shule hizi ilikuwa imewasilisha tamthilia kwenye mashindano ya mkoa ya shule na vyuo (Taz.1.5). Watoto waliohojiwa ni wale walioshiriki katika maigizo ya tamthilia hizo jukwaani.

Jedwali (2.1) lifuatalo linaonyesha matokeo ya hojaji kwa wanafunzi *(Kiambatisho 1A).*

**Jedwali 2.1**

**Ushiriki wa Watoto katika Michezo ya Ut**

| SHULE | PRECIOUS GIFT | NYALI PRI. | ST.ANN-MUMIAS |
|---|---|---|---|
| Asilimia ya watoto waliohojiwa | 68 | 72 | 93 |
| Jina la michezo waliyoshiriki | At Home, Bank Robber, Paka Mshike Panya, Naughty Pupil, Commando, Guess Who? Hide & Seek, Mababi na Makarau, Doctor Doctor | Kalongolongo, At School, Army-Navy, Bank Robber Paka Mshike Panya, Guess Who? Commando, Hide & Seek , Mababi na Makarau, Doctor Doctor | Kalongolongo, Teacher Teacher, Doctor & Patient, Paka Mshike Panya, Let's Prete Hide & Seek, Police & Robbers |
| Nafasi walizoigiza | Baba, Mama Daktari, Mbabe Askari, Jambazi, Mwanafunzi, Mwalimu, Dereva | Baba, Mama Daktari, Mwanajeshi, Jambazi, Mbabe Askari, Mwalimu Mwanafunzi, Dereva | Baba, Mama, Daktari, Mbabe, Mgonjwa, Mtoto, Mwanafunzi, Mw Polisi, Jambazi |
| Asilimia ya watoto waliyoifurahia michezo ya utotoni | 80 | 88 | 90 |
| Sababu ya kuifurahia | • Huchekesha<br>• Hufunza juu ya maisha<br>• Hupatia madaraka<br>• Kuwaadhibu majambazi | • Hufunza jinsi ya kuishi pamoja vizuri.<br>• Hufurahisha<br>• Kuishi kama mtu mzima<br>• Kuwaadhibu majambazi | • Hufunza juu y maisha.<br>• Hufurahisha<br>• Hufunza kazi mbalimbali. |

Katika jedwali 2.1, tunaona kwamba watoto wengi hushiriki katika michezo au maigizo ya utotoni. Takriban kila mtoto aliyehojiwa kutoka shule ya *Mtakatifu Anna-Mumias* (Mkoa wa Magharibi) na ya *Maseno* (Mkoa wa Nyanza) hushiriki katika michezo hiyo.

Watoto wengine hasa kutoka shule zilizo mijini (*Precious Gift* – Nairobi na *Nyali*- Mombasa) hawashiriki katika michezo hii bia kwa sababu mbalimbali. Wachache walikiri kwamba walipendelea kutazama michezo kwenye runinga kuliko walivyopendelea kujihusisha katika uigizaji. Shule hizi kadhalika zilikuwa na vifaa vingine vya burudani kama vile tarakilishi ambavyo huwavutia watoto wakati wa mapumziko. Desturi ya kusoma vitabu vya hadithi wakati wa mapumziko aidha imeshamiri katika shule hizi kiasi cha watoto kuiona michezo hii kama ni upotezaji wakati.

Asilimia 12.75 ya watoto waliohojiwa hawakufurahia michezo hii. Sababu kuu waliyopeana ni kuwa sehemu waliyopewa kuigiza haikuwavutia. Sehemu kama hizo ni kama vile kuigiza kijakazi au mlinzi wa kibinafsi au ya kujifanya gari ili 'aendeshwe' na mtoto mwingine.

Masuala yanayoshughulikiwa katika michezo hii ya utotoni yanaweza kujumulishwa katika migawo ifuatayo: masuala ya nyumbani, ya shuleni, ya hospitalini na yale ya mijini.

### 2.3.1 Masuala ya Kinyumbani.

Michezo ambayo imeshughulikia masuala ya watoto majumbani mwao imepewa anwani tofauti tofauti kulingana na mazingira kama vile: *At Home* (Nairobi) na *Kalongolongo* (Mazingira ya Mombasa na yale ya shule za mashambani). Japo anwani yazo ni tofauti, michezo hiyo inamulika migogoro ya kinyumbani kupitia kwa mboni za watoto. Kwa mfano,

katika michezo hizo, mama hubaki nyumbani kuwalea watoto pamoja na kupika. Baba hushinda kazini na pia ana gari. Anaporudi nyumbani, anapokewa na mkewe pamoja na watoto. Jambo la kwanza analouliza ni chakula. Iwapo ataambiwa kuwa chakula hakikuwa tayari, atalalamika na kumlaumu mkewe kwa uvivu. Aghalabu mke atalalamika kuwa bwana hakuacha pesa za chakula. Papo, baba atatoa pesa ili chakula kinunuliwe.

### 2.3.2 Masuala ya Shuleni.

Michezo ambayo imesheheni maisha ya shuleni jinsi wanavyoyaona watoto ni: *Naughty Pupil*, *At School*, na *Teacher Teacher*

Michezo hii inawahusisha walimu, wanafunzi, viranja na kadhalika wazazi kwa madhumuni ya kumkashifu mwanafunzi mtoro. Mandhari ni ya darasani ambapo mwalimu anafundisha. Mwalimu anawaadhibu wanafunzi waliofanya makosa kwa viboko. Mwanafunzi mmoja mtukutu anakataa adhabu hiyo kisha anatoroka shuleni. Baadaye, anarejeshwa shuleni na mzaziwe. Mzazi anamkashifu mwanawe na kumwomba mwalimu amsamehe na kumruhusu asome. Mwalimu anakubali lakini baada ya mtoto huyo kuchapwa viboko maradufu kadamnasi ya wenzake.

Mchezo huu huvutia watoto sana. Hali hii hutokana na uwezo wa mwigizaji kumshabihi mwalimu wake kikwelikweli. Ushabihikweli huu ndio huupa mchezo wenyewe uhalisia wenye mnato.

### 2.3.3 Masuala ya Hospitalini.

Watoto huogopa sana mandhari ya hospitalini. Uigizaji wa maswala ya hospitalini kwa hivyo huwapa watoto ujasiri wa kukabiliana na daktari

pale wanapougua. Kisa kinachojenga masuala hayo huanza na ajali ya barabarani. Mwanafunzi anagongwa na gari anapovuka barabara kuelekea shuleni. Mwenye gari anasaidiwa na watoto wengine kumpeleka hospitalini. Huko hospitalini anatibiwa na daktari baada ya mwenye gari kulipa pesa nyingi.

Michezo inayojenga masuala haya ni *Doctor Doctor* na *Doctor & Patient*. Mafunzo makuu kwa watoto ni kuwa wawe waangalifu barabarani na kadhalika wawe wasamaria wema wa kuweza kumsaidia yeyote ambaye atahitaji usaidizi.

### 2.3.4 Masuala ya Mijini.

Maisha ya mijini kwa mboni za watoto yameghoshi wizi na ujambazi. Hali hii inajidhihirisha kupitia kwa michezo inayoitwa *Bank Robber* na *Mababi na Makarau* na *Police & Robbers*.

Katika michezo hii, mapambano kati ya shujaa chanya (Makarau au Polisi) na shujaa kinzani (Mababi au Majambazi) hushamiri baada ya wezi kuvamia benki na kupora pesa nyingi. Polisi wanawasaka kichakani walikojificha. Polisi wanajificha kwa kujifunga nyasi mwilini na kuwavizia. Marushiano makali ya risasi yanazuka lakini hatimaye aidha majambazi 'wanauawa' au wanatiwa mbaroni.

### 2.3.5 Masuala ya Kibunilizi.

Kama tulivyoona hapo kabla, watoto walio na umri chini ya miaka kumi na miwili ni wadhanifu mno na wanavutiwa na drama yenye wahusika walio na nguvu ajabu, wenye ujasiri na uwajibikaji na ambao wataweza kutatua matatizo makubwa makubwa (Siks. 1977). Wahusika kama

hawa aghalabu hupatikana katika vipindi vya runinga au kwenye maonyesho ya sinema.

Michezo kama *Guess who? Hide and Seek, Commando* na *Army-Navy* ndio uwanja wanaoutumia watoto hasa wale kutoka mijini kupalilia vipawa vyao vya ubunifu. Kwa vile katika mazingira yao upatikanaji wa vyombo vya kisasa vya burudani ni rahisi, mababe kama vile *Superman, Commando, Ronaldo* (mwanakandanda), Schumacher (bingwa wa magari ya langalanga) na hata watangazaji katika runinga huigwa. Kwa mfano, mtoto anayedhamiria kumwiga mtangazaji wa runinga kama vile *Emanuel Juma* au *Swaleh Mdoe*[1] atachukua kisanduku kilichotobolewa shimo upande mmoja. Ataupenyeza uso wake katika kishimo hicho huku akitangaza jinsi ambavyo shujaa wake hufanya. Mwishowe, atawauliza waliokuwa wakimsikiza kukisi yeye alikuwa nani.

## 2.4 VIAMBAJENGO VYA MICHEZO YA UTOTONI.

Viungo mbalimbali vinajumuishwa ili kuisimamisha sanaa ya utendaji ambayo inajulikana kama michezo ya utotoni. Miongoni mwa viungo hivyo muhimu ni: ploti, maudhui, wahusika na mandhari.

### 2.4.1 Ploti.

Kama tulivyogusia hapo awali, licha ya kwamba michezo ya utotoni huigizwa na watoto wenye umri usiozidi miaka kumi na miwili na aidha, watoto hao huiga maisha ya kila siku jinsi wanavyoyaona, michezo hii haina miswada iliyoandikwa. Watoto hujikusanya, na baada ya kukubaliana juu ya mchezo watakaouigiza, uigizaji huanza.

Visa katika michezo hii hukunjuka kwa kasi na hudhihirika waziwazi kwa mwigizaji na hata mtazamaji. Aidha mwanzo na mwisho wa mchezo

hudhihirika kwa kila mhusika. Kwa mfano, kisa cha *Makarau na Mababi*, huanza majambazi wanapovunja benki na kupora pesa. Polisi watawasaka hadi wawakamate na wawangamize wote kwa bunduki, kisha mchezo utakamilika.

Kila mhusika katika michezo ya utotoni hutarajiwa kubuni maneno atakayosema pamoja na vitendo vitakavyoandama maneno yake. Kwa hivyo, mwigizaji huwa na wajibu wa kubuni huku akiendelea kuigiza. Kipawa cha kubuni atakihitaji wakati wa kutafsiria hisia zake na kadhalika wakati wa kumithili maisha ya kila siku jinsi anavyoyaona.

### 2.4.2 Maudhui

Maswala yanayoshughulikiwa katika michezo ya utotoni yameathiriwa sana na mazingira wanamochipukia watoto; yaani yamejengeka kwenye matukio ambayo watoto hukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku.

Kwa vile viumbe wa kwanza maishani mwa watoto aghalabu huwa ni wazazi pamoja na wale wote wajengao aila yao, maisha ya nyumbani huwa suala muhimu la kushughulikiwa. Katika maigizo haya kwa mfano, iwapo baba ni mkali, basi mvulana anayeiigiza sehemu hiyo naye ataonyesha ukali. Kama kuna ugomvi wa mara kwa mara nyumbani kwao, jambo hili aidha litajitokeza. (Taz. *At Home* na *Kalongolongo*)

Hali ilivyo shuleni ni suala lingine muhimu katika ulimwengu wa watoto. Sababu ni kwamba, kwa muda mwingi (kati ya masaa manne na manane) watoto huwa shuleni. Maingiliano kati yao na walimu, watoto wenzao na kadhalika wazazi wao huzua mambo mengi ya kumithili. (Taz. *Naughty Pupil. Guess who?* Au *Let's Pretend, Teacher Teacher*)

Watu wa amali zifuatazo ndio aghalabu hupatikana katika ulimwengu wa watoto kuliko wengineo: walimu, askari, daktari na wauguzi, dereva na rubani. Yamkini watoto hukumbana na watu hawa kwa hali moja au nyingine au wao huthamani amali hizo katika mustakabali wao. Mtazamo wa watoto kuhusu kazi hizi huzua masuala nyeti ya kushughulikiwa. (Taz. *Doctor Doctor* au *Doctor & Patient, Teacher Teacher, Mababi na Makarau* au *Police & Robbers, Army – Navy*).

Watoto wanapenda maisha yenye vitimbi zaidi ya maisha yaliyo teketeke. Maudhui ambayo yamesheheni michezo yao kwa hivyo, ni yale ambayo huzunguka maisha ya mababe na majagina kama vile wacheza filamu hodari, wanamichezo wanaosifika na hata vibonzo vya runinga ambavyo huvusha watoto hadi ulimwengu wa kinjozi ambao una uwezo wa kuchachawa damu yao. (Taz. *Commando, Guess who?* Au *Lets Pretend, Army-Navy*).

### 2.4.3 Wahusika.

Viumbe ambao hupatikana katika maigizo ya utotoni huchaguliwa na watoto wenyewe kwa wenyewe. Sifa za nje pamoja na masuala yanayodhamiriwa kukuzwa na mchezo fulani huwa ndiyo dira iwaongozayo katika uteuzi wa wahusika.

Katika kukuza na kuendeleza maudhui ya kinyumbani kwa mfano, wasichana huchukua nafasi ya mama nao wavulana ile ya baba. Watoto wadogo kwa kimo au umri hujifanya kuwa watoto wa familia hiyo. Ikiwa kuna mtoto mcheshi (ni nadra akosekane), ataicheza nafsi ya mifugo hasa jogoo wa kuiamsha aila hiyo.

Japo watoto hujichagulia nafasi za kuigiza, ni nadra wasichana kuchagua nafasi kama vile daktari, rubani, askari na dereva kama wavulana wapo. Taasubi hii tumegundua imekita mizizi yake katika

mazingira ambayo hulea watoto wala si jambo linaloanza katika utu uzima wao.

### 2.4.4 Mandhari.

Kulingana na Wamitila (2002:27), mandhari ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Anaendelea kujumulisha elementi hizo za mandhari katika migawo mitatu. Migawo hiyo ni: eneo la kijiografia, amali za wahusika pamoja na desturi za maisha yao ya kila siku na hatimaye, wakati ambapo tukio fulani linatendeka.

Kijielezi hicho cha Wamitila pamoja na ufafanuzi wake vimewekea uchanganuzi wetu wa mandhari ya maigizo ya watoto nguzo halisi. Tunatumia 'eneo la kijiografia' katika usahili wake kumaanisha jukwaa pamoja mazingira yanayosawiriwa na mchezo.

Pili, tumemega kibendo cha amali ya wahusika kwa kutumia maleba kufafanulia desturi za maisha ya wahusika ya kila siku. Tumepuuza maelezo ya wakati kwa sababu michezo ya utotoni haipo katika kiwango cha kuhitaji misingi ya kihistoria na kiwakati. Hebu tufafanue maleba na jukwaa la michezo ya utotoni zaidi.

#### 2.4.4.1 *Maleba katika Michezo ya Utotoni.*

Katika kuteua maleba ya kusawiria wahusika na kadhalika hali anuwai zinazoigizwa, ufaragusi sahili hufanywa. Kwa mfano, msichana anapofunga leso juu ya sare ya shule tayari anageuka na kuwa mama. Kadhalika, mvulana avaapo bleza, anakuwa baba. Barakoa au vizuizui pia hutumiwa kama kuna haja ya kuiga mnyama kama vile sungura ama simba. Katika kupika, watoto hutumia vifaa kama vyungu na mchanga kama chakula; majani ndiyo yanayotumiwa kama mboga;

vipande vya karatasi ndizo pesa navyo vijiti hutumika kama panga au sindano.

### *2.4.4.2 Jukwaa katika Michezo ya Utotoni.*

Uigizaji wa michezo ya utotoni hauna jukwaa maalumu wala sheria mithaki; kilichoko ni nafasi unde. Hii ni nafasi ambayo huchukuliwa na waigizaji pamoja na watazamaji kutekelezea juhudi za kuigiza na kutazamia maigizo. Nafasi hii unde huenda ikawa ni nje kama vile kwenye barabara, kwenye bustani, au uwanjani. Nafasi hii huundwa na watoto wenyewe kwa wenyewe kwa minajili ya maigizo yao. Kuhusu jukwaa la aina hii, Courtney (1974:15) anasema kuwa:

> Mipangilio ya aina hii ni ya kimajaribio tu na
> huenda isiwe na umuhimu wowote wa kijumla
> (Tafsiri yetu)

Ingawa mpangilio wa maigizo ya utotoni huenda ulitokana na juhudi za kimajaribio, si kweli kwamba jukwaa hili halina umuhimu wowote. Nafasi unde aghalabu huwaleta pamoja waigizaji na hadhira yao kwenye mazingira ambayo hayajazoelewa na hivyo kuwaweka wote kwenye ngazi sawa inayosaidia sana katika ushirika wao.

Nafasi kama hii hutumiwa sana na watoto wanapoigiza maisha ya kila siku jinsi wanavyoyaona. Katika jukwaa hili kwa mfano, nyumba hujengwa kwa mchezo wa nyumbani kama vile katika *Kalongolongo* au *At Home* nalo korokoro la kuzuilia wafungwa katika mchezo wa *Makarau na Mababi* au *Bank Robber*. 'Majengo' hayo aghalabu hubomolewa baada ya kutimiza wajibu wake ingawaje katika shule zingine, nyumba za kudumu miezi mitatu (muhula mmoja) hujengwa na watoto hao wenyewe kwa minajili ya michezo hii.

## 2.5 DHIMA YA MICHEZO YA UTOTONI MAISHANI MWA WATOTO.

Teneti za nadharia ambazo zimewasilishwa kuhusu michezo zimethibitisha umuhimu wa kucheza katika maisha ya mtoto. Nadharia ya Schiller-Spenser (Courtney:1974) imekita mizizi yake katika imani kwamba umuhimu wa kucheza ni kumpatia mchezaji fursa ya kutumia nguvu zake za zaida.

Imani hii ina mushikili kwani inamwona mtoto kama kiumbe tu mwenye nguvu za ziada ambazo zinangoja kutumiwa. Ukweli ni kwamba, mtoto si mtu mzima mdogo na atacheza tu, awe ana nguvu au asiwe nazo. Tunasema hivyo kwa sababu tumegundua kwamba mtoto amejaliwa vipaji vya kisanaa ambavyo atavitumia kutekea hisia zake fiche na waaidha kumithilia hali anazokumbana nazo katika mazingira yake kupitia kwa michezo ya utotoni.

Slade (1973:1) anaiona michezo ya utotoni kama kifaa mufti cha kujengea hulka. Michezo hii anadai, humpa mtoto fursa ya kufikiri, kuthibitisha, kuburudika, kufanya kazi, kukumbuka, kuonyesha ujasiri wake, kufanya majaribio, kubuni na isitoshe, kujishughulisha na mambo mengi maishani mwake.

Mara kwa mara, watoto wanapocheza hisia zao batini na zile sahili hupata mwanya na hapo kumwezesha kufanyia majaribio hali anuwai akumbanazo maishani pamoja na zile za kuogofya. Kwa mfano, mandhari ya hospitalini huogofya kila mtoto lakini michezo kama vile *Doctor Doctor* ama *Doctor Patient* husaidia kupunguza uoga huo baada ya mtoto 'kudungwa' sindano ya bandia. Hali ambayo ingemtia mtoto jitimai ataweza sasa kuithubutu. Courtney (1974:32) anasema;

> Njia mwafaka zaidi ya kujifanya mtu mwingine-yaani kupata hisia zake batini-ni kuigiza nafsi yake pamoja na shughuli zake.
>
> (Tafsiri yetu)

Kulingana na maoni haya, watoto watawaelewa watu wengine wanaopatikana katika ulimwengu wao vizuri zaidi baada ya kuigiza nafsi zao. Watoto wanapojifanya kuwa baba, mama, mwalimu, daktari na askari na kujaribu kuishi jinsi wanavyoishi, kufanya wanavyofanya kazi zao, kufikiria wanavyofikiri, kuamua wanavyoamua na isitoshe, kuhisi hisia zao, japo kwa muda mfupi, watawaelewa wahusika hao zaidi ya ambavyo wangewaelewa kama wangeishia tu kuingiliana nao katika hali za kawaida za maisha yao.

Watoto wanapenda kuiga watu wazima. Sababu ni kwamba, watu wazima ndio wanaothibiti maisha yao. Kucheza au kufanya kazi kwa watoto, kucheka au kulia, kulala au kuamka, yote ni hiari ya mtu mzima na ndio sababu tunakubaliana na mawazo ya Alington (1961) kuwa azma kuu ya mtoto yeyote yule ni kuwa mtu mzima ili aweze kutwaa madaraka ya ki-utu uzima. Kwa kuiga watu wazima kwa hivyo, watoto hupata mamlaka ya kuamua au kuadhibu wenzao bila mzomo wa watu wazima. Isitoshe, kuiga watu wazima kutawawezesha kumiliki vifaa vya mamlaka kama vile pesa, magari makubwa na hata vijakazi. Hali hii humpatia mtoto yakini ya mamlaka aliyonayo kama kiumbe na papo hapo nafsi yake hukita mkuki.

Michezo ya utotoni kadhalika ni njia ya mtoto kuweza kuishi maisha ya kinjozi. Ni katika michezo hii ambapo mtoto ataweza kuifunganisha nafsi yake na ile ya shujaa wake maishani ambaye pengine huwa anamwona tu katika runinga au sinema. Kwa vile mashujaa hawa huishi maisha yapitao uwezo wa kibinadamu, mtoto anapowaiga, papo hapo ataweza kuishi katika ulimwengu wa ajabu au wa kinjozi hali wanayoipenda sana. Kwa vile mashujaa wa watoto huishi katika jamii timilifu ya kufikirika, anapowaiga, mtoto atahisi ufanisi mkubwa, kuongezeka kwa

mamlaka yake na isitoshe, matamanio yake ya kibinafsi yatatimizika ajabu.

Adhabu katika michezo ya utotoni ni ya bandia. Kwa mfano, katika mchezo unaoitwa *Naughty Pupil, At School* au *Teacher Teacher,* mtoto mtukutu atandikwaye viboko na mwalimu huwa hahisi uchungu kwa sababu huwa tayari amefunga nguo nyingi kiunoni. Michezo ya utotoni kwa hivyo, humwezesha mtoto kuvunja sheria au kujiingiza katika tabia zisizokubalika katika jamii. Baada ya kudadisi tabia hizo, huenda asiwe na hamu ya kuziendeleza katika maisha yake ya usoni.

Watoto wanapoiga watu wa amali mbalimbali kama vile udaktari, uwalimu, uaskari na udereva na kadhalika wazazi, wajomba au shangazi, papo hapo, watakuwa wakifanyia maisha yao ya baadaye mazoezi. Mazoezi hayo bila shaka huwawezesha watoto hao kuwa wenye haiba katika maisha yao ya utu-uzima na kadhalika kuwawezesha kutimiza hadhi mbalimbali za kijamii katika jamii pevu.

Jamii nyingi za Afrika zinasifika kutokana na ushirikiano pamoja na mwingiliano wazo. Hali hii ni muhimu kwa vile ndiyo isababishayo utangamano wa kijamii. Kwa vile michezo ya utotoni ina sifa ya michezo ya ujumuii, bila shaka, michezo hii inayo umuhimu wa kuipitisha amali muhimu ya kijumuii kutoka kizazi kimoja na kukipokeza kizazi cha pili. Kupitia michezo hii ya utotoni, watoto hupata fursa ya kujifunza umuhimu wa kushirikiana, kuheshimiana na kufanya mambo kwa zamu bila mwongozo wa sheria au amri mithaki ambazo zimekita katika jamii-pevu. Mazoezi haya ya kijumuia, licha ya kuendeleza tabia nzuri na kuimarisha busara ya kila kijana limbukeni kujiwekea nidhamu, huwaelimisha thamani ya ujima.

Michezo ya utotoni huchochea ubunifu, usimulizi au usemaji wenye ufundi, umahiri wa matumizi ya lugha na kadhalika mbinu mufti za mawasiliano hasa yale yenye kushirikisha mwili wote. Mbinu hizi ni kifaa madhubuti katika maisha ya mtoto ya baadaye.

Mpaka hapa, ni wazi kwamba ulimwengu wa mtoto bado ni mfinyu. Mtoto hatarajiwi kushughulikia masuala mengi na tena changamano. Mtoto bado hajapata tajriba ya kuingiliana na viumbe tofauti tofauti wa ulimwengu wetu mpana. Kadhalika, mandhari yake huwa bado ni sahili. Kwa kifupi, wakati huu ndipo mtoto anabobea maisha: yaani, ulimwengu mpana wa watu wazima ndipo unampombazukia mtoto huyu.

**TANBIHI.**

1. Hawa ni wasomaji habari katika runinga. Wanahabari hawa wanapendwa na watazamaji wengi kwa ukakamavu wauonyeshao wanaposoma habari. Wanatambulika na hadhira ya watoto kwa vile wao husoma habari za saa moja usiku ambazo aghalabu hutazamwa na watoto wengi.

# SURA YA TATU

## MAUDHUI KATIKA DRAMA YA WATOTO

### 3.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunajishughulisha na uchambuzi wa masuala muhimu katika tamthilia zilizowasilishwa na watoto wa shule za msingi katika tamasha za drama za mwaka 2002. Tamasha hizi ziliandaliwa chini ya himaya ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi.

Imethibitika katika sura ya pili kwamba, mtoto amejaaliwa kipawa cha usanii-tendi ambacho wasanii wamtungiaye tamthilia hawana budi kukiteka. Ili waweze kukiteka barabara, ni faradhi wasanii hao watafakari juu ya maudhui yanayoendelezwa na mtoto huyo katika maigizo yake ya utotoni.

Maudhui tumeyachukulia kuwa ni yale yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Maudhui haya huibuka katika uendelezaji pamoja na ukuzaji wa dhamira ya kazi hiyo ya kifasihi. Dhamira nayo ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji wake anapoisoma kazi hiyo.

Tukiyadadisi zaidi maelezo haya tunagundua mambo mawili ya maana. Kwanza, tunagundua kwamba maudhui na dhamira ni dhana mbili zinazoingiliana na kuchangizana kwa kiasi kikubwa. Uchanganuzi wowote wa maudhui bila shaka lazima ushungulikie dhamira. Kwa mtazamo mwingine kwa hivyo, maudhui ni maana ya ndani ya kazi ya fasihi nayo dhamira ni sehemu ya maudhui ambayo inatuelekeza katika

maana inayobainika tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Fasiri hii ndiyo kurunzi itakayotumulikia maudhui katika drama ya watoto.

Pili, maelezo hayo yametufaa kwa sababu hayajalenga mtunzi wa tamthilia pekee, yamemlenga msomaji pia. Vivyo hivyo, uchambuzi wetu wa maudhui katika drama ya watoto umewalenga watunzi na watoto wanaozisoma na kuziigiza tamthilia hizo.

Azma ya sura hii kwa hivyo, ni kukadiria kama kweli maudhui yanayoshughulikiwa katika drama ya watoto yana mshabaha na yale masuala ambayo watoto hujishughulisha nayo katika maigizo yao ya utotoni kama tulivyoyaona katika sura ya pili.

Tumegundua vile vile kwamba tamthilia za watoto zinaweza kuwa na maana changamano. Kwa vile msomaji huenda asiwe na bahati ya kukutana na mtunzi na kumuuliza alichokusudia kukisema katika tamthilia yake, hatuna budi kuchanganua maana hizo zote kwa kina na makini ili tuweze kukadiria kama fasiri ya maudhui hayo na mtunzi imelingana na urazini wa watoto.

Uelewaji wetu wa mambo haya yote tuliyokwishaeleza unaongozwa na nadharia yetu ya semiotiki. Kama tulivyotakadamu kufafanua, Barthes alitambua misimbo mitano mikuu ya usomaji wa kazi ya fasihi (Elam. 1980). Msimbo wa kihemetiki unaihusu taharuki na Barthes alidhihirisha kuwa msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anwani ya kazi ya fasihi. Kwa vile dhamira ya tamthilia aghalabu hujitokeza katika anwani yake, msimbo huu umetufaa sana katika utambuzi wa dhamira za watunzi wa tamthilia za watoto ambazo tumezihakiki.

Msimbo wa kirejelezi nao kwa mujibu wa Barthes, hujengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelwa katika kazi inayohusika. Msimbo huu umesaidia kutathmini kama kweli msanii ambaye

amewatungia watoto tamthilia amefinyanga maudhui yake kuyaafiki masuala tuliyoyapambanua katika michezo ya utotoni.

Kwa vile tamasha za drama za shule na vyuo ambazo huandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi ndilo, mpaka leo, jukwaa la kipekee wapewalo watoto kuwasilishia tamthilia, sura hii tutaifungua kwa uchambuzi wa muundo na madhumuni ya aina hii ya thieta ya watoto ili kitathmini kama tamasha hizi zimefaulu kukumbatia dhima ya drama maishani mwa watoto.

Japo ni vigumu kutenga fani na maudhui katika tahakiki nyingi, sisi tumevishughulikia vipengee hivi mbalimbali. Suala la fani tutalishughulikia katika sura inayofuata.

## 3.2 TAMASHA ZA DRAMA ZA SHULE NA VYUO.

Tamasha za drama za shule na vyuo zilianzishwa mnamo 1959 na Halmashauri ya Uingereza (British Council) ikishirikiana na Chama cha Thieta ya Kiafrika (African Theatre Guild) pamoja na Wizara ya Elimu. Shule za msingi zilishirikishwa mara ya kwanza mnamo 1980 na Bw. Wasambo-Were aliyekuwa Mwafrika wa kwanza kushikilia wadhifa wa katibu wa kamati andalizi ya tamasha hizo. Leo, zaidi ya watoto mia saba[1] hushiriki katika mashindano ya kitaifa ya tamasha hizi kila mwaka.

Katika tamasha hizi kuna mashindano. Uigizaji wa tamthilia, mashairi, densi za kitamaduni pamoja na uganaji huwasilishwa kuanzia mashinani hadi kiwango cha kitaifa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi. Mwanzo mwanzo, maigizo yaliwasilishwa katika Kiingereza pekee lakini sasa, Kiswahili na lugha za kienyeji zimetia fora.

Tamthilia ambazo huigizwa aidha ni zile zilizochapishwa, zilizotoholewa (kutoka nakala zilizochapishwa au ambazo hazijachapishwa) au tungo asilia ambazo hazijachapishwa. Tasnifu yetu imeshughulikia tungo asilia zilizotungiwa watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na mitatu na ambazo hazijachapishwa.

Kwa vile haya ni mojawapo ya mashindano muhimu katika Wizara, jopo la waamuzi hukabidhiwa jukumu la kukata uamuzi kwa kutumia mwongozo uliosanifishwa na Wizara. Mwongozo huu una vitengo vitano. Kila kitengo kimetengewa alama kama ifuatavyo:

| | | | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| i. | Uteuzi wa Mchezo | - | 20 |
| ii. | Maigizo | - | 30 |
| iii. | Mawasilisho | - | 25 |
| iv. | Mapambo/Maleba | - | 15 |
| v. | Ubunifu/Uasilia | - | 10 |
| | **Jumla** | - | **100** |

(Kenya National Drama Festival, 2000:18)

Tamasha hizi za shule na vyuo huongozwa na madhumuni yafuatayo:

a. Kuwapa vijana fursa ya kukuza hulka njema.

b. Kufunza na kukazia ustahimilivu pamoja na unyoofu kati ya vijana.

c. Kukuza vipawa vya umbuji vitakavyowawezesha washiriki kutumia lugha shawishi wanapoeleza mawazo na hisia zao ili kuyafanikisha mawasiliano yao ya kila wakati.

d. Kuifunza pamoja na kuiwezesha jamii kuyatambua maswala-ibuka ambayo yanaiathiri.

e. Kuwafichulia vijana tamaduni zetu mbalimbali na ambazo zina ukwasi mkubwa.

f. Kutoa fursa ya kujiburudisha na kadhalika kuutumia muda wa mapumziko kwa njia yenye ufanisi.

(*Tafsiri yetu*)

Kutokana na orodha hii, inathibitika kwamba takriban madhumuni yote ya tamasha za shule na vyuo yamemlenga mshiriki. Kwa sababu mshiriki huyu ni kijana, inahalisi kuamua kuwa kijana huyu yuko katika kipindi nyeti cha mabadiliko. Hiki ni kipindi ambapo imani yake ya kimsingi ndipo inaendelea kujengeka. Tamasha hizi kwa hivyo, zina nafasi kubwa ya kumwelimisha, kumzindua na kuifinyanga mitazamo yake ili ainukie kuwa mwananchi wa kuheshimika. Uchanganuzi wetu wa maudhui ya tamthilia anazoziigiza mshiriki huyu hatuna budi utatusaidia kuamua kama kweli madhumuni tuliyotaja hapo juu hutimilika.

Kamati andalizi ya tamasha hizi iliandaa mashindano ya mikoa kati ya tarehe 4 na 16 Machi, 2002. Tasnifu hii inachambua tamthilia nne (Taz. 1.5) kama kielelezo kiwakilishi cha tamthilia zilizowasilishwa na watoto kote nchini.

### 3.2.1 MAUDHUI YA *TUZO AZIZI* (Kiambatisho 2a)

Mchezo huu unazungumzia ufanisi anaoupata mwalimu mwenye bidii na nidhamu kazini. Wanafunzi wake wanapasi Kiingereza (somo analofundisha) katika mitihani ya kitaifa kuliko masomo mengine. Katika mashindano ya drama ( anayofundisha), wanafunzi kadhalika

hufaulu kuliko michezo mingineyo. Bidii na nidhamu yake inaonekana pale mwalimu huyu anapofika shuleni mbele ya wenzake na wenzake wanapoondoka baada ya kazi kwenda kujumuika katika anasa mbalimbali, yeye hutumia wakati huo kufunzia michezo ya kuigiza. Bila shaka, mwalimu huyu ni kielelezo bora kwa walimu wenzake na kadhalika wanafunzi na anastahili *tuzo azizi.*

Maudhui haya yametokama na mazingira ya watoto. Kama tulivyoona hapo awali katika michezo ya utotoni (Taz.2.3.2), *Tuzo Azizi* utampatia mtoto fursa ya kujishughulisha na mambo mengi maishani mwake kwa jinsi anavyoyashuhudia kila siku. Kwa mfano, ataweza kuadhibu wanafunzi watundu na wakati uo huo kufundisha jinsi mwalimu hodari anavyofundisha.

Mchezo unapoendelea, maudhui ya wivu yanaanza kushughulikiwa. Mwalimu Mkuu anamfitini mwenzake kwa Mkurugenzi wa shule ili afutwe kazi. Migogoro hii kati ya walimu, japo imo shuleni, ilikuwa vigumu kwa watoto kuimudu na kuiwasilisha kisawasawa. Iliwawia vigumu kuendeleza wivu wa Mwalimu Mkuu kwani ilikuwa nadra watoto kushuhudia migogoro kama hii na hapo kuwawia vigumu kuiga hali ambazo hazitongolewi wazi. Kadhalika, waliogopa kuwavunjia walimu wao heshima kwa kuwaiga kama wenye wivu. Suala hili, bila shaka, haliko katika mawanda ya watoto.

Mchezo huu uliyasawiri masuala ya kinyumbani jinsi yanavyoendelezwa katika michezo ya utotoni. Lakini, tafsiri ya maisha ya mume na mke nyumbani haikulingana na urazini wa watoto. Wanawake walitumiwa kama chombo cha kuendeleza maovu katika jamii. Mkurugenzi ambaye alikuwa mhusika wa kike, alikubali fitina za Mwalimu Mkuu bila ya kuzifanyia upurukushani wowote. Naye mkewe mwalimu alikubali hongo ya shilingi elfu mbili kutoka kwa mwalimu yuyo huyo ili aweze kumsaliti mumewe.

Mtazamo huu hasi wa mwanamke unamsawiri kama kiumbe dhaifu na mwovu. Mtazamo huu huenda umetawaliwa na itikadi ya kiubabedume. Hizi ni fikira ambazo zinamchukulia mwanamke kama kiumbe duni asiyekuwa na uwezo wowote katika jamii. Katika jamii ya aina hii, mwanamke huwa chombo cha mwanamume tu, na hutumiwa na mwanamume jinsi anavyotamani.

Ulimwengu wa watoto, kama tulivyouona katika michezo ya utotoni, hauna wanawake wa aina hii. Kwa mboni za mtoto, mwanamke ni 'mama' naye mwanamume ni 'baba'. Mama kwa hivyo, hutunza familia nyumbani au hufanya kazi aidha ya ualimu au uuguzi. Baba naye huiongoza familia yake. Mtazamo huu hasi wa mwanamke kwa hivyo, haukuwavutia watoto kwa vile hili ni suala geni katika ulimwengu wao.

Njama zote dhidi ya mwalimu mwenye bidii na nidhamu zilipoambulia patupu na mwalimu huyo kupandishwa madaraka na kuwa mwalimu mkuu, watoto walichangamuka sana. Hili ni dhihirisho kwamba katika ulimwengu wa watoto, maudhui yanayoendeleza wema na uadilifu hutiliwa mkazo. Hapo, mtunzi alifanikiwa kulitazama suala la haki ya mja kutoweza kuzama kupitia kwa mboni za watoto.

### 3.2.2 MAUDHUI YA *MAJUTO* (Kiambatisho 2b)

*Majuto* ni tamthilia inayoizunguka jamii ambayo imevamiwa na nduli ukimwi. Aghalabu mtu anapoambukizwa ugonjwa huu yeye hubaguliwa. Kwanza, uwele huu bado hauna tiba kwa hivyo kushirikiana na mtu anayeugua kuna hatari ya kuambukizwa. Pili, ndwele hii huhusishwa na uasherati. Aliye nao huchukuliwa kama asiye mnyoofu wala mwadilifu. Kwa sababu hii, Baba Majuto anaonekana mwenye babaiko na kuchanganyikiwa ukweli ulipomfunukia kwamba Majuto, mwanawe wa pekee, alikuwa mgonjwa wa ukimwi.

Baba Majuto ni Waziri wa Afya. Cheo hiki kinamzonga zaidi kwa sababu alihitajika kuonyesha mfano bora zaidi. Anaamua kumbagua bintiye kwa kumfukuza nyumbani licha ya kwamba huo ndio wakati ambapo mwana alihitaji mapenzi ya mzazi kuliko wakati mwingine ule. Baba Majuto aidha alikuwa hapo mbeleni amekwishambagua nduguye wa toka nitoke (Baba Dola) kwa sababu yeye alikuwa maskini.

Suala hili la ubaguzi limejengeka katika mazingira ya kinyumbani wanayoyaelewa watoto. Hata hivyo, ukimwi una athari ya moja kwa moja kwa watu wazima kuliko ilivyo kwa watoto. Kwa muda mrefu, watoto wamekuwa wakiteseka tu baada ya kuambukizwa na wazazi wao au baada ya kuachwa mayatima. Siku hizi, mambo yamebadilika. Ukweli huu unadhirika Majuto anaponajisiwa na *mashifta*[2] akiwa njiani kwenda shuleni. Watoto wenzake walimwonea huruma sana ishara kwamba fasiri ya hatari ya ukimwi katika ulimwengu wao imekaribiana na ile ya ulimwengu wa watu wazima.

Suala la umaskini kadhalika lilifasirika kulingana na urazini wa watoto. Katika mazingira ya watoto, kama ilivyo katika tamthilia ya *Majuto*, kuna matajiri ambao wamewaajiri vijakazi. Matajiri hawa yumkini hukosa utu na ubinadamu na huanza kuabudu bidhaa na vyeo. Sifa hii inawafanya wawaone binadamu wengine walio maskini kama si watu tena bali wanachukuliwa sawa na vitu. Huu ndio uhusiano uliosawiriwa kati ya Baba Majuto na Baba Dola. Utengano kati ya Dola na Majuto ulisababishwa na tofauti kati ya wazazi wao. Watoto walilitambua suala hili kuliko masuala mengi makubwa ambayo watu wazima waliyaona kuwa muhimu. Hali ya Majuto na Dola kutoweza kucheza pamoja tena ndiyo iliyowahuzunisha watoto wengi katika hadhira. Mtunzi hakuendeleza suala hili kwa sababu aliliona kuwa dogo mno. Angeliendeleza, mchezo huu ungevutia watoto zaidi ya ilivyoshuhudiwa.

### 3.2.3 MAUDHUI YA *MONALISA* (Kiambatisho 2c)

Tamthilia ya *Monalisa* inamulika nuru masuala yanayofungamana na haki za watoto wa kike. Mtunzi anatuangazia kwa jicho la upekuzi ubaguzi unaofanyiwa mwana huyu (Monalisa) nyumbani mwao na hata shuleni. Nyumbani, babake Monalisa anaamini kuwa mtoto wa kike hastahili kurithishwa mali. Kadhalika, anaona kuwa kumwelimisha ni kama "kunyunyizia shamba la jirani maji!"[3] Shuleni, anakabiliwa na ubaguzi zaidi. Japo alishika mimba, kitendo hiki kiliwahusu watu wawili: yeye na mwanafunzi-mwenza, Timothy. Monalisa ndiye aliyefukuzwa shuleni na Mwalimu Mkuu (ambaye ni mhusika mwanaume), akidai kuwa "kuku akiruhisiwa kukaa na vifaranga, vifaranga hao watajifunza kutaga mayai!"[4] Adhabu aliyopewa Timothy ilikuwa kutandikwa viboko sita na kupiga deki vyoo kwa wiki moja.

Kama ilivyobainika hapo awali, itikadi ya ki-ubabedume inatumiwa kumbagua na kumdhalilisha mwana wa kike. Mwana huyu anakandamizwa na mifumo inayompa mwana wa kiume nafasi ya kukosa bila kukosolewa. Katika ulimwengu wa watoto, mtoto ni mtoto, awe wa kike au wa kiume. Amali za kitamaduni kwamba aila haikamiliki bila mwana wa kiume hazina mashiko katika ulimwengu wa watoto. Kinachowatofautisha katika michezo yao ya utotoni ni wajibu wanaotengewa kuucheza. Kwa mfano, mtoto mvulana atachukua wajibu wa 'baba' naye mtoto msichana atachukua wajibu wa 'mama'. Fasiri ambayo itikadi hii ya ki-ubabedume ilipewa katika tamthilia hii waama imepita urazini wa watoto.

Suala la Monalisa kushika mimba waaidha haliafikiani na ulimwengu wa watoto. Katika ulimwengu wao, watoto huishi katika hali ya kinyumba bila ya kuishi maisha ya kinyumba. Mapenzi ya kimwili huchukulika kama 'tabia mbaya'. Ingawa siku hizi wasichana wenye umri tunaoushughulikia hushika mimba, suala hili liliwaaibisha watoto

kiasi. Kwao hii ilikuwa 'tabia mbaya' ambayo haikufaa kutongolewa wazi. Tunawaunga mkono hapa; watoto ni bora wafundishwe jinsi ya kujihini na shauku za ngono badala ya kuonyeshwa madhara ya ngono.

Tunashuhudia mamake Monalisa akiuawa na babake na papo hapo mimba ya Monalisa ikiharibika. Mtunzi analifanya onyesho hili kuwa lenye majonzi makuu. Waigizaji wanalia na pia kuwaliza watazamaji kwa muda. Katika ulimwengu wa watoto, mambo hujifumbua kwa kasi na hamna wakati wa majonzi marefu. Hali hii ilimnyima mtoto fursa ya kufurahia na kadhalika kujiburudisha huku akijielimisha. Kwa kiasi kikubwa, sehemu hiyo ilionekana kama iliyoshindiliwa mihemko ya kiutu uzima.

Watoto walishangilia Luseka alipompiga risasi mkewe na kadhalika korti ya umma alipomhukumu kifo Luseka kwa kuua. Hawakusadiki kwamba yote yaliyotendeka yalikuwa ya kweli. Huu waliuona kama ulimwengu bunifu jinsi wauonavyo katika runinga. Huu ndio ulimwengu uwapatiao mamlaka ya kuwaadhibu watenda maovu bila kusababisha majonzi yoyote. Huu ndio ulimwengu wa watoto ambao mtunzi angeuendeleza.

Mwishoni mwa mchezo, Monalisa anatuzwa digrii na kuchaguliwa na umma kuwa kiongozi wa jamii. Huu ni ulimwengu wa madaraka na siasa na katika mboni za watoto, ulimwengu kama huo ni wa watu wazima. Dhamira ya mtunzi kuumaliza mchezo jinsi hii (alikiri katika mahojiano yetu), ilikuwa ni kuuhamasisha umma mkubwa wa wanawake unaokandamizwa kuibadilisha hali yao ya maisha. Lakini je, mwana wa kike aliye chini ya miaka kumi na mitatu ataweza kujitwika mzigo huu wa kuizindua jumuia ya wanawake? Suala hili ni la ukombozi wa wanawake. Licha ya kuwa lina athari kubwa kwa mtoto wa kike, fasiri aliyolipa mtunzi imepita mawanda ya watoto. Migogoro kama hii yastahili ulimwengu wa watu wazima kwani mara nyingi itawawia vigumu watoto kuiongoza jumuia ya wanawake katika masuala nyeti na ya kiutu uzima kama haya.

### 3.2.4 MAUDHUI YA *VISOSAUTI* (Kiambatisho 2d)

Mchezo wa *Visosauti* unahusu watoto kufanyishwa kazi za shokoa. Mtunzi wa mchezo huu anapigania maslahi ya watoto hasa wale wa kike kama kielelezo huku akiwazingatia kama viumbe wenye mahitaji maalumu wakilinganishwa na wale wa kiume. Matatizo ya watoto hawa wa kike kwa hivyo, ni darubini anayotumia kuangalilia matatizo yanayoukabili ulimwengu wa watoto kwa jumla. Anawatumia kama mfano wa kuizindulia jamii ili iweze kuwakinga watoto wote dhidi ya aina hii ya dhuluma na kadhalika, kuwakomboa watoto wale walionaswa tayari na mikatale ya kazi za shokoa inayohatarisha maisha pamoja na maslahi yao.

Charity ana kipawa cha kuendeleza masomo yake hadi upeo wa kuwa daktari lakini Susanna (mamake wa kambo) anakuwa kizuizi kikuu. Akiongozwa na inda iliyochanganyika nao ujuhula pamoja na tamaa, Susanna anakitoa kisichana hiki shuleni na 'kukiuza' (jinsi walivyouzwa watumwa) kwa kiwanda cha kuchimba migodi.

Tunaona kuwa mtoto hatima hana nafasi maalumu katika jamii. Ni jukumu la walezi, ukoo, jamii na serikali kuwakimu na kuwaelimisha mayatima. Jukumu hili halikutimizwa na Priscilla hali ambayo iliwafedhehesha watoto waliokuwa ukumbini. Ujahili alioupitia mtoto mwenzao ulimulika nuru hali kama hizo zilizotamalaki majumbani ambamo baadhi ya watoto hukulia. Bila shaka, baada ya mchezo huo, watoto walikuwa na mtazamo tofauti wa maisha. Mchezo huo ulikuwa umefukuta cheche za upinzani dhidi ya udhalimu ambao watoto mayatima hufanyiwa.

Suala la uke-wenza limejitokeza katika tamthilia hii. Tunawaona wazazi wakihatarisha maisha ya watoto kwa kuwalelea katika mazingira yasiyo salama na thabiti. Ndoa ya wake wengi tunaishuhudia ikifinyanga

mazingira yaliyosheheni inda na dhuluma. Mfano mwafaka ni pale Susanna anapomwangamiza mke mwenzake pamoja na mume wao hali inayowaacha watoto taabani. Huo ni uzinduzi kwa watoto kujihadhari na mama wa kambo kama huyu.

Ingawa masuala haya ambayo tumeyachambua yanapatikana katika ulimwengu wa watu wazima, wanaodhurika zaidi ni watoto. Ulimwengu wa leo unahitaji watoto wahusishwe katika utatuzi wa matatizo yanayowakumba ili kuufanya ulimwengu wao kuwa mahali bora pa kukulia na kuishi. Kwa mujibu wa mtunzi, matatuzi hayawezi kuanguka kutoka mbinguni mithili ya mana na kupachikwa juu yao na ndio sababu watoto wa *Visosauti* wanajikomboa wenyewe kwa wenyewe kutoka mikatale ya uchimbaji migodi.

Hata hivyo, hali ya majonzi mazito mazito ilipigwa mwangwi katika tamthilia hii kiasi cha kumnyima mtoto fursa ya kuburudika huku akielimika. Maisha ya watoto yamejaa michezo (Courtney: 1974) na kwa vile michezo ya watoto inafaa ichukulike kama kifaa cha kujengea hulka (Slade 1973:1), ni bora watoto baada ya kuuigiza au kuitazama michezo hii waweze kusimama tisti na kupinga hali zozote kandamizo iwe ni majumbani mwao au kwokwote kule. Majonzi, kwa maoni yetu, yangefungamanishwa na kucheza kwao hawa watoto zaidi ya ilivyofanyika tamthilia ya *Vososauti* ilipoigizwa jukwaani.

Kitendo cha utu na ubinadamu kinachotokea mwishoni mwa tamthilia kimeoana na sifa kuu ya watoto ya kusahau madhila waliyofanyiwa baada ya muda mfupi. Aghalabu hawaweki kinyongo wala kulipiza kisasi. Charity anakubali kumpa 'figo ya uhai' Susanna licha ya kwamba hapo mbeleni alikuwa amewaua wazazi wake na kumtendea yeye na dadake ujuhula usio kipimo. Ulimwengu wa watoto umesheheni sifa hii ya kuyasahau yaliyopita na kusamehe wote waliowakosea. Watoto ukumbini kufarijika Charity alipokubali kumpa uhai katili Susanna ni ishara kwamba suala hili lilifasirika katika mawanda yao.

## 3.3 KIMALIZIO.

Katika sehemu hii tumechambua maudhui muhimu yaliyoshughulikiwa katika michezo iliyoigizwa na watoto. Imethibitika kwamba maudhui hayo yana mshabaha mkubwa na masuala yanayopatikana katika ulimwengu wa watoto. Hata hivyo, fasiri ya baadhi ya maudhui hayo haikulingana na urazini wa watoto; fasiri hiyo ilikuwa katika mawanda ya watu wazima. Tathmini ya ufanisi wa fani katika kuyawasilisha maudhui hayo haijashughulikiwa hapa. Suala hii limeelezwa katika sura inayofuata.

**TANBIHI.**

1. Idadi hii ni kwa mujibu ya ripoti ya kila mwaka ambayo hutolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi. (Taz. *Annual Inspectorate Report on Co-curricula Activities 2002*, Ministry of Education Science & Technology. uk.8).

2. *Mashifta* ni majambazi wenye asili ya Somalia ambao huhangaisha wasafiri katika mkoa wa Kaskazini Mashariki.

3. Taz. Katika Masinde, W.K. E. *Monalisa* (Kiambatisho 3c) Tamthilia hii haijachapishwa. Uk. 1

4. Kama hapo juu uk.lv

# SURA YA NNE

## WAHUSIKA NA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA DRAMA YA WATOTO

### 4.1 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu, tumechambua maudhui ambayo yalishughulikiwa katika tamthilia zilizowasilishwa na watoto katika tamasha za drama za shule na vyuo mnamo 2002. Sura hii ya nne inapiga hatua zaidi. Tunachanganua usawiri wa wahusika wakuu wanaopatikana katika tamthilia hizo pamoja na matumizi yao ya lugha.

Wahusika, kwa minajili ya utafiti wetu, ni wale watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Viumbe hawa ni kama nguzo kuu ya dhamira na maudhui katika tamthilia kwa sababu tamthilia, tofauti na tanzu zingine za fasihi, ni utagaa wa fasihi ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji kuuwasilishia ujumbe wake. Kwa mtazamo mwingine, huu ni utagaa ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika. Mazungumzo hayo si majibizano ya semi au kauli tu bali ni msingi mkuu wa kuendelezwa na kukuzwa kwa dhamira na maudhui mbalimbali katika tamthilia.

Wahusika hufanana kwa kiasi kikubwa na binadamu katika maisha yao ya kawaida hata ingawa sio lazima wadhibitiwe na kanuni zote za binadamu halisi. Na kwa vile tumekwisha sadiki hapo awali kwamba ulimwengu wa watoto ni tofauti na ule wa watu wazima, mtunzi wa tamthilia ya watoto atafanikiwa kutunga mtungo ulio katika mawanda ya watoto ikiwa wahusika wake, kwa kiasi kikubwa, watakuwa na sifa zinazofungamana na majukumu ambayo watoto huyatekeleza katika ulimwengu wao. Wahusika kama hao wataweza kuliendeleza tendo kuu vizuri na kadhalika kuiaminisha hadhira-lengwa.

Mtunzi wa tamthilia ya watoto, kwa hivyo, atapata ufanisi zaidi ikiwa mhusika anayemuumba ataweza kutambulikana kutokana na lugha yake. Na ili lugha yake iweze kuuwasilisha ujumbe anaonuia vyema pamoja na kuwashawishi na kuwaathiri ipasavyo watoto-lengwa, ni lazima lugha hii iwe yenye mshabaha mkuu na ile lugha isemwayo katika ulimwengu wa watoto.

Mpaka hapa, imedhihirika kwamba uhusiano kati ya wahusika na matumizi yao ya lugha ni muhimu na ni wa kutegemeana, mmoja ni kama upande mmoja wa sarafu. Sura hii kwa hivyo, katika tahakiki yake ya tamthilia zilizowasilishwa katika tamasha za drama za 2002, azma yake itakuwa kuchunguza kama usawiri wa wahusika pamoja na matumizi yao ya lugha, vyote viko katika mawanda ya watoto-lengwa.

### 4.2.1 *TUZO AZIZI:* WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA (Kiambatisho 3a)

Mandhari ya tamthilia ya *Tuzo Azizi* ni shuleni na kwa uchache nyumbani. Mazingira haya kama tulivyoona hapo awali ni mhimili mkuu wa kuendelezea masuala ambayo watoto hukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku. Mama Mkurugenzi, Mwalimu Mkuu, Mwalimu na Wanafunzi ndio wahusika ambao mtunzi amewatumia kama kipaza sauti cha kuwasilishia mawazo yake.

Migogoro katika mchezo huu inamzunguka mwalimu wa Kiingereza na Drama. Bidii na nidhamu yake kazini vinamletea ufanisi mkubwa. Wanafunzi wanapita mtihani wa Kiingereza na timu yake ya michezo ya kuigiza inafaulu kuliko nyinginezo katika shule hiyo. Mwalimu huyu ndiye nguli kielelezo katika jamii na ambayc angefaa kuigwa na walimu wenzake na kadhalika wanafunzi katika mustakabali wao.

Hata hivyo, ufanisi wa mwalimu huyu unazaa wivu kutoka kwa Mwalimu Mkuu. Hapa tunakumbana na mhusika-kinzani. Mwalimu Mkuu kwa hivyo anasawiriwa kama mtu mwenye wivu na inda. Anamtia sumu mama Mkurugenzi ili ampige kalamu mwalimu huyu mwenye bidii kwa sababu tayari alikuwa tisho kwa madaraka yao. Mkewe mwalimu anajiunga na kikosi hiki kwa sababu ya tamaa yake ya pesa na ubinafsi.

Wahusika hawa wanasawiriwa na mtunzi kama vielelezo vya mfumo na matabaka yanayokwamisha maendeleo shuleni. Wao ni vielelezo vya ubinafsi na jinsi unavyoweza kuwa kizuizi kikubwa katika kupata matokeo mazuri shuleni katika mitihani ya kitaifa pamoja na katika mashindano ya mtalaa mwenzi. Wahusika kama hawa wanawakilisha nguvu zozote hasi ambazo hukita kwenye ufanisi wa walimu na wanafunzi kwa jumla.

Hadhira ya watu wazima iliielewa migogoro hii kiasi cha kuweza kuchukua misimamo kinzani. Kuna wale waliomtukuza mwalimu na kuna wengine waliomuunga mkewe mkono kwa kudai kwamba bidii yake kazini ilimfanya asitimize matakwa ya mkewe nyumbani. Wachache walimhurumia mama Mkurugenzi na Mwalimu Mkuu. Hii ni ishara kuwa udhalimu, wowote ule, haukubaliki katika jamii.

Hata hivyo, iliiwia vigumu hadhira ya watoto kujitambulisha na wahusika hasi. Walivyosawiriwa sivyo ilivyo katika ulimwengu wa watoto. Davies na mwenzake Watkins (1960) wanapendekeza kuwa wahusika mwafaka kwa drama ya watoto ni wale ambao hupatikana katika ulimwengu wa watoto. Wahusika kama hawa aghalabu huwa ni watoto au wanyama. Wanaendelea kusema kuwa watoto huvutiwa na kupumbazwa zaidi na wanyama au wadudu ambao huwakilisha tabia na mienendo ya binadamu.

Kutokana na mawazo hayo ya Davies na Watkins inaonekama kwamba hadhira ya watoto hushawishika kujihusisha zaidi na wale wahusika

ambao ni watoto kama wao. Mnato huo hutokana na uwezo wa wahusika-watoto kujishirikisha katika hali anuwai na zilizo na muumano na maisha ya kila siku ya watoto. Kwa mfano, itawawia rahisi wahusika-watoto kuimba na kucheza katika michezo ya utotoni kama vile kibemasa na kuweza kuishirikisha hadhira ya watoto wengine kuliko wawezavyo kufanya watu wazima au mabarubaru.

Hata ingawa watoto ndio waliotungiwa tamthilia hii ya *Tuzo Azizi,* mtunzi aliwatengea nafasi moja pekee, ile ya kuigiza wanafunzi. Nafasi waliyocheza kama wanafunzi kwa hivyo, ilikuwa ile tu ya kufukuta migogoro kati ya wahusika wengine. Msimamo wa watoto haujitokezi waziwazi katika migaragazano kati ya walimu wao mpaka mwishoni mwa mchezo ambapo mtunzi anawatumia kumwadhibu Mwalimu Mkuu kwa madai kuwa alikuwa amesababisha kifo cha mwalimu wao mpendwa.

Kadhalika, iliwawia vigumu watoto wa shule ya msingi kuandamana jukwaani ifanywavyo mashuleni na kadhalika vyuoni kwa sababu watoto katika shule za msingi hawajazoea maandamano. Rabsha kama hizo mara nyingi huhusishwa na wanafunzi wa sekondari na vyuo. Mchezo huu ungewavutia watoto-lengwa zaidi kama migogoro mikuu ingejengwa na wahusika-watoto na kama migogoro hiyo ingewasilishwa kupitia mboni zao watoto hao.

Kuhusu matumizi ya lugha, tumegundua kwamba, kwa vile nguli katika *Tuzo Azizi* ni watu wazima, lugha wanayotumia kadhalika ni ya kiutu uzima. Stevens John (1992:4) akizungumzia suala la lugha na itikadi katika sanaa bunilizi ya watoto anasema:

> .... Lugha mwafaka kwa watoto ni ile ambayo ina uwezo wa kuamsha hisia za ulimwengu halisi. Azma kuu hapa yumkini ni kumzoesha mtoto kwa mazingira ya ulimwengu halisi.
>
> *(Tafsiri yetu).*

Kulingana na maoni haya, ulimwengu halisi wa watoto aghalabu u tofauti na ule ulimwengu wa watu wazima. Kwa hivyo, haihalisi lugha ya ki-utu uzima kutumiwa na watoto katika maigizo yao. Mawazo haya tunavyoona, hayana mshabaha na jinsi lugha ilivyotumiwa katika tamthilia ya *Tuzo Azizi*. Mtunzi, kupitia kwa drama, hakuchukua fursa ya kuwaandaa watoto kwa matumizi mapevu ya lugha. Alitumia kwa mfano methali na nahau ambazo watoto hawakuzielewa. Ingawaje mtunzi alifaulu kuitia pambo tamthilia kwa kufinyanga matumizi ya tamathali mpaka yakakaribiana na jinsi yanavyotumiwa katika hali yao ya kawaida, kwa limbukeni, huu haukuwa msingi thabiti wa kuonyeshea uhalisi wa matumizi ya lugha. Ilidhihirika kwamba tamathali nyingi hazikuwa katika urazini wa watoto.

Methali zilizotumika ziliufanya ujumbe uliowasilishwa kuwa na uzito wa kisanaa ambao watoto bado hawana tajriba ya kuuhimili. Matumizi ya methali yalikita katika mazungumzo ya watu wazima kuonyesha kuwa hivyo ndivyo walivyotumia lugha katika ulimwengu wao halisi na wala sivyo ilivyo ulimwengu wa watoto. Kwa mfano, mama Mkurugenzi alipowahutubia walimu alitumia methali (uk.xv) *mgaagaa na upwa hali wali mkavu* naye Mwalimu Mkuu aliwaambia walimu kuwa *ukweli ukidhihiri uongo hujitenga* (uk.xvi). Kwa mtazamo fagia, methali hizi huenda zikaonekana nyepesi lakini ukweli ni kwamba, matumizi yake yana uwezo wa kukanganya hasa umri ambao haujaupata uzoefu wa kutosha wa mafumbo na muktadha wake.

Kuipatia matini ya fasihi ya watoto muala, Stevens John (1992:38) anapendekeza 'matumizi ya msamiati mwepesi na unaorudiwarudiwa'. Hii ndiyo sababu hadhira ya watoto ilichangamshwa kiasi na urudiaji wa maneno kati ya wahusika fulani. Kwa mfano (uk.xxii):

| | | |
|---|---|---|
| Mke | : | Mbona mabadiliko haya niyaonayo?<br>Ulikunywa nini? Ulivuta nini? |
| Mwalimu | : | Uliza swali moja kisha jingine.<br>Sitaki mkururo wa maswali! |

| | | |
|---|---|---|
| Mke | : | Ulikunyani? |
| Mwalimu | : | Swali mufti. La pili? |
| Mke | : | Ulifyonza matingasi na mbagara? |
| Mwalimu | : | Umeliuliza vizuri, hata zaidi. |
| Mke | : | Yule mzazi aliyetaka kukuona labda amenyambua kichwa chako! |
| Mwalimu | : | Mzazi yupi? Lini? Wapi? |
| Mke | : | Swali mufti, la pili? |
| Mwalimu | : | Mzazi yupi? |
| Mke | : | Umeliuliza vizuri hata na zaidi. |
| Mwalimu | : | Aliyekueleza kwamba mzazi alitaka kuniona ni nani? |
| Mke | : | Swali zuri hata zaidi. |

Japo hadhira ya watoto iliyachukulia matumizi haya ya lugha kuwa kiburudisho tosha kwa vile maswali yenyewe yanaonekana yenye upuzi mwingi, fasiri hiyo kwetu ni sisisi. Ukweli ni kwamba ndani ya maswali haya ya kipuuzi mna falsafa nzito. Wanafunzi wale ambao wameweza kusoma tamthilia za kibwege kama vile *Amezidi* ya S.A. Mohamed ama *Waiting for Godot* ya Samuel Bickett ndio pengine wangeelewa falsafa iliyomo katika matumizi hayo ya lugha wala sio watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na mitatu.

Kabla ya kuikamilisha sehemu hii, inahalisi kutaja kwamba sio matumizi yote ya lugha katika tamthilia hii yaliyokuwa juu ya urazini wa watoto. Mtunzi mara kwa mara alifaulu kuogelea katika ziwa moja na wanafunzi wake ki-lugha. Kwa mfano, katika mazingira ya kileo, tabia ya kuchanganya au kuhamisha ndimi imewamba. Hali hii pia tuliishuhudia katika michezo ya utotoni (Taz.2.3). Watoto walichanganya Kiingereza na Kiswahili au walihama kutoka kwa lugha hizi hadi lugha ya *Sheng* ama *Engsh*[1]. Mtunzi wa *Tuzo Azizi* aliathirika na hali hii. Kwa mfano, tazama mkewe mwalimu anavyosema (uk.xxi):

> Mimi ni mkeo na hunitishi.
> You cant *bwogo*[2] me!

Matumizi haya ya lugha yanasawiri mazingira halisi ya watoto. Na kwa vile watoto huchoshwa kiurahisi na mafululizo wa kitu au hali moja kwa muda mrefu, mabadiliko ya mara kwa mara ya lugha mathalan kuchanganya na kuhamisha ndimi huwapumbaza kiasi.

### 4.2.2 *MAJUTO* : WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA (Kiambatisho 3b)

Migogoro mikuu katika tamthilia hii imejengeka kwenye wahusika watano. Wahusika hao ni Baba Majuto, Mama Majuto, Majuto, Shamu na Baba Dola. Kwa vile wote, isipokuwa Shamu, ni wa mbari moja, mwandishi amewatumia kujengea mandhari ya kinyumbani. Kama tulivyotakadamu kusema hapo awali, mandhari ya kinyumbani pamoja na wahusika wa mbari moja ni vipengee vinavyopatikana katika ulimwengu wa watoto.

Majuto ndiye mzushi wa mgogoro mkuu unaokuzwa na tamthilia hii. Mchezo unapoanza, tunamuona kijana huyu amedinda kurudi shuleni hata ingawa huo ulikuwa mwaka wake wa mwisho wa masomo yake ya msingi. Anataka kujitia kitanzi. Sababu ya kutaka kujiua tunagundua mwishoni mwa mchezo; Majuto anaugua Ukimwi na hangestahimili aibu ya kuugua ugonjwa huo hatari.

Mchezo unavyoendelea kukunjuka ndivyo wahusika wenye sifa mbalimbali wanavyoibuka. Maingiliano ya wahusika hao na Majuto ndiyo yanayozitambulisha sifa zao za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa. Baba Majuto ni Waziri wa Afya serikalini. Kwa sababu ya cheo chake, hawezi kuhimili tahayari ya bintiye kuugua Ukimwi. Mzee huyu anasawirika kama kielelezo cha ubinafsi na ubaguzi dhidi ya tabaka la wanyonge hasa anapomfukuza bintiye nyumbani kwa kuogopea cheo chake.

Wahusika waliosalia wanasawiriwa kama wenye utu na ubinadamu kwa vile wanamwonea huruma Majuto. Baba Dola, licha ya kufukuzwa na Baba Majuto (ambaye ni kakake) katika kasri lake, anampokea Majuto kwa moyo mkunjufu na kumuuguza. Mtunzi anadhihirisha kwamba cheo na mali aghalabu huzaa ubinafsi na ukatili.

Uteuzi wa wahusika walioigiza sehemu za watoto haukuafikiana na mazingira ya watoto. Yaani, Majuto, Shamu na Dola, wote walionekana wakubwa wa kimo. Tulipowahoji, tuligundua kwamba walikuwa wenye hirimu ya takriban miaka kumi na mitano. Mchezo kwa hivyo uliishia kuwavutia na kuwanata vijana waliokwishabaleghe na ambao wengi wao hupatikana katika shule za upili na vyuo. Sehemu za watoto zingeigizwa na watoto kwa umri na kimo, bila shaka, hadhira ya watoto ingejihusisha zaidi ya ilivyoonekana.

Kwa vile mgogoro mkuu wa tamthilia hii u kati ya mabarubaru na wazazi wao, ililazimu matumizi ya lugha pevu. Mtunzi kwa kuogopa kutumia lugha yenye matusi au fedheha, anakoleza tamthilia ya *Majuto* mafumbo na vitia ladha vya kila nui. Hebu tuyatazame mazungumzo kati ya wazazi wa Dola (uk. xli - xlii).

| | | |
|---|---|---|
| Baba Dola | : | Bibie, mafarakano haya yote yameletwa na nani? |
| Mama Dola | : | Muulize huyo bintiye eti. Umri huu aliwo nao tayari kesha jua *kuinika kinu cha kutwangia!* |
| Baba Dola | : | Swadakta mwanangu! |
| Mama Dola | : | Swadakta! Swadakta za nini? Yaani mambo aliyoyafanya yamekufurahisha? |
| Baba Dola | : | Sasa kwa nini nisifurahie. Mwanangu ameshajua... kuinika kinu. Baadaye atajua kutwanga au kupepeta nafaka. |
| Mama Dola | : | Baba Dola! Yaani wajifanya huelewi Kiswahili? Ngoja nikutoe taka masikioni. Dola bintiyo keshanza *kujifunza kukwea minazi na kugema.* |
| Baba Dola | : | .... Mambo haya yote Dola mwanangu |

| | | |
|---|---|---|
| | | kajifunza kwa usiku mmoja tu! Mashalla! |
| Mama Dola | : | ... Mtume na asimame!... haya, mtwae huyo mtailshamsi wako, umvike nishani ya dhahabu kwa hayo aliyoyafanya, *akishagemwa* barabara, ndipo utaelewa maana ya tabia chafu. |
| Baba Dola | : | *Tabia chafu!* |
| Mama Dola | : | Tabia chafu! |
| Baba Dola | : | .... Hebu subiri kidogo. Wajua mimi mpaka sasa sijaelewa sawa. Hebu nitoe gizani... Kwani Dola amefanya nini hasa kikubwa? |
| Mama Dola | : | ... nimemfumania kule kichorochoroni na yule kizuka wa Mzee Juma Kitwana *wakitafunana midomo!* |
| Baba Dola | : | Walitafunana midomo? Na huko ndio kufanya nini? |
| Mama Dola | : | Si huko ni kupigana busu! Mdomo bin mdomo! |
| Baba Dola | : | ... Lahaulah! Huyu, huyu Dola wangu! |

*(Msisitizo ni wetu)*

Tumeidondoa sehemu hii ya tamthilia kwa marefu kwa sababu imechangia ushahidi wa madai yetu kuhusu matumizi ya lugha pevu. Mama Dola anatumia mafumbo kufichia makali fulani hususan anapoongea juu ya mapenzi. Baba Dola hang'amui anachomaanisha mkewe haraka si kwa sababu mzee huyu ni bozi bali huenda alidhani kuwa hirimu ya bintiye haingemruhusu kujihusisha na *tabia chafu*. Utafiti wetu kadhalika ulidhihirisha kwamba, watoto wengi, isipokuwa pengine wale wanaozungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza, hawakung'amua upesi upesi alichokuwa akisema mama Dola, walielea mithili ya boya bandarini. Wengi wa watoto, kama alivyokuwa Baba Dola, walimakinika tu baada ya Mama Dola kufafanua zaidi. Lugha hii ya mafumbo bila shaka haiko katika mawanda ya watoto-lengwa.

Mbali na lugha hiyo ya tasfida, methali na nahau chekwachekwa zimetumika katika tamthilia hii. Methali zingine, hata hivyo, haziko katika urazini wa watoto-lengwa kama vile *kikosa mwaka na ruza, silimi vuli kachekwa; chagagana na ngangandu asamehewe; Samli ya Pemba*

*haimpati mtu macho (uk.xxxvi).* Watoto tuliowahoji walikiri kwamba hawakuelewa maana ya methali hizo. Kadhalika, ziliwawia ngumu kutamka. Iliwabidi waziseme kikasuku tu. Matumizi kama haya ya lugha huenda yakatatiza faka ya mtoto kustahabu matumizi ya methali katika mustakabali wao.

Mtunzi wa *Majuto* amefaulu katika matumizi ya sifa za kishairi za kinyambulizi kuundia sentensi na kuteulia msamiati. Anaunda msamiati kutokana na mzizi na hapo kuyapa mazungumzo kati ya wahusika mtiririko na mdundo wa kimziki. Mbinu hii iliibua hisi-mseto katika hadhira ya watoto. Hii hapa ni mifano michache:

.. Nimeangukiwa na *mlelema*... siwezi hata *kuhema* (uk.xxxv)
.. *Shamu* ... *Shamu* binti *Amu*... alidhani umepata *tende* kumbe umepata *mende* (uk.xxxvi)
.. Heri wewe *kilema*, mimi hivi unionavyo ni zaidi ya *kiselema* (uk.xxxvi)
.. haya si *majaaliwa* huku ni *kulaaniwa* (uk.xxxvi)

Japo watoto wengi hawakuelewa maana ya maneno yaliyonyambuliwa, mtiririko wa kimziki wa minyambuliko hii uliwapa burudani mzomzo. Lau mtunzi angenyambua msamiati ulio katika mawanda yao, licha ya kuburudika, watoto hao wangeelimika mno.

Sifa nyingine inayojitokeza katika tamthilia hii ni yale matumizi ya msamiati ambao si wa Kiswahili sanifu au ambao haujazoeleka na watumiaji wa Kiswahili. Ilisikitisha kuwaona watoto waking'ang'ana kutamka istilahi na msamiati 'unaojaza vinywa' na isitoshe, msamiati ambao katu hawauelewi maana. Utafiti wetu waaidha ulithibitisha kwamba wengi wa waigizaji walioyatumia maneno haya hawakuyaelewa maana. Waliyatamka kitarumbeta tu! Maneno yenyewe ni kama:

Maadal – basar (uk.xxxvii); Bon-Viyajz (uk. xxxviii)
Sakatal jabal (uk.xli); Swadakta, Aghstafiruu
(uk. xlii); Mamsatubuh (uk.xliii); Astalavista,
audhubilahi (uk.xliii)

Tulipomhoji mtunzi, alisadiki kwamba asasi ya maneno mengi ilikuwa lugha ya mitaani ya Mombasa na lugha ya Kiarabu. Aliyatumia ili aweze kuichangamsha hadhira lengo alilotimiza kwa hasara ya kuelimisha watoto.

### 4.2.3 *MONALISA*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA (Kiambatisho 3c)

Mgogoro mkuu katika tamthilia ya *Monalisa* unachimbukia katika aila ya bwana Luseka. Bwana huyu hataki bintiye (yaani Monalisa) aendelee na masomo. Harakati zake hizi zinashadidiwa na wanaume wengine wawili: Mwalimu Mkuu na Timothy (mwanafunzi-mwenza wa Monalisa). Kwa vile Monalisa ni kisichana kidogo, shauku yake ya kutaka kuendelea na masomo inatiwa kani na Tina (mamake) akisaidiwa na chama cha wanawake. Kwa jicho pekuzi, kuna makundi mawili kinzani ya wahusika katika mchezo huu: wahusika nguli wakiongozwa na Monalisa na Tina dhidi ya wahusika kinzani wakiongozwa na Luseka.

Luseka anasawiriwa kama mwanamume anayeongozwa na itikadi ya ubabedume anapitangaza nia ya kuoa bibi wa pili kwa sababu Tina alikuwa amefeli kumzalia mwana wa kiume. Kwake, mwana wa kiume ndiye angerithi mali yake na pia ndiye angeweza kumkinga wakati wa janga (uk. xlix). Luseka hamuoni bintiye kama ni mwana. Anamchukulia si kama tu kiumbe duni bali pia chombo cha kutumiwa na mwanamume jinsi anavyotamani. Anasema (uk.l):

> ... Kumfunza mvulana kweli ni sawa na
> kulifunza taifa zima lakini kumfunza
> msichana ni kama kunyunyizia maji
> shamba la jirani.

Mwalimu Mkuu anatumiwa na mtunzi kuivuvia itikadi hii ya ki-ubabedume. Monalisa anapodungwa mimba na Timothy, anayetimuliwa shuleni ni mwana wa kike huku mwana wa kiume, aliyeidunga mimba hiyo, akiendelea na masomo. Tuangalie anavyojitetea Mwalimu Mkuu (uk. lv).

> ... Nani atamruhusu kuku kukaa na vifaranga.
> Huoni kwamba vifaranga hao watajifunza kutaga
> mayai?

Mwalimu huyu haoni kwamba 'jogoo' anayewatagisha 'vifaranga' alikuwa angali mumo humo shuleni. Yumkini hali ikibaki iyo hiyo, bila shaka, 'kifaranga' mwingine huenda atatagishwa mayai. Jamii ya ki-ubabedume humwona mwanamke kama chombo cha kueneza maovu na uzinzi na ndiyo sababu anayelaumiwa ni Monalisa pekee yake huku Timothy akitukuzwa.

Suala linaloshughulikiwa na tamthilia hii ni suala-ibuka linalowahusu mabarobaro wala sio watoto. Kama tulivyoona katika *Majuto,* wahusika wanaoumbwa katika tamthilia hii ni aidha wazazi au vijana waliokwisha baleghe. Watoto hawana mhusika wa kujihususha naye. Kitendo cha wanafunzi kitiana mimba kinawatenga wahusika hawa kimasafa na watoto wenzao kwa vile maswala ya kushika mimba kwao watoto ni 'tabia chafu' kama tulivyoona katika tamthilia ya *Majuto*. Kwa mboni za watoto, wanafunzi walioshika mimba ni watoto walikosa adabu na wanafaa kuadhibiwa wala sio kukarabatiwa.

Tulipomhoji msichana aliyeigiza sehemu ya Monalisa,alikiri kwamba "kitendo cha kushika mimba kulinitia soni". Kama angepewa nafasi nyingine ya kuuigiza mchezo huo, aliapa kwamba hangeichagua nafasi hiyo. Ijapokuwa katika michezo ya utotoni watoto huigiza nafasi ya 'baba' na 'mama', ishara nzito nzito za ngono kama ilivyodokezwa katika *Monalisa* hazipigiwi debe. Na hii ndiyo sababu watoto walioigiza sehemu

ya Monalisa na ile ya Timothy walitahayarika. Hii ni ithibati kuwa, wahusika hawa hawakifinyangwa katika mawanda ya watoto.

Kuhusu lugha waliyotumia wahusika wa tamthilia ya Monalisa, hadhira ya watoto ilitatizika kiasi kuelewa maana ya jazanda zilizotumika. Hali hiyo haikutushangaza kwa sababu maswala yaliyoshughulikiwa yalikuwa ya kiutu-uzima na ilimlazimu mtunzi mara kwa mara kutoyatongoa ya pembeni kadamnasi ya watoto. Kwa mfano, baada ya ndoa kati ya Tina na Luseka, mtunzi anaeleza unyumba wao ifuatavyo (uk.li):

| | | |
|---|---|---|
| Luseka | : | Na hapo nakumbuka mdundo wa *msondo ngoma*.. nami *nikawa sogora.* |
| Tina | : | Nami nikasakata *rumba ya uzazi.* Nitasahau vipi *uchungu wa uzazi* niliouhisi! Bado nakumbuka Luseka. |

*(Msisitizo wetu)*

Si watoto pekee waliokosa kutafsiri hiyo sakata ya *msondo ngoma* na *rumba ya uzazi* iliyosababisha kuzaliwa kwa Monalisa. Watu wazima kadhalika, ilitubidi kupiga alinacha. Katika mahojiano yetu, mtunzi alisadiki kuwa ilimuia vigumu kuifasiri jazanda hiyo kwa vile ingewafedhehesha waigizaji.

Tina anapokosa kumzalia mumewe mwana wa kiume, mumewe anamfananisha na '*ardhi butu ambayo haitatoa mavuno tena*' (uk.liii). Tina anajitetea kwa kusema *teknolojia ya kisasa yasema kuwa ardhi yaweza kutoa mazao ikitunzwa vizuri* (uk.liii). Majibizano haya yanagusia maswala nyeti ya uzazi na jinsi iwawiavyo vigumu wazazi kumjibu mwana anapotaka kujua alikotoka, iliwawia vigumu wasimamizi wa mchezo huu kuyafumbua mafumbo haya. Hii ni ishara kwamba lugha hii haipo katika urazini wa watoto.

Lugha ya mafumbo haikukitwa katika mazungumzo ya watu wazima pekee; wahusika-watoto kadhalika walikuwa na mafumbo yao. Timothy na Monalisa wanapotongozana, yafuatayo ndiyo wanayoambiana (uk.liii-liv):

| | | |
|---|---|---|
| Monalisa | : | Ningekudanganya vipi huku *umenitanda akilini ....* Huoni umande unavyometameta kana kwamba ni vigae vya vioo vilivyopasuka. |
| Timothy | : | Matamshi yako yanaweza *kumtoa nyoka pangoni* Monalisa. Najihisi kama *kibogoyo aliyeota meno. Ningekuwa ndege, ningepuruka.* |
| Monalisa | : | Lakini huna mabawa. |
| Timothy | : | *Wewe ndio mabawa yangu* Monalisa. *Najiona nikiruka angani bila ya tahadhari yoyote hata ya jua linalonichoma.* Maneno yako ni kama ganga ganga ya mganga. Kwa ajili yako, naweza hata kujitoma baharini. Hata iwe na urefu upi. Mkono wako mwororo unaponiguza, hunifanya nihisi joto mwilini. |

*(Msisitizo wetu)*

Maneno haya bila shaka yanachangia hisia ainati. Kuna hisia za kusikia kutokana na sauti ya Monalisa ambayo inasemekana ina uwezo wa *kumtoa nyoka pangoni.* Kunazo hisia za mguso ambazo zina uwezo wa kusababisha halijoto kali mwilini. Watoto-lengwa huenda wasizielewe hisia hizi, zinaeleweka na mabarubaru na watu wazima. Watoto ukumbini walizielewa tu hizo hisia za kifantasia kama vile *kupuruka kama ndege na kujitoma baharini kuogelea.* Siks (1977) anapendekeza drama ya kifantasia kwa watoto kwa sababu wao huvutiwa na viumbe asilia. Katika maono na njozi, watoto hao huweza kupuruka kama ndege au kupiga mbizi ja samaki. Hawa ni watoto ambao chambilecho Alembi[3]:

> ... wangependa kushuhudia petali za maua
> zikifumbuka, kuwasikiza ndege wakiimba
> na yumkini kuimba nao, kuwawinda panzi na
> kuwachunga mithili ya wachungwavyo mifugo.
>
> *(Tafsiri yetu)*

Watoto aliofikiria Siks na Alembi bila shaka hawawezi kuzifasiri hisia za wahusika kama Monalisa na Timothy jinsi mtunzi alivyodhamiria. Hisia zao hizi ni za kimapenzi na bila shaka ni nzito kushinda tajriba ya watoto-lengwa. Hii ni kwa sababu ulimwengu wa mtoto ni ulimwengu wa kinjozi au kifantasia na wenye vitimbi jazila wala si ulimwengu asilia uliogoshi hisia zimwe kama vile ilivyo katika ulimwengu wa watu wazima (Lewis katika Fox 1976).

Lugha ya mwalimu katika tamthilia hii, ambayo ingetarajiwa kuwa sahili na iliyo kwenye kiwango cha watoto, waaidha imepita mawanda yao. Lugha ya mafumbo kama hiyo tuliyoichanganua hapo awali ndiyo iliyopigwa mwangwi katika mazungumzo kati ya mwalimu na mwanafunzi wake Monalisa alipoambiwa kuwa hangeruhusiwa kuendelea na masomo, kwa vile angewatagisha vifaranga wengine (*kama hapo juu*)

Ni maoni yetu kuwa, japo maswala aliyoyawasilisha yalikuwa ya kiutu uzima, mtunzi angechukua fursa hii kuwapa wanafunzi nyaadhi mzomzo ili wasitekwe bakunja na hisia zao za kimwili. Matumizi ya mafumbo kwa hivyo, yanasonga mawasiliano kati ya mtunzi na hadhira yake na papo kuusaki ujumbe nyeti na teketeke ambao ungewafaidi watoto.

Baada ya mimba ya Monalisa kuharibika, anarejeshwa masomoni na kusoma akitumia rasilimali iliyokongwa na umma. Lugha inayotumiwa na mtunzi kuwasilisha hali hii kadhalika ni ya kimafumbo. Hakimu na Hadhira wanamtia shime Monalisa kwa kusema (uk.lxi)

Hakimu : Na wee mwanangu, *vuka daraja la elimu.*

| | | |
|---|---|---|
| Hadhira | : | Vuka daraja Monalisa, vuka! |
| Monalisa | : | Lakini mheshimiwa, *kuna moto mvunguni*, naogopa! |

*(Msisitizo wetu)*

Ni dhahiri kwamba, Monalisa wa hadithi anang'amua fumbo la *kuvuka daraja* kwa vile tayari ana tajriba ya maisha ya kutosha. Je, Monalisa-mwigizaji na hadhira yake walilielewa fumbo hilo? Wengi tuliowahoji walitupatia fasiri mbalimbali. Wengine walidai kuwa Monalisa alikuwa ameogopa kuvuka daraja alipokuwa akienda shuleni na wenzake walikuwa wanamtia shime. Maoni hayo ni ithibati kuwa hadhira ya watoto haikung'amua maana batini ya fumbo hilo.

### 4.2.4 *VISOSAUTI*: WAHUSIKA NA MATUMIZI YAO YA LUGHA (Kiambatisho 3d)

Katika tamthilia ambazo tumezihakiki, *Visosauti* inasimama kama kielelezo kiwakilishi cha tamthilia ambayo wahusika wake walisawirika katika mawanda ya watoto. Tamthilia hii inajishughulisha na moja ya maswala-ibuka nyeti; watoto kufanyishwa kazi za shokoa. Hali hii imewamba si humu nchini au barani Afrika pekee bali ulimwengu mzima hasa katika mataifa yanayoendelea.

Mtunzi anawatumia watoto wa kike, Charity na Purity kama kielelezo cha kuakisi jinsi ukandamizwaji wa watoto ulivyosaki katika jamii. Jira ya kandamizi hizo ni watu wazima wakiwakilishwa na Susanna ambaye ni mama wa kambo wa hawa watoto (Charity na Purity). Wahusika kama Priscilla na Mathayo (mamao na babao watoto hao) pamoja na Daktari hawachukui nafasi kubwa katika tamthilia hii hata ingawa wanachangia pakubwa kuradili dhamira kuu.

Charity na Purity waliteka hisia za hadhira ya watoto tangu mwanzoni hadi mwisho wa maigizo. Sababu kuu ilikuwa kwamba, mandhari

ambamo mtunzi aliwafinyangia yaliakisi mazingira ambamo watoto hujipata mara kwa mara. Majina ya wahusika hawa yanaendana na sifa ambazo mwandishi alitaka zijitokeze waziwazi. Charity[4] kama jina lake linavyoakisi, kilijitokeza kama kisichana kilichosheni silika njema. Mtoto huyu alikuwa na ujasiri usio na hadhari ambao aghalabu hushuhudiwa tu katika maisha ya utotoni. Mara kwa mara hakuchelea kujitoa kama sadaka kwa minajili ya waliokuwa wakiteseka. Kwa mfano, alitia maisha yake hatarini ili kumwokoa Purity kutokana na makali ya upanga wa Konstantino (uk. lxiii).

Katika kiwanda cha kuchimba migodi, Charity alijitolea kuchomwa, badala ya Purity kwa chuma moto kilichotumiwa '*kuwachorea*' namba za kuwatambua wachimba migodi (uk.lxviii). Sadaka kubwa zaidi aliyoitoa ni alipompulizia Susanna pumzi za uhai kwa kumpa figo (uk.lxxv).

Tabia hii ya Charity inatudhihirishia kwamba binadamu wote wamezaliwa na chembe fulani cha utu. Mazingira yanayowakuza ndiyo yumkini huweza kuizizima chembe hiyo. Kupitia kwa mhusika huyu, watoto wanakumbushwa kuyaweka maslahi ya wenzao mbele ya maslahi yao. La mno, wanakumbushwa kuradili wema kwa kusahau udhalimu wa nduli walioghoshi duniani na badala ya kulipiza kisasi, wawasamehe wale wote wawatendeao maovu.

Purity[5], ingawa hashikilii nafasi kubwa katika mchezo huu, mtunzi wa tamthilia hii amefaulu kumtumia kusawiri usafi na utakatifu wa watoto utotoni. Mara nyingi watoto huitwa 'malaika' kwa sababu ya sifa hii. Utakatifu huu aghalabu hutiwa najisi na ulimwengu wa watu wazima. Utakatifu wa kitoto hiki unaonekana pale Kobra (nokoa katika kiwanda cha kuchimba migodi), anapojaribu kumpapasapapapasa Charity. Licha ya udogo wake, Purity anamkemea na kumuonya "*usimguse dadangu kwa mikono yako michafu*". (uk.lxvi)

Mapambano ya kujinasua kutokana na mikatale waliyotwikwa na wachimba migodi yanapopamba moto kiasi cha Charity kutaka kukata tamaa, Purity hamkatizi faka, anamtia moyo kwa kumkumbusha kuwa mapambano ya wanyonge dhidi ya wakandamizaji ni ya Mungu (uk.lxvi)

Watoto hawa wanapomkuta Susanna katika hali mahtuti, Purity ndiye anayemsihi mwenzake kumpa 'figo ya uhai' nduli huyu kwa kusema "....Kwani tuliishi kwa nini ikiwa hatuwezi kutumia maisha yetu aliyotupa Mungu kwa maisha ya mtoto mwingine wa Mungu". (uk.lxx).

Kama tulivyotakadamu kuona hapo kabla, mtunzi kadhalika alifanikiwa kumsawiri Purity kwa mboni za watoto. Yeye alitumiwa kama kielelezo cha utakatifu ambao watoto wametunikiwa na Mungu na hakuchelea kuikumbusha hadhira kuwa watoto wote walikuwa 'watoto wa Mungu' wawe wamekuwa wazima ama bado wangali wachanga (kama hapo juu). Waadhi huu ulipokelewa vizuri na watoto kwa sababu Purity alikuwa mtoto ambaye watoto wengine waliweza kujitambulisha naye ki-urahisi.

Katika mandhari ya shuleni na ya hospitalini, Mwalimu na Daktari ndio wahusika muhimu. Mwalimu anajitokeza kama mtetezi wa haki za watoto hasa wana wa kike. Kwa mfano, anapohutubia gwaride ya wanafunzi, anahimiza kwamba "chochote awezacho mume, mke aweza kufanya hata zaidi" (uk.lviii). Waama, aliwaonya wazazi kutowaondoa mabinti zao shuleni na kuwapeleka katika ulimwengu wa kufanya kazi kwa sababu aliwataka wasichana wasome kwa bidii ili waibukie kuwa mawakili, madaktari, wahandisi, mahakimu na hata wanasiasa (uk.lviii). Mawaidha haya bila shaka yanawatia shime watoto, hasa wa kike, kuupenya ulimwengu mtarazaki na kudai amali ambazo kwa muda mrefu zimetengewa wanaume.

Daktari tunayemuona katika mchezo huu ni yule ambaye watoto wamezoea kukabiliana naye hospitalini. Sifa yake ya utarazaki inajitokeza katika pirikapirika zake za kuyaokoa maisha ya Susanna na

kuitia mwapuza migogoro iliyokuwa imetamalaki maisha ya mama huyu na hao watoto wake wa kambo. Utulivu na kumakinika kwa Daktari kazini bila shaka ni mshawasha kwa watoto kutamani amali ya udaktari katika mustakabali wao.

Mtunzi anatumia mandhari ya nyumbani na yale ya kuchimba migodi kukuzia wahusika kinzani. Nyumbani tunaonjeshwa jazila ukatili na udhalimu wa Susanna. Mama huyu ni nduli. Alimuua Mathayo (bwanake), Priscilla (mke mwenzake) pamoja na kutaka kuwaua Purity na Charity (wanawe wa kambo). Washirika wake katika dhuluma hizo ni Konstantino na Kobra.

Japo mtunzi anawadididimiza wahusika hawa katika ujahili uliokithiri mipaka, anafaulu hatimaye kutukatia kibendo cha utu na ubinadamu wao kama ithibati kwamba, kila binadamu kajaaliwa utu kwa upande mmoja na unyama kwa upande wa pili. Matendo ya binadamu kwa hivyo, hutegemea nguzo inayohimili uamuzi wake. Kwa mfano, Konstantino anaonyesha utu anapomshawishi afriti Susanna kubadili nia ya kuwaua Purity na Charity kwa kupendekeza wauziwe kiwanda cha kuchimba migodi. (uk.lxiv) Uamuzi huo uliyaokoa maisha ya hao mayatima. Kibendo kingine cha ubinadamu tunakishuhudia Susanna anapowakubali Purity na Charity kama wanawe na kadhalika kuwarudishia urithi wao aliokuwa amewapokonya (uk.lxxv - lxxvi)

Wahusika hawa ijapokuwa walikuwa watu wazima, mtunzi amefanikiwa kuwashikamanisha vya kutosha na hadhira ya watoto kwa kukimega hicho kibendo chao cha utu. Hali hii inawafanya wakubalike katika ulimwengu wa watoto.

Kuhusu matumizi ya lugha, mwandishi amefaulu kuwakuza wahusika wanaomaanisha kile wanachokisema. Stevens John (1992:194) anasema:

> Fasihi ya watoto lazima imaanishe kile inachotarajia kumaanisha; ni lazima msomaji asome na kukomea papo hapo wala asisumbuke kutafuta fasiri zingine.
>
> *(Tafsiti yetu)*

Japo Susanna, Priscilla, Daktari, Mwalimu Mkuu na wengineo ni watu wazima katika mchezo huu, wanatumia lugha sahili. Mwandishi hayashadidii wala kuyaradidia mazungumzo yao mafumbo; anahakikisha kwamba wahusika hawa wanamaanisha kile wanachokisema. Mchezo ulipokunjuka, hadhira ya watoto haikusumbuka kukuna vichwa kwa kutafuta fasiri za semi za wahusika mara kwa mara kama tulivyoona katika mchezo wa *Majuto* na *Monalisa*.

Msamiati anaoutumia mtunzi kadhalika upo katika urazini wa watoto. Kwa mfano anatohoa istilahi mbali mbali kutoka kwa Kiingereza ili ladha ya ujumbe unaonuiwa kuuwasilisha isipotee. Hii hapa ni mifano michache:

Eksirei - *X-ray* (uk.xlix); Daktari - *Doctor* (uk.xlix);
O negative - *O- ve* (uk.l); Oparesheni – *Operation* (uk.lv)

Tulisema hapo awali kwamba watoto huvutiwa sana na viumbe asilia hasa ikiwa msanii katumia wanyama au wadudu kuwakilisha tabia na mienendo ya binadamu. Tashibihi na sitiari anazotumia mwandishi kwa hivyo, zinahusu wanyama au vitu ambavyo yamkini watoto wamewahi kukutana navyo katika mazingira yao mathalan:

... macho yako madogo ya *mwewe* (uk.liv)
... nyamaza ewe *mbwa mwehu* (uk.liv)
... uliwavamia kama *nzige* wanavyovamia *mimea* (uk. lviii)
... kama *nzi* aliyevutiwa na harufu ya *kinyesi* cha binadamu (uk.lxi)
... nitalipuka kama *bomu* (uk. lxii)
... nitawachinja mmoja baada ya mwingine kama *kuku* (uk.lxiii) n.k.

Ulinganishi kama huu wa waziwazi na ulio sahili unasaidia kuhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi umenata katika akili za watoto limbukeni bila kimeme.

Lugha ya ushairi inadhihirika mara kwa mara katika mchezo wa *Visosauti.* Kwa vile watoto hustahabu maumbo yenye ulinganifu, matumizi haya ya lugha yaliwachangamsha ajabu ukumbini. Katika utangulizi, watoto wanasema (uk.xlvii)

Tulieni... wanadamu tulieni
Sikilizeni.
Sikilizeni wimbo wetu
Wimbo wa waliohasirika
Na nyoyo zilizosumbuliwa.
Nyoyo zinazosafiri ardhi nzima zikiwa na uchovu zikitafuta
Zikipekua
        Zikiangalia

Shamba la Edeni lililopotea
Shamba la Edeni
Linalozua kilio cha furaha.

Tutazame tena watoto walivyolalamika dhidi ya ukandamizaji mwishoni mwa hadithi. Wanaimba (uk.lxxi)

Kuna uchungu kwenye ubinadamu
Kuna uchungu kwenye mioyo yetu
Kuna uchungu kwenye roho zetu
Kuna uchungu kwenye mawazo yetu
Kuna uchungu
Kuna uchungu pote pote

Mtunzi anatumia lugha hii ya kishairi kushadidi na kuradidi hisia za ndani za watoto kwa njia ambayo inazaa matokeo makubwa. Jukwaani watoto waliziimba hisia hizi na hapo kuzizima majonzi makubwa waliyokuwa wanayapitia. Kwa maoni yetu, mtunzi wa *Vososauti* amefaulu kwa kiwango kikubwa kugotanisha mchezo wa utotoni na uwasilishaji wa maswala mazito mazito. Waama, matumizi haya ya lugha

yanafanikisha kuwapa watoto ushirika, nguvu na shime ya kubadilisha hali yao ya maisha.

## 4.4 KIMALIZIO

Tahakiki yetu ya tamthilia za watoto zilizowasilishwa katika tamasha za drama za 2002 imezingatia tamthilia nne. Tamthilia hizo ni *Tuzo Azizi*, *Majuto, Monalisa* na *Visosauti* mtawalio. Kati ya tamthilia hizi, imebainika kwamba, tamthilia ya *Visosauti* iliyotungwa na Otieno Nyangla akishirikiana na Wenceslause W.K.E. Masinde na kuigizwa na watoto kutoka shule ya msingi ya *Maseno* ndiyo ambayo kipengee chake cha uhusika na kile cha matumizi ya lugha viko katika mawanda ya watoto walio na umri usiozidi miaka kumi na mitatu. Nyinginezo tumezichukulia zote kumbo moja kuwa zimelenga mabarobaro zaidi ya watoto wenye umri tulioutaja.

**TANBIHI.**

1. Hizi ni lugha za siri zilizoibushwa na vijana marika mijini (lugha za mitaa).

   *Sheng* ni lugha ambayo umbo lake la kisarufi limetokana na Kiswahili nao msamiati wake umetokana na lugha za kienyeji na Kiingereza.

   *Engsh* nayo, umbo lake la kisarufi limetokana na Kiingereza lakini msamiati wake umetoka lugha nyinginezo kama vile Kiswahili na lugha za kienyeji.

   Taz. *Sheng and Engsh: Development of mixed codes among the urban youth in Kenya.* Makala ya Mohamed H. Abdulaziz na Ken Osinde (uk.4-5). Makala haya hayana tarehe.

2. Hili ni neno kutoka lugha ya Kijaluo lenye maana ya *tisha, shtua.*

3. Taz. katika Alembi "*Children are not Miniature Adults*" *Some Reflections on Primary Schools' Category Scripts' of the Kenya Schools and Colleges' Drama Festivals* uk. 3. Makala haya yaliwasilishwa katika warsha ya wasanii mnamo Agosti 26-28, 2003 huko Mombasa Polytechnic.

4. *Charity* ni neno la Kiingereza. Kwa mujibu wa *English-Swahili Dictionary* (2001), neno hili linamaanisha *wema, fadhila, hisani* au *huruma.*

5. Kama hapo juu, *Purity* nalo lina maana ya *usafi, weupe* au *utakatifu.*

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 HITIMISHO

Tasnifu hii imehakiki drama ya watoto kama zao la michezo au maigizo ya utotoni. Kufanya hivyo, tumechunguza michezo ya utotoni kama awamu mojawapo ya maendeleo ya drama ya watoto. Tumechambua maudhui na fani katika tamthilia za watoto. Kuhusu fani, tumechanganua usawiri wa wahusika pamoja na matumizi yao ya lugha. Azma yetu imekuwa kutathmini kama vipengee hivi vya fani viko katika mawanda ya watoto.

Katika sura ya pili, tumeona kwamba asilimia 87 ya watoto walioshiriki katika michezo ya utotoni waliifurahia michezo hiyo. Tuliyachunguza maudhui muhimu ambayo hushughulikiwa, tukaona kuwa, yalikuwa pamoja na maswala ya kinyumbani, ya shuleni, ya hospialini, ya mijini na ya kibunilizi. Tumeonyesha kwamba maudhui hayo yamejengeka kwenye matukio ambayo watoto hukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku.

Sura hii kadhalika imechambua viambajengo muhimu ambavyo huijenga michezo ya utotoni. Tumeona kwamba ploti ya michezo ya utotoni huwa sahili na hukunjuka kwa kasi. Wahusika wa michezo hii huwa ni watoto wa hirimu moja au wale viumbe wanaopatikana katika mazingira ya watoto. Ikiwa viumbe hao ni wanyama au wadudu basi watawakilisha tabia na mienendo ya binadamu. Mandhari ya maigizo ya utotoni tumegundua yana uhalisi wa kijiografia na hakuna jukwaa maalum wala

sheria mithaki. Katika kuteua maleba ya kusawiria wahusika pamoja na hali anuwai wanazoigiza, tumeona kuwa watoto hufanya ufaragusi sahili.

Aidha, tumeona kwamba michezo ya utotoni ina uamilifu mkubwa maishani mwa watoto. Licha ya kuwaburundisha, michezo hii ni nyenzo muhimu ya kuwaelimisha watoto. Maadili kama umoja wa jamii, heshima stahili kwa watu wazima na ukashifu wa tabia zipingazo mwingiliano wa kijamii mathalan ulafi au anasa hufunzwa kupitia michezo hii.

Sura ya tatu imeonyesha kwamba japo mengi ya maudhui yanayoshughulikiwa katika drama ya watoto wa shule za msingi yamejengeka kwenye matukio yanayohusiana na mazingira ya watoto, fasiri ya maudhui hayo haipo katika mawanda ya watoto-lengwa. Tumeona kwamba watunzi wengi wameyashindilia maudhui ya tamthilia za watoto hayo hisia za kiutu uzima. Watoto kwa hivyo wamebakia kuyawasilisha kikasuku maswala ambayo aghalabu hayawahusu moja kwa moja.

Katika sura ya nne, tumeona kwamba wengi wa wahusika wakuu ambao walipewa jukumu la kuendeleza tendo kuu katika drama ya watoto walikuwa aidha mabarobaro au watu wazima. Haikuwa rahisi kwa hivyo, kwa hadhira ya watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na mitatu, kujihusisha na wahusika kama hao kwa vile ilikuwa nadra kuwapata katika michezo ya utotoni kama ilivyodhihirika katika sura ya pili. Watoto wachanga, tumeonyesha, walichangamshwa na drama ambayo iliwahusisha marika zao kama wahusika katika tendo kuu la kidrama ama iliyowahusisha wahusika wa kifantasia. Wahusika wa kifantasia ni wale wa kinjozi ambao wana nguvu ajabu, ujasiri mwingi pamoja na uwajibikaji na wanaoweza kutatua matatizo makubwa makubwa.

Waama, tumeona kuwa lugha iliyotumiwa katika nyingi ya tamthilia za watoto ilisheheni mafumbo ambayo watoto hawakuyamaizi. Hii ni lugha

ya kiutu uzima ambayo hailingani na urazini wa watoto. Watoto tumegundua wanavutiwa na lugha yenye mipigo ya kishairi na hususan lugha inayomaanisha kile inachotarajia kumaanisha. Wala sio lugha ya kimafumbo.

Mpaka hapa, ni dhahiri kwamba, nyingi ya ishara ambazo watunzi wa tamthilia za watoto hutumia katika drama ya watoto haziko katika mawanda ya watoto-lengwa. Haya yanakwenda sambamba na nadharia tete ya utafiti wetu.

## 5.2 MAPENDEKEZO

Ili kuiboresha drama ya watoto, utafiti wetu unapendekeza yafuatayo:

1. Kwa vile watoto wengi wanapenda drama, michezo au maigizo ya utotoni yakuzwe katika shule chekechea na za msingi kote nchini. Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi itambue michezo hii kama mojawapo ya michezo ya mtaala-mwenzi na kuitengea muda maalum kama ilivyo katika michezo mingine mathalan riadha na michezo ya mpira. Tumegundua kwamba shule zingine za msingi zinatumia muda wa mapumziko au wa michezo kufunzia mafunzo ya ziada au kuwaadhibia watoto. Hali hii inawanyima watoto fursa muhimu ya kujihusisha katika michezo ya utotoni.

2. Kwa vile tamasha za drama za shule na vyuo ambazo huandaliwa kila mwaka na Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi ndilo jukwaa la kipekee la drama ya watoto, wizara ihakikishe kwamba tamthilia zinazowasilishwa na watoto katika tamasha hizi ziko katika mawanda yao. Hili litawezekana kama kwanza, watunzi wa tamthilia za watoto watahimizwa kujenga maudhui ya tamthilia hizi kwenye matukio ambayo hushughulikiwa na watoto katika michezo au maigizo ya utotoni. Pili, uteuzi wa wahusika na lugha wanayoitumia

vinapaswa kulingana na urazini wa watoto. Tatu, watoto-washiriki wahusishwe katika utunzi wa tamthilia zao.

3. Kwa vile njia mojawapo ya kupimia ufanifu wa tamthilia ni pale inapoigizwa jukwaani, uamuzi katika mashindano ya shule za msingi ya tamasha za drama za shule na vyuo uzingatie uwezo wa mchezo wanaouigiza watoto wa kudhibiti mazingira ya watoto pamoja na kufaulu kwa mchezo huo kuwafanya 'watoto wabakie watoto' katika maigizo.

4. Warsha kwa watunzi wa tamthilia za watoto ziandaliwe kote nchini mara kwa mara. Azma ya warsha hizi iwe kuwatangamanisha watunzi wa tamthilia za watoto na kuwapa fursa ya kunoa mbinu zao za kiutunzi kama vile, uteuzi wao wa maudhui pamoja na fani mwafaka ya kuyawasilishia.

5. Kwa vile tamthilia za watoto zilizochapishwa ni chache mno, watunzi wa drama ya watoto wahimizwe kutohoa michezo kutoka kwenye kazikigezo za fasihi ya watoto zilizotungwa katika Kiingereza mno mno zile ambazo mazingira zinazoyasawiri yanashabihiana na yale ya watoto-lengwa. Kazikigezo kwa mujibu wa Mbatiah (2001) zina sifa ya kuwa kazi mwanana zilizotungwa na waandishi ambao, kwa makubaliano miongoni mwa wataalamu, wahakiki, walimu na wasomaji, wametambuliwa kuwa wakuu. Kazikigezo zitawapa watunzi mwongozo mufti wa kutungia tamthilia zilizo katika urazini wa watoto.

6. Utafiti wetu ulishughulikia vipengee viwili vya fani: wahusika na matumizi yao ya lugha. Utafiti zaidi kuhusu vipengee vinginevyo vya fani unahitajika. Aidha, mada hii tuliyoshughulikia inaweza kufanyiwa utafiti na watafiti wengine kwa kutumia mielekeo mingine ya kinadharia.

**MAREJELEO**


Alembi, E. B. (2000) *Appreciating Drama.* Nairobi, Acacia Stantex Publishers.

Alington, F. A. (1961) *Drama and Education.* London, Basil Blackwell & Mott Ltd.

Courtney, R (1974) *Play, Drama and Thought.* London, Macmillan

Davies, G (1983) *Practical Primary Drama.* London. Heinmann.

Davies, J.H and Mary Watkins (1960) *Children's Theatre.* New York, Harper and Row.

Elam, K. (1980) *The Semiotics of Theatre and Drama.* London, Methuen.

Fox, G. et al (1978) *Writers, Critics and Children.* New York, Agathon.

Gill, R. (1985) *Mastering English Literature.* Houndmills, Macmillan Education Ltd.

Jackson, T. (1980) *Learning Through Theatre.* London, Manchester University.

Kabui, E. W. (1997) *The Status of Children's Theatre in Nairobi.* Tasnifu ya M.A. Haijachapishwa.

Kamera, W.D.(1978) *Fasihi Simulizi na Uandishi katika Shule za Msingi.* Dar es Salaam, Institute of Kiswahili Research.

Kenya National Drama Festival (2000) *Kenya National Drama Festival: Revised Rules & Regulations.* Nairobi Ministry of Education.

Kingei, K. (2003) 'Criticism of Literature in Kiswahili: Bridging the Gaps' Makala katika *The Nairobi Journal of Literature, University of Nairobi.*

Kithaka wa Mberia (2003) 'Kiswahili and other Indigenous Kenyan Languages in the Performing Arts'. Makala katika *The Nairobi Journal of Literature, University of Nairobi.*

Mbatiah, M (2001) *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi, Standard Textbooks Graphics & Publishing.

Mlama, P.O. (1979) *The Mass Media and Culture Relevant to the Child; In Early Childhood and Education.* A Report on the International Year of the Child, Dar es salaam.

Mpesha, N. (1995) *Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth & Development.* Tasnifu ya PHD. Haijachapishwa

Msokile, Mbunda (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi, East African Educational Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Odhiambo, C. (2000) 'The Aesthetics of theatre For Community Development in Kenya'. Makala katika *The Nairobi Journal of Literature, University of Nairobi.*

Omari, C.K. na Mvungi, M (1980) *Urithi wa Utamaduni Wetu.* Dar es Salaam,Tanzania Publishing House.

Senkoro, F.E.M.K (1982) *Fasihi.* Dar es Salaam, Press & Publicity Center.

Siks, G.B. (1958) *Creative Dramatics: An Art For Children.* New York, Harper And Row.

______________ (1978) *Drama with Children.* New York, Harper and Row

Slade, P. (1973) *An Introduction to Children's Drama.* London, University of London Press.

Stephens, John (1992) *Language and Ideology in Children's Fiction.* London, Longman.

Syambo, B. na Alamin, M. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi.* Nairobi, East African Educational Publishers.

Wafula R.M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W.(2002) *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi, Phoenix Publishers ltd.

*(2003)* *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi, Focus Publications Ltd.

*(2003)* *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi, Focus Publications Ltd.

## KIAMBATISHO 1A

## HOJAJI KWA WATOTO.

*Sehemu ya A. (Mwalimu atoe usaidizi)*

1. Shule yako inaitwaje?..................................................................
...................................................................................................

2. Shule yako inapatikana katika mkoa gani? ..................................
...................................................................................................

*Sehemu ya B. (kwa mwanafunzi).*

1. Una umri wa miaka mingapi?......................................................
...................................................................................................

2. Wakati wa mapumziko shuleni (break time) huwa unafanya nini?

| | |
|---|---|
| Kusoma vitabu vya hadithi | |
| Kucheza na marafiki | |
| Kupiga gumzo na marafiki | |
| Kinginecho (taja). | |

3. Kwa nini unatumia wakati wako wa mapumziko kwa jinsi hii? ...
...................................................................................................
...................................................................................................

4. i) Mkicheza na marafiki zako, mnapenda kucheza michezo gani? Taja miwili: a) ................................................................
b) ................................................................

ii) Umewahi kucheza michezo ambapo unajifanya kuwa mtu mwengine kama vile mwalimu, baba, askari n.k.?

iii) Mchezo kama huo huwa mnauitaje?...........................................
...................................................................................................

iv) Mlipoucheza mchezo huo ulijifanya kuwa nani?..........................
...................................................................................................

v) Ni nani aliyekuchagua?

| | |
|---|---|
| Mimi mwenyewe | |
| Wenzangu | |
| Mwingineyo (taja) | |

vi) Kwa nini ulijichagua au ulichaguliwa kuchukua nafasi hiyo?
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

vii) Uliifurahia nafasi hiyo?

a)

| | |
|---|---|
| Ndio | |
| La | |

b) Kwa nini? ..........................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

viii) Ungali unaucheza mchezo huo?

a)

| | |
|---|---|
| Ndio | |
| La | |

b) Ikiwa uliacha kuucheza, ulikuwa na umri gani ulipoacha kuucheza? ..........................................................................

ix) Ni mafunzo gani muhimu unayoyapata kutokana na mchezo huo?
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

x) Ni mambo gani muhimu yanayoweza kufanywa ili kuufanya mchezo huo uweze kuvutia zaidi? ..........................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

5\. i) Umeshiriki katika tamasha za shule na vyuo kwa miaka mingapi?..........................................................................
..........................................................................................

ii) Taja majina ya michezo ambayo umeweza kuigiza mpaka kiwango cha mkoani au cha kitaifa..........................................................
..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................

iii) Mchezo mlioigiza mwaka huu unaitwaje? ....................................
..........................................................................................
..........................................................................................

iv) Mchezo huu uliandikwa na nani? ..............................................

.....................................................................................................

v) Ni nafasi gani uliyoigiza katika mchezo huu? ..............................
.....................................................................................................

vi) a) Ni nani aliyekuchagua?.........................................................................
.....................................................................................................

b) Kwa nini? .........................................................................................
.....................................................................................................

v) a) Ni nafasi gani iliyokupendeza zaidi katika mchezo huu?................
.....................................................................................................

b) Kwa nini? .........................................................................................
.....................................................................................................

vi) Ni mafunzo gani uliyoyapata kutokana na mchezo huo?..............
.....................................................................................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................

vii) Ni matatizo gani uliyoyapata

a) Wakati wa kuusoma mchezo huu? ..........................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................

b) Wakati wa kuugiza ..............................................................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................

6. Kama ungepewa nafasi nyingine kuuigiza mchezo huu ni mabadiliko gani ambayo ungependekeza yafanywe ....................
.....................................................................................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................
.....................................................................................................

## Kiambatisho 1B

### HOJAJI KWA WATUNZI/WALIMU

1. i) Jina lako ni nani?..........................................................................
.............................................................................................

ii) Jina la shule yako.........................................................................
.............................................................................................

iii) Shule yako inapatikana katika mkoa gani? ...........................
.............................................................................................
.............................................................................................

2. i) Taja majina ya tamthilia ambazo umeweza kutungia watoto kwa miaka mitano ambayo imepita.................................................
.............................................................................................
.............................................................................................
.............................................................................................
.............................................................................................

ii) Ni tamthilia gani ambazo ziliweza kufika kiwango cha mkoa katika tamasha za shule na vyuo?.................................................
.............................................................................................
.............................................................................................

3. i) Ni masuala gani ambayo umeyazungumzia katika tamthilia ya mwaka huu?.................................................................................
.............................................................................................
.............................................................................................

ii) Karisha au ithamu (inspiration) ya kutunga tamthilia hii uliipataje? ................................................................................
.............................................................................................

iii) Tamthilia hii ilikuchukua miezi mingapi kuikamilisha.

| | |
|---|---|
| 1 - 3 | |
| 4 - 6 | |
| 7 - 9 | |
| 10 - 12 | |
| 12 na zaidi | |

4. Ni sifa zipi ulizozingatia katika kuwateua waigizaji wa tamthilia hii?.........................................................................................
.............................................................................................
.............................................................................................

5. i) Kati ya tamthilia ambazo umeweza kuwatungia watoto ni ipi iliyowavutia zaidi? ....................................................................
........................................................................................

ii) Kwa maoni yako, ni sifa zipi zilizowavutia sana ..........................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

6. Taja matatizo ambayo umewahi kukumbana nayo.

i) Katika harakati za kuwatungia watoto tamthilia..........................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

ii) Katika kuwasilisha tamthilia hizo jukwaani..................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

iii) Uliyakabili vipi matatizo hayo? ..................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

7. Kama ungepewa fursa nyingine kuitunga tamthilia hii na kisha kuiwasilisha jukwaani,

i) Ni mabadiliko gani ambayo utayapa kipeo cha mbele................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

ii) Kwa nini? Toa sababu ............................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................
........................................................................................

**Ahsante sana.**

## Kiambatisho 2a

*TUZO AZIZI*

*Tuzo Azizi* ni tamthilia iliyotungwa na Ndugu Isaiah Otieno, mwalimu wa drama katika shule ya msingi ya *Precious Gift*. Tamthilia hii iliwasiliswa katika mashindano ya drama ya shule na vyuo ya mkoa wa Nairobi mnamo tarehe 7 Mechi, 2002.

**Tamthilia kwa ufupi**

Kama ambavyo kichwa chake kinavyodokeza, tamthilia hii inahusu zawadi mufti anayostahili kutunukiwa mwalimu mwenye bidii na nidhamu kazini. Aghalabu, sifa hizo hupuuzwa wakati wa upandishaji walimu vyeo kwa sababu za ufisadi na mapendeleo.

Mwanzoni mwa mchezo, wanafunzi, walimu, pamoja na mkurungenzi wa shule wana bashasha kubwa kwa sababu shule yao ilikuwa imeibuka na ushindi katika mtihani wa kitaifa. Waandishi wa gazeti fulani wanamhoji mkurugenzi ambaye anajirundikia sifa kwa kudai kwamba matokeo hayo mazuri yalikuwa yametokana na uongozi kabambe ambao yeye hupeana.

Kwa vile Kiingereza ndilo somo lililotia fora zaidi ya mengine, aidha wanamhoji mwalimu ambaye alifunza somo hili. Mwalimu yuyu huyu ndiye hufunza drama, mchezo ambao kadhalika, hunawiri kuliko mingineyo shuleni humo. Anapoulizwa kilichosababisha matokeo hayo mazuri anasimama tisti na kusema kuwa ilikuwa nidhamu na bidii kazini. Jibu hili linamuudhi mkurugenzi na ndilo linalojenga mgogoro mkuu katika mchezo huu.

Mgogoro huu unapaliliwa na kunyunyuziwa fitina na mwalimu mkuu ambaye kadhalika anamwonea kinyongo mwalimu huyu. Isitoshe, mwalimu huyu hapewi amani nyumbani kwake na mkewe. Fitina za mwalimu mkuu zinamfanya mama huyu aamini kwamba mumewe hampendi na anaposhinda shuleni huwa yuko kwa kidosho mwingine. Mambo yanamwendea mrama zaidi Tusker, mbwa wake, anapomuua sungura wa shule.

Kifo hiki cha sungura, kilimpa mwalimu mkuu mwatuko wa kupenyezea fitina zaidi. Anamtia pumzi mkurugenzi kwamba mwalimu huyu wa drama ndiye aliyetenda kitendo hicho cha unyama na alikitenda maksudi. Mkurugenzi hana lingine ila kumpiga kalamu mwalimu huyu anayependwa na wanafunzi wote kwa bidii yake kazini.

Kisadfa, mkurugenzi na mwalimu mkuu wanafumaniwa wakila njama hiyo ya kumtimua mwalimu kazini na mkewe mwalimu huyo. Wanamhonga kwa shilingi elfu mbili ili asiifichue siri hiyo. Kwa vile ndoa yao ilikuwa imeanza kutumbukia nyongo, bibiye anakubali kunyamaza pengine akifikiri kwamba akifutwa kazi, basi mwalimu atakuwa nyumbani siku zote na hivyo mapenzi yao yatachachawa.

Wingu la mtafaruku linaitanda jamii ya mwalimu wanafunzi wanapoleta shati alilokuwa amevaa huku limeloa damu chepechepe. Wakati uo huo, mwenye pikipiki anawasili na kuripoti kuwa 'mgonjwa' alikuwa ameaga dunia. Ushahidi huo wote ulithibitisha kwamba mwalimu wao kipenzi ndiye aliyekuwa amefariki kutokana na ajali ya barabarani. Wanafunzi wanaanza kuandamana huku dole lao la lawama limeelekezwa mwalimu mkuu. Waaidha, wanaitisha mabadiliko katika uongozi wa shule yao. Wanachukua sheria mikononi mwao na kuamua kumuua mwalimu mkuu kama adhabu ya kumuua mwalimu wao kipenzi.

Katika hekaheka za kumtoa roho mwalimu mkuu, ghafla, mwalimu 'mfu' anajitokeza! Ukweli anajidhihirisha; aliyekufa kwa kugongwa na pikipiki ni Tusker na mwalimu alikuwa ametumia shati lake kufungia majeraha aliyoyapata mbwa huyo. Kadhalika Sungura wa shule hakuuliwa na mbwa wa mwalimu, mwanafunzi mmoja alikiri kumuua. Tusker alimfukua tu alikozikwa na mwanafunzi huyo.

Njama ya kumfuta kazi mwalimu haifui dafu. Ukweli umempambazukia mkurugenzi na papo hapo anamtimua kazini na kadhalika ofisini mwalimu mkuu. Wadhifa huu, kwa nguvu za umma, anamkabidhi mwalimu wa Kiingereza na Drama.

Hilo ndilo tuzo azizi kwa mwalimu mwenye bidii na nidhamu.

**Kiambatisho 2b**

*MAJUTO*

Tamthilia hii ilitungwa na wasanii chipukizi wa drama ya watoto: mwalimu Khamis Johnson Kanganji na Athuman Mohamed Amani. Wasanii hawa wana tajriba ya miaka mingi ya kutungia watoto tamthilia. Pamoja na mchezo huu, wamewahi kutunga *Jakamoyo* (2003) na *Gaetano* (2004) na kuiwasilisha hadi mashindano ya kitaifa. *Majuto* uliwasilishwa na shule ya msingi ya Nyali mnamo Aprili 2002.

**Hadithi kwa ufupi.**

Hadithi ya tamthilia ya *Majuto* inamzunguka Majuto bintiye waziri wa Afya. Majuto ameambukizwa Ukimwi, uwele ambao hauna tiba. Anakata kauli kuacha shule na ili kuiepusha aila yake fedheha iliyokuwa imeikodolea macho, anaamua kujitia kitanzi. Shamu, mwandani wake, anamsihi asikate tamaa maishani na kumtaka warudi shuleni lakini anadinda.

Babake Majuto anaamua kumfukuza bintiye licha ya maombi ya msamaha kutoka kwa mamake na Majuto mwenyewe. Mamake Majuto kadhalika anazolewa na wimbi la hasira za bwanake na kufukuzwa nyumbani baada ya kumlaumu bwanake kwa kuthamini cheo chake cha uwaziri kuliko bintiye. Aila ya Waziri wa Afya inasambaratishwa na nduli, Ukimwi.

Baada ya kutimuliwa kwao, Majuto anapokelewa na Baba Dola. Huyu ni nduguye Baba Majuto wa toka nitoke. Yeye na familia yake waliishi mjini kwa Baba Majuto kwa sababu hawakuwa na kazi. Baba na mama Majuto, licha ya utajiri wao na kuishi kwao katika kasri kubwa, waliamua kuifukuza aila ya Baba Dola ambaye sasa anafanya uvuvi kijijini.

Migogoro hii inafikia kilele inapogundulika kwamba Majuto hakuambukizwa Ukimwi kupitia uasherati jinsi babake alivyoamini. Alinajisiwa na *mashifta** baada ya basi yao kutekwa nyara walipokuwa wakielekea shuleni. Baba Majuto anamwomba bintiye msamaha kwa yote aliyokuwa ameyafanya. Majuto anatupilia mbali jaribio la kujitia kitanzi. Anawasamehe wote waliombagua. Wote wanarudiana.

---

* *Hawa ni majambazi wenye asili ya Somalia ambao huhangaisha wasafiri katika mkoa wa Kaskazini Mashariki.*

## Kiambatisho 2c

### ***MONALISA***

*Monalisa* ni tamthilia iliyotungwa na Masinde W.K.E. Wenceslause. Mchezo huu uliigizwa katika tamasha za shule na vyuo mkoani Magharibi na shule ya msingi ya Mtakatifu Anna-Mumias mnamo Mechi 2002.

**Hadithi kwa kifupi.**

Monalisa ni msichana mwerevu sana shuleni. Ana azma ya kuwa rubani baada ya masomo yake ili aweze kuwa kielelezo kwa wanawake ambao wamekandamizwa na kudhalilishwa na wanaume. Kutimiza ndoto hii, anang'ang'ana na vizuizi vingi vilivyokita mikuki katika itikadi kongwe ya ki-ubabedume.

Mchezo unapoanza, Tina (Mamake Monalisa) na Luseka (babake) wanagombana kwa sababu Luseka alikuwa amekata shauri kuoa bibi wa pili. Sababu anayoitoa ni kuwa, Tina alikuwa ameshindwa kumzalia mtoto wa kiume ambaye angeweza kurithi mali yake. Mgongano huu unachachawa Luseka, kutokana na shinikizo la hii itikadi ya ki-ubabedume, anapoamua kukatiza kisomo cha Monalisa kwa sababu kwake, kumwelimisha mwanamke ni sawa na 'kunyunyizia maji shamba la jirani'. Uamuzi huo unazima ndoto ya Monalisa kujiunga na shule ya upili licha ya yeye kupasi kwa alama za juu sana. Tina naye anaamua kwamba, bintiye atasoma liwe liwalo. Anaandaa mkutano wa kumchangia pesa za kuendeleza masomo. Kutokana na ushirika wa wanawake wenzake, wanafaulu kumpeleka msichana huyu shuleni.

Huko shuleni, maskini Monalisa anatekwa bakunja na mapenzi ya Timothy, mwanafunzi mwenzake. Inapogundulika kwamba alikuwa ana mimba, Mwalimu Mkuu anamtimua shuleni kwa kudai kuwa 'kuku akiruhusiwa kukaa na vifaranga bila shaka atawafunza kutaga kabla ya

wakati wao'. Ajabu ni kuwa, Timothy hakufukuzwa shuleni; alitandikwa viboko sita na kupewa kazi ya kusafisha vyoo kwa wiki moja! Hakuna kielelezo bora zaidi cha ukandamizaji wa mwanamke kama uamuzi huo wa Mwalimu Mkuu.

Mimba hii inasababisha mgongano zaidi katika aila ya Luseka. Madadi yanampanda mume huyu mpaka anaamua kumuua binti yake kwa bunduki. Tina kuona hivyo, anajitoa mhanga kwa kuizuia risasi isimfikie Monalisa. Papo hapo, maskini mama huyu anauawa. Kisadfa, mimba aliyokuwa ameibeba Tina, inaharibika. Luseka anatiwa mbaroni na kuhukumiwa kifo na korti ya umma. Monalisa anarejeshwa shuleni ambako anatia bidii mpaka anafaulu na kutuzwa digrii. Mwishoni mwa mchezo, umma kwa kauli moja, unamchangua Monalisa kuwa kiongozi wao na hapo anapata fursa ya kuendeleza kazi aliyoacha marehemu mamake: kazi ya kuwapulizia wanawake wengine mawazo ya kiukombozi.

## Kiambatisho 2d

*VISOSAUTI*

Tamthilia hii ni utunzi wa Masinde W.K.E. Wenceslause akishirikiana na Otieno Nyangla. *Visosauti* iliwasilishwa katika mashindano ya mkoa ya tamasha za shule na vyuo na shule ya msingi ya Westlands kutoka mkoa wa Nairobi mnamo Mechi 2002.

**Hadithi kwa kifupi.**

Hadithi ya *Visosauti* inamulika mateso ambayo watoto hatima hukumbana nayo maishani mwao. Mahatima hukandamizwa na kudhalilishwa na wazazi wao wa kambo. Hali huwa mbaya zaidi kama mahatima hao ni watoto wa kike na wanalewa katika ndoa ya wake wengi.

Mzee Mathayo alikuwa na bibi wawili, Susanna na Priscilla. Priscilla alijaliwa kumzalia binti wawili, Charity na Purity. Kawaida ya uke-wenza, Susanna alimwonea mke mwenzake wivu na unyambi. Aliamua kupanga njama ya kumuua Mzee Mathayo pamoja na Priscilla ili aweze kurithi mali ya aila hiyo pekee yake hasa shamba la aila hii ambalo lilikuwa na almasi.

Baada ya kutimiza njama ya kwanza ya kishetani, ukatili wake unamea mabawa zaidi na kumvusha hadi hatua ya juu zaidi ya mauaji. Anakataa kuwalipia karo hao mahatima na papo hapo kuiua tamaa ya Charity ya kuwa daktari. Hata hivyo, mpango wake wa kurithi shamba lenye almasi unapiga mwamba. Wakili anamshauri kwamba urithi huo haungewezekana bila idhini ya Charity.

Kwa vile Charity alikuwa kashagundua kuwa mamake wa kambo ndiye aliyewaua wazaziwe, anadinda kuziwekea stakabadhi idhini. Susanna

anakasirika na kuamua kuwaua wototo hawa wawili. Konstantino, mshirika wake katika njama hizo zake, anamshauri kutowaua. Maskini mahatima hawa 'wanauzwa' katika kiwanda cha wachimba migodi kufanya kazi za shokoa. Hii ilikuwa njia nyingine ya kuwaua kwa sababu ilikuwa nadra kwa watoto kutoka katika kiwanda hiki wakiwa hai.

Katika kiwanda cha kuchimba migodi, watoto wanapitia mateso mengi kama vile kucharazwa mijeledi, kuchorwa namba miilini kwa chuma moto, kufanyishwa kazi ya shokoa na kunyimwa chakula. Watoto lukuki wanapoteza maisha yao. Hali hii inamfanya Charity awazindue wenzake ili wajinasuwe kwa minyororo hiyo kandamizi. Wenzake wanaitikia na kuanzisha vita dhidi ya walinzi wao. Ingawa wengi waliangamizwa, Charity na Purity walinusurika.

Nyumbani, Susanna alikuwa katika hali mahtuti. Uwele wa figo ulitisha kuipokonya roho yake kama hangepewa figo nyingine. Figo hiyo 'mpya' ingetoka tu kwa mtu mwenye damu ya (O-) na aliye na umri usiopungua miaka kumi na mitano. Kisadfa, ni Charity peke yake ndiye aliyetimiza masharti hayo. Charity aliombwa kuyaokoa maisha ya mamake wa kambo lakini alikataa katakata; alitaka kulipiza kisasi. Alimtaka Susanna afe kama malipo ya kuwaua wazazi wake na isitoshe, kutaka kuwaua yeye na Purity.

Baada ya ushawishi wa muda mrefu kutoka kwa Purity, Charity anaulegeza msimamo na kutoa figo yake kama sadaka ya kumrejeshea 'uhai' nduli Susanna. Kitendo hiki chenye utu na ubinadamu kinamgusa sana Susanna mpaka anawarejeshea mahatima hawa urithi wao wote.

# TUZO AZIZI

*NA OTIENO ISAIAH*

hari ni ya shule. Walimu wanaonekana wenye bashasha mno kisa na maana; matokeo
-i katika mtihani wa ghaya. Mkurugenzi wa shule, mama, akiwapongeza walimu.

a : Walimu wateule, au niseme watukufu.
Kweli mgaagaa na upwa…………

mu : Hali wali mkavu.

a : Leo nina furaha kama tasa aliyejipatia mwana.
Mwenyezi Mungu atunukiwe sifa zake.

mu : Amina!

a : Mungu hamtupi mja wake. (*Akiongoza wimbo*)
Pendo langu na Yesu si pendo la nyama choma…..
Na tuombe

Mwalimu wa kwanza anajitokeza kuongoza maombi.

limu : (*Akiimba*) Muzina….

mu : (*Wanajibu*) Muzina kitata, yebi mwana, yebi tele……..

: Mkurugenzi anatoka ghafla jukwaani huku walimu wakipiga gumzo

alimu 1 : Imekuwa kiroja. Kwa mara ya kwanza nimemwona mama akiwa na furaha. (*Kwa stihizai*) – Nimepata kuona hata magezo yake.

alimu 2 : Huu basi ndio wakati wa kuvuna tulichopanda jangwa lile ambalo mimi huita meza sasa labda litapata angaa kijisahani cha sukumawiki na tonge la ziada. Matumbo sasa yatashitaki njaa.

alimu 1 : Ungalifahamu unachokisema, pengine ungalifyata ulimi wako mrefu. Nani hamtambui mama. Waulize wajuao.

alimu 2 : Asiyeweza kutambua ubora wa matokeo haya labda nimrudike kati ya wale wenye akili punguani au awe ni maiti si mtu.

mu : Kwani huna habari kuwa umtukuzaye huyo ni maiti atembeaye?

imu 1 : La upenuni halisemwi nje, hata hivyo mwalimu wa lugha ya kimombo atambulikaye kote kote toka Misri hadi Afrika Kusini kama siye huyu azungumzaye basi bado hajazaliwa - Matokeo yamedhihirisha.

mu : (*Wote wanamaka*) Aah!

limu : Ukweli ukidhihiri, uongo hujitenga.

mu : Aah!

*(Mara wanaingia waandishi wa habari)*

ndishi 1 : Tumekuja kujumuika nanyi siku hii ya leo. Taifa zima linafurahia matokeo haya.

limu 2 : Karibuni. Hata nasi tuna-furaha zisizo kifani. Wanafunzi hawa wametutunukia sifa mno.

ndishi 2 : Je, tunaweza kumhoji mwalimu mkuu?

limu 2 : Bila shaka. Mlango wa ofisi yake ni huo. Karibuni.

alimu 1 : Ndugu zanguni, mkutano wetu haujatibuka. Ungali upo. Mzima kama kigongo. Twenzetu au sivyo tutarajie wali mkavu.

: Kabla hawajatoka jukwaani. Mama na waandishi wa habari wanajitoma ndani.

na : Karibuni kwenye jungu kuu la Elimu.

andishi 1 : Asante Bi Mkurugenzi.

na : Hili ndilo jina lisikikalo kila pembe?

andishi 2 : Nini chanzo cha matokeo haya mufti?

na : Siri. Twaelewa fika siri za matokeo bora. Kwanza; uongozi bora. Pili; watunze vizuri walimu wako.... Yaliyobaki ni kupumguza siasa.

dishi 1 : Kweli ukiona vyaelea, vimeundwa. Nyuso za walimu wako zaonyesha waziwazi kwamba matamshi yako si umbea bali ni ukweli mtupu.

: Hata hivyo. Usimwambie mtu.

dishi 1 : Shukrani Bi. Mkurugenzi. Jalali katupa masikio mawili.

: Waandishi wanatoka. Mama anabaki jukwaani na walimu wake. Wanatarajia uhondo fulani.

: Walimu!

nu : (*Kwa furaha kama hapa awali*) Labeka Bi Mkurugnzi.

: (*Kwa hasira*) Hebu nipate maelezo tosha kuhusu tukio ambalo limejiri hapa sasa hivi.

: (*Wote wanashangaa*). Ni nani aliyewaruhusu waandishi kumhoji mwalimu mkuu ilhali mlijua vema kwamba mimi mkurugenzi nipo? Ama hamkukiona kitambulisho changu hapo uani? Gari langu aina ya Prado hamkuliona? (*Kimya*) Swali hili lahitaji jibu.
Tena mara moja. (*Walimu wanainua mikona kumjibu*)

a : (*Akichagua wa kujibu*) Aah!

imu : Lakini Bi mkurugenzi!

a : Lakini zako hazinilishi wala kunipa mavazi au marashi. Naelewa kwamba wengine wenu hawaupendi uso wangu. Hata hivyo, lau uko hapa lazima ushirikiane nami kwa kuwa mwenyezi Mungu aliniumba nikaumbika. Mwaelewa?

limu 2 : Ndiyo Bi mkurugenzi.

a : Basi mbona mwanikodolea macho kama kwamba mimi ni mkate wa boflo?.... Hata nashangaa kuona eti wengine wenu hapa nao ni walimu wa Jungu hili kuu la Elimu.

limu 1 : Pole Bi Mkurugenzi. Sikujua jambo hili lingekuudhi hivi.

limu 2 : Twaomba msamaha Bi Mkurugenzi. Tumekiri kosa letu.

na : Pole zenu hazitoshi. Hivi mimi sijalazwa hospitalini. Pole na maua wapelekeeni wagonjwa. Eleweni kwamba hapa kuna mtindo mfululizo wa

kazi na wasioamini, shule hii waione mapaa. Lango li wazi. Tena wazi kabisa.

*(waandishi wanarejea. Mkurugenzi anaonyesha kushangaa)*

dishi 1 : Samahani. Tungependa kumhoji mwalimu wa Kiingereza tafadhali.

imu 1 : Nipo. Msaada mtaupata.

dishi 2 : Tueleze mbinu uzitumiazo ili kupokea matokeo haya kabambe.

: Kwa kweli, wa kusifiwa ni mimi Mkurugenzi. Mbinu hizi mimi huzizoa toka Afrika kusini.

dishi 1 : Asante bibie. (Kwa mwalimu 1). Tupe uhondo.

imu 1 : Nidhamu na juhudi. Hayo maneno mawili ndiyo msingi wa matokeo.

dishi 2 : Asanteni. Basi tungependa kusheheneza magazeti yetu kwa picha zenu murua. Twende kazi.
(Wanajipanga kupiga picha) shukrani.

nu : Burudani.

a : Mwalimu, ulimaanisha nini kwa kusema kuwa nidhamu na juhudi ndizo msingi wa matokeo. Wewe hasa nidhamu gani unayo? Juhudi zipi ulizodhihirisha? (Kimya) Haya basi kwa kuwa hamwezi kunijibu kila mmoja atapata mshahara wake kasoro shilingi mia tano.

*(Mwalimu mkuu anaonyesha kumbembeleza mwalimu 1.)*

limu mkuu : Poa bwana. Biashara haigombi.

: Mimi hata sikuwa na manuio ya kumwudhi mama.

u : Usitie shaka. Nitazungumza naye.
(Mkurugenzi anamwita mwalimu mkuu)

a : Bwana hedimasta! Huyu kweli ni mmoja wetu?

u : Naam Bi Mkurugenzi.

a : Nani alimhoji?

: Mimi na wewe, lakini naona amekuwa kigeugeu kama kinyonga. Mtukutu kushinda…. Hata sijui nisemeje.
Naona *tumpige kalamu.*

: Acha pupa. Mla kwa pupa hadiriki kula tamu.
Niletee orodha zote nilizokuagiza. Wazazi watafika hapa mara tu.

(*Wanafunzi wanafanya mazoezi ya uigizaji. Wanaonyesha furaha teletele. Anaingia mwalimu wao. Mwalimu 1.)*

mu 1 : Basi tuendelee.

afunzi : Nani yule aliyekuita

mu 1 : Aliyefanya nini?

afunzi : Aliyekushurutisha kutukatizia mchezo (*wanacheka*) Baradhuli.

mu 1 : Unamwita mwalimu mkuu baradhuli?

afunzi : Hatukujua kuwa mhusika ni Mwalimu Mkuu.

: Yeye ndiye aliyekushurutisha siyo?

: Mwaelewa nyema kwamba naelewa kuwa mwaelewa kwamba naelewa yale mnayoyanuia kuyasema.
Haya twende kazi (*wanafunzi wanajipanga kuendelea na uigizaji).*

*(Mwalimu anakatiza mara na kuwaeleza mfululizo bora wa matukio)*

limu mkuu : Mwalimu, nipe daftari yako ya ratiba ya mafunzo. Mkurugenzi angetaka kuiona.

limu 1 : Haya, sawa nitakuletea afisini.

u : Anaihitaji sasa hivi

alimu 1 : Lakini waona nikitekeleza jukumu bwana Hedimasta.

u : Maneno mengi hayatakusaidia. Usijitie ukasuku.
Je, sarakasi na masomo ipi bora zaidi?

mu 1 : (*Amekasirika*) Haya wanafunzi, fumukaneni.

: Na ueleze ni kwa nini umewatawanyisha waigizaji kabla ya wakati unaofaa.

mu 1 : Bwana Hedimasta!

: Ratiba ya masomo. Tosha.
(*Mwalimu anaketi chini na kuwaza*)

mu 1 : Kisirani gani hiki? Watu hawa wameyasahau niliyowatekelezea mwaka jana.

*(Akikumbuka sherehe za mwaka jana baada ya kushinda katika mashindano ya uigizaji)*

mu 1 : (*Akisimama*) Ratiba ya masomo. Tosha. Wengi wape halafu.

*(Anatoka huku muziki wa kutoa hisia za huzuni ukicheza. Bibiye mwalimu anaonekana jukwaani-nyumbani – hana furaha.*

: (*Akiingia Mwalimu 1*) Watarajia tuishi vipi?

mu 1 : Vipi bibie, hunipi hata chembe cha furaha?

: Furaha! Furaha! Wanihadaa na kunicheza shere kisha watarajia furaha. Unaniona mjinga? Hee! Umenifanya juha?
(*Akimshika mashati*)

imu 1 : Wana Adamu na Hawa, sasa mwajionea wenyewe kwamba mume hana budi kumtwanga mke kama mahindi?

: Na mke ana jukumu la kuktia mme adabu.

limu 1 : Nani wa kumfunza mwenzake?

: Mimi?

limu 1 : (*Akistaajabu*) Nani?

: Haya basi tuzingatie uajibikaji na uwazi. Darahima zile, pesa zile ulizopewa kama tuzo miezi mitano iliyopita ziko wapi? Je, umenunua hata angalau kijiko kimoja cha shilingi tano hapa nyumbani?

mu 1 : Sasa wewe nani? Who are you? What are you?

: Mimi ni mkeo na hunitishi. You cant bwogo me.

mu 1 : (*Anampachika kofi. Anatoka*).

*(Anamwacha mke akilia. Mwanafunzi mmoja anaingia)*

afunzi : Shikamoo mama! (*Analia zaidi*) Nikuitie mkunga mama?

: (*Anamtambua*) Oh! Pole. Sikutarajia utafika.
Nilikuwa nikijaribu kuigiza mchezo ambao mwalimu wenu anapanga kuwafunza.

afunzi : Sawa.

: Mbona ukapapia kumwita mkunga?

afunzi : Wajua, mara yangu ya kwanza kumwona mtu mzima akitoa machozi ni wakati mama alikuwa mja mzito tayari kupata mwana.

: Alizaa nyumbani, ukimtizama?

nafunzi : La, hospitalini nami nilikuwepo.

: Ulikubaliwa kuingia, ushenzi mkubwa.

nafunzi : Basi daktari wote ni washenzi.

: Mbona?

nafunzi : Wao huwakubalia wanaozaliwa kuwaona wazazi wao wakati huo mgumu. Haya basi. La haja ni kwamba kuna mzazi aliyetaka kujadiliana na mwalimu kuhusu mambo fulani. Ahsante.

: Ahsante (*Bashasha zinadidimia, anahuzunika tena*). Mmh! Majambo hayo. Mzazi yupi anayetaka kumwona na kwa nini? Nimechoka kufanywa gunia la wanamasumbwi.

alimu 1 : (*Akiita*) Embe langu!

e : (*Akilia*) Wooih!

mu 1 : Ua langu la wa….

: (*Akilia kwa sauti*) Wooiah!

mu 1 : Kuna nini penzi langu?

: Naona shetani akikuelekeza.

mu 1 : Shetani au Yesu? Umepagawa?

: Labda wewe!

mu 1 : Mwanamke wee!

: Wajiandaa kunipiga naona.

imu 1 : La, kukunyorosha ulainike.

: Mbona mabadiliko haya nionayo? Ulikunywa nini, ulivuta nini?

imu 1 : Uliza swali moja kasha jingine. Sitaki mkururo wa maswali.

: Ulikunywani?

limu 1 : Swali mufti. La pili?

: Ulifyonza matingasi na mbagara?

limu 1 : Umeliuliza vizuri, hata zaidi.

: Yule Mzazi aliyetaka kukuona labda amenyambua kichwa chako.

limu 1 : Mzazi yupi? Lini/ wapi?

: Swali mufti, la pili?

alimu 1 : Mzazi yupi?

: : Umeliuliza vizuri hata zaidi.

alimu 1 : Aliyekueleza kwamba mzazi alitaka kuniona ni nani?

: Swali zuri hata zaidi.

mu 1 : Mwanamke wewe. Yafaa ufahamu kwamba nina uwezo wa kufanya sura yako iwe kama ramani ya Afrika.

: Anabaki jukwaani akipakia mizigo.

*(maigizo mawili yakitendeka sambamba. Jukwaa la chini, mwalimu na mzazi).*

mu 1 : Oh! Baba Dennis hujambo.

: Siku nyingi bwana hatujaonana. Vipi?

imu 1 : Safi kabisa.

i : Mwanangu Dennis?

imu 1 : Dennis yu salama salimini. Alifaulu mtihani wa kutathmini kwa alama za juu. Labda hisabati. Hesabu imemlemea kidogo.

i : Aah! Usijali. Hata mimi Hesabu ilinigusa kisogo tu.

mu 1 : Eeh! Usiseme hayo Dennis. Lazima tumhimize kufanya kazi na kusoma kwa bidii. (*Huku mke akiendelea*).

: (*Akijizingumzia*) Umuhimu wa kivuli huonekana mti ukatwapo. Hapa sipo tena. Mimi si jukwaa la kuigizia sarakasi. Wala mimi si kijana wa kidato cha kwanza wa kuonekana tu wala si kusikizwa.

*(Jukwaa la nchini)*

zi : Asante kwa mawaidha maridhawa. Natumai tutawasiliana kila mara ili tuweze kukifinyanga hicho chungu changu.

alimu 1 : Usiwe na wasiwasi kumhusu Dennis.

zi : Laini yako ni "Kencell" au "Safaricom"

alimu 1 : Kusema kweli …. Sijapata uwezo wa kuwa na…..

zi : Unamaanisha ….. mteja hapatikani kwa sasa?
Basi usitie shaka. Chukua dude hili ili tuweze kuwasiliana mara kwa mara.

nu 1 : Shukrani. Mola ajaze palipotoka dude hili.

: Tutawasiliana wakati wowote kuanzia sasa.
Kwaheri.

(*Mzazi anatoka. Jukwaa la juu. Mke anakunja virago vyake*).

nu 1 : (*Kwa furaha*) Kipenzi changu!

: (*Kwa hasira, akirudia*) Kipenzi changu!

mu 1 : Kipenzi! Wewe ndiwe pumzi yangu. Bila wewe najihisi mfu. Bila wewe mtima wangu utakoma kudunda. Wewe kwangu ni kama emembe dodo.

: (*Akitabasamu*) Unafurahisha wakati mwingine. Maneno yako hata yaweza kuwatoa nyoka mapangoni. Wanifanya kusahau ulivyoniezeka kofi sekunde kadhaa zilizopita. Hata hivyo, niwe embe dodo au sukari nguru.. mnimefanya uamuzi wangu.

: *(Mlio wa simu unasikika. Mwalimu 1, anakumbuka dude lake, mke anaonyesha kushangaa.)*

imu 1 : Hallo Baba Dennis!…. Sawa! Sawa! Haya.

: Ala!….. Umenunua simu tamba.

imu 1 : Simu ninayo bibi.

: Waonyesha kuendelea sana siku hizi.

limu 1 : Ahsante mke wangu.

: Lakini hivyo si vishawishi. La, nimeamua, uwazi tuna uajibikaji ndiyo maneno halisi (*Akitoweka*)

limu 1 : Usinifume mkuki moyoni mke wewe. Nifariji nipate kuhisi kama waume wengine.

: La! Tutalakiane huku tunapendana.
Mimi sina kinyongo.

alimu 1 : *(Mke anatoweka. Ameghadhabika)*

Bibiye! Mbona.... (*Mbwa wa mwalimu anabweka. Amembeba sungura mdomoni*)
Maajabu gani haya! Ulimpata wapi huyu sungura? Umemwua sungura? Mali ya shule! Mimi basi nachungulia kufutwa kazi. Lazima nimwoshe sungura huyu, nimkaushe manyoya na kumrejesha maskani mwake.

*(Mwalimu mkuu na mkurugenzi wanazungumsa wakiingia).*

: Umeandika barua ya kumfuta kazi.

: Tayari ....(*akisoma*) umeipa kalamu kwa sababu ya kutoelewa kazi yako, uvivu na uchochezi.

a : Utaelezaji mashtaka hayo matatu?

: Rahisi (1) Kutoelewa kazi - Kumwacha mbwa huru kufanya chochote akitakao
(2) Uchochezi - Kuitisha shilingi elfu hamsini ulizoahidiwa.
(3) Uvivu - Kuwaachilia manafunzi waigizaji wafumukane kabla ya muda rasmi.

a : Shabashi. Nitazungumza naye Jumatatu. Tumpe muda wa kusali na kumba rehema za Rabuka siku ya Jumapili. (*Mkurugenzi anatoka. Mwalimu mkuu anaigiza anavyokadiria kuwa mambo yatakuwa*).

u : Mwalimu (*akiigiza kama mwalimu 1*) Labeka Mwalimu Mkuu... pokea tuzo lako azizi...... sipendi bahasha kama hizi. Au labda ni habari za tanzia?.... mja huvuna akipandacho, basi shika mavuno yako.... Akijifanya kusoma barua ya kufutwa kazi. Umeipwa kalamu kwa uchochezi, kutoelewa kazi na uvivu.... (*Anajidai kuzirai, anaingia bibiye mwalimu wa kwanza*)

: Bwana Hedimasta!

u : Dada!

: U mgonjwa?

u : La niko salama tu. Furaha ndizo tele.

: Kuna habari motomoto eeh!

u : Kweli kabisa. Mimi ni mmoja wa wale watakaozuru nchi ya Afrika Kusini

mwaka huu na….

: Aah! Ukidhani sielewi chanzo cha furaha yako. Niliwapata vizuri sana wewe na mkurugenzi. Naelewa kuwa unasherehekea kufutwa kazi kwa bwanangu.

: Dada. Usigeuze kijiti cha kiberiti kuonekana bomu. Nitakupokeza kadhongo ili siri iwe ni ya wawili tu.

: Fanya wangu wangu au nimpashe habari mara moja.

: (*Akiimba*) Tausi ndege wangu, ndege wangu wa fahari, nitakupa utakacho……..

: Unanipa pesa ngapi? Au nizushe zogo!

: Shika basi (*Anampokeza shilingi mia tano mkononi*)

: Shilingi mia tano. Unaniona maaluni, kinyangarika. Utolinganisha kazi ya bwanangu na shilingi mia tano? Unacheza wewe!

ı : Ewe! Usibadilishe mambo hata nimekana kwamba ndimi ninayemfuta mumeo kazi.

: Haya basi toa kitu kikubwa.

ı : (*Akitoa shilingi elfu mbili*) Haya dada. Misichotaka ni mnong'ono kwamba ndimi ninayemfuta kazi mumeo.

: La upenuni halisemwi nje. Yeyote akipata habari hizi basi ni wewe wakushtakiwa.

u : Alhamdulilahi!

(*Mwalimu wa 1 akiwaza nyumbani kwake*)

alimu 1 : Ole wangu! Hivi ndivyo makapera huishi?

: (Akiingia) Hivi basi ndivyo wauaji katili wa sungura wa shule huwa.

alimu 1 : Mke wangu (*kwa furaha*) umerudi! Yesu apewe sifa.

e : Wa kupewa sifa si wengine bali ni Mwalimu Mkuu na bi. Mkurugenzi.

mu 1 : Keani.

: Maadam ni wao walionipelekea kuwa hapa.

mu 1 : Una maana gani wewe, umepagawa?

: Gazeti la leo umelitia macho?

mu 1 : Naam, kwani?

: Nyota yako, uliisoma? (*akirushiwa gazeti*)

mu 1 : Naam. Ilikuwa hivi.... *(akisoma)* tarajia viroja wiki ijayo. Rangi yako ni nyekundu. Natarajia mema kwa kuwa Mungu si Athumani. Haamtupi mja wake.

: Chungusa ili nawe usimtupe Mungu wako.

imu 1 : Kwani una fununu ya viroja hivi? Haya basi karibu nyumbani lakini.

: Hata hivyo kumbuka kuwa sijayasahau yale ya awali. Hivyo nipumbaze ili niweze kusahau.

imu 1 : (*Akichukua gita*) Kwa kucheza gita siyo?
*Mwalimu anaimba wimbo wa kimapenzi kwa gita kasha kwa kubonyeza piano*

: (*Anacheza. Kisha...*) Wanikumbusha enzi zangu. Wakati nyimbo za reggea zilishamiri anga za muziki.

limu 1 : Nieleze yaliyo kifuani mama. Yabwage niyasikie.

: Hamna chochote ila chuchu tu. (*Kwa watazamaji*)
Nitamwelezea vipi kwamba kesho atapigwa kalamu?

alimu 1 : Wajua niliota ndoto. Kuwa nimepandishwa cheo.
Nimeongezewa madaraka.

: Ati umeongezewa ma.... Nini?

alimu 1 : Madaraka. (*Saa yaonyesha asubuhi. Jogoo anawika*) Lo' ni Jumataatu. Leo nitafunza mithili ya Yesu Kristo. Maana hakuna aliyeweza kufunza kama

yeye.

: Hata hivyo, tarajia kupigwa na butwaa.

mu 1 : Usiseme hata hivyo… sema kwa hivyo. Matarajio haya si kwa ubaya ila uzuri tu.

: Hata baada ya kumwua sungura wa shule?

mu 1 : Kama hiyo ni kesi basi mimi ningalihukumiwa kifo kwa sasa. Wajua mii nimewahi kuua?
Nilikuwa na umri wa nini tisa?

: Miaka tisa?

imu 1 : La, miezi tisa

: Usilete mzaha.

imu 1 : Mzaha upi!

: Ulimwua nani?

limu 1 : Dudu manyoya. Tena mkubwa ajabu.

: Mmh! Si binadamu?

limu 1 : Kwa kweli…. Nilimwua binadamu hata awali zaidi; katika dakika zangu za mwanzo humu duniani.

: Elewa kwamba mimi sicheki na watu.

limu 1 : Kweli hatucheki na watu. Nilimwua mamangu pucde tu nilipozaliwa…. Nilipozaliwa tu paap! Mama naye akaenda nyweeeh!

: Haya basi. Tega sikio, usikimbilie kwenda shuleni.

alimu 1 : Nimechelewa tayari mke wewe. Ni saa mbili za asubuhi. (*Anaingia Mwalimu Mkuu*)

u : Hujambo mwalimu!

alimu 1 : Sijambo.

: (*Kwa uoga*) Wakati ndio huu umewadia (kwa Mwalimu Mkuu).
Bwana Hedimasta, tafadhali tumia lugha ya tasifida.
Usitupashe habari kiholela.

mu 1 : Papara za nini? Hata chiriku hunyamaza.
Bwana Hedimasta, kuna lipi la haja?
Naelewa kuwa nimechelewa kufika kazini, hata hivyo nilikuwa nikitatua shida fulani humu nyumbani.

: Hata nami nilishangazwa. Bi. Mkurugenzi angetaka kujadiliana nawe kwa faragha. Ahsante. (*Anatoka*).

: Hayo basi ndiyo mambo. Kilichonifanya kurudi ni hicho. Nilipata kuwasikia wakisema kuwa utapigwa kalamu ifikapo Jumatatu. Ilinilazimu kurudi kwa kuwa nilielewa kwamba hatuna budi kugura nyumba hii.

: (*Anamshika bibi*) Wewe, umekuwa chizi. Mimi natumainia kuongezwa madaraka huku wewe waona kwamba nitafutwa kazi?

: Niamini. Nilisikiliza maongezi yao.

imu 1 : Nianzie wapi? Niende au nidinde?

: Uende kusomewa? Mbona tusifanye halahala twende zetu? Kunja virago.

imu 1 : Hapana. Mimi ni mwanamme. Acha nikamwone huyo afiriti.

: Nianze kukunja virago.

limu 1 : Huna la ziada.

*(Mwalimu 1 anaenda kwake Mkurugenzi. Mwalimu mkuu ananyemelea na kurudi)*

u : Dada, natumai mwalimu ameelekea kumwona Bi mkurugenzi!

: Nawe kazi yako ni nini hapa? Watakani?

u : Eeh! Unamfokea nani hivyo?

: Utamwamini vipi mwanamme akutembeleaye atokapo tu mumeo?

: Hasa ikiwa aliwahi kukupatia kitu kidogo!

: Pesa zako bado nimezihifadhi kama ithibati.

: Utathibitisha vipi kwamba ni hizo pesa nilizokupa wewe?

: Kwa bahati nzuri. Ulikuwa umeshika wino na alama za vidole vyako ingaliko.

: Sadfa gani hiyo. Nirejeshee pesa zangu.

: (*Akitembea kwa madaha*) Aaha!

: Mwanamke weeh! Ungalifahamu kwamba mimi ni Hedimasta!

: Shuleni si nyumbani kwangu.

: Tazama huyu msichana.

: Waniita msichana?

: Kwani wewe nani? (*Mke akitembea kwa madaha*)

: Mke wa mwalimu.

: Wake wa waalimu hujulikana kwa vilemba. Wewe ni kijisichana tu.

: Mimi! Mimi ni mwanadada tosha.

: Mwanadada kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ni kiumbe kilichoumbwa kama malaika.

: Na Hedimasta ni mwanamme anayegonga milango ya wengine mabwana zao wakishaondoka.

(*Mlango unabishwa*)

: Ingia' mlango uko wazi.

...nafunzi : Bibie. Tumeliokota shati hili.
(*Shati ni la Mwalimu 1 na limelowa damu chepechepe*)

: Wapi?

: Lini?

: Vipi?

afunzi : Tulikuwa tukicheza njiani na kwa bahati nzuri, la, bahati mbaya tukapata shati hili. (*Wanakimbilia kulikotokea kisa hicho*)
*Anaingia mwenye pikipiki. Wanafunzi na walimu wako mbele ya afisi ya mkurugenzi. Wanajadiliana.*

imu 2 : Nilijua hatimaye itakuwa vivi hivi.

funzi : Kuna nini?

imu 2 : Mwalimu wenu wa sarakasi... hata hatujui....

funzi : Ameuawa?

imu 2 : Hatuna uhakika.
(*Anaingia Mwalimu Mkuu, mkewe mwalimu 1 na mwanafunzi*)

: Nina wasiwasi. Dukuduku zimenitanda.

funzi : Tweleze. Tweleze kilichojiri bwana Hedimasta.

: Wewe ndiwe mwasisi wa haya yote.

nyepikipiki : Nimetumwa (*wote wananyamaa*)

: Eti.

iki : Eti mgonjwa aliyeletwa hospitalini amepiga dunia teke.

(*Muziki wa tanzia unasikika*)

afunzi Bwana Hedimasta, yote haya ni juu yako.

u Vipi tena?

afunzi Wewe ndiwe uliyekuwa kihunzi kwa mwalimu wetu.

Ukamtimua kazini.

Hakufutwa kazi. Aliyenena hayo ni nani?

nu 2 Alikuwa afutwe kazi lakini kwa sababu mwalimu mwingine alileta barua ya kutaka kuacha kazi akaponea chupuchupu. (Wote wanashangaa)

funzi 2 Hata ulimtuhumu kwa kumwua sungura.

Mbwa wake alimwua sungura.

funzi 2 Mimi ndiye huchunga sungura hao. Huyu sungura alikufa kwa sababu ya kukosa pumzi. Hapo nilimzika shimoni. Mbwa wa mwalimu alimfukua tu kutoka shimoni.

Kweli! Mbona hukutueleza awali.

funzi 2 Nilimwogopa Mwalimu Mkuu. (*Kwa mwalimu mkuu*)
Nitakushtaki! Mimi nitakushtaki! Nilimweleza Mwalimu Mkuu haya yote lakini akaniambia nifyate ulimi wangu.

Hata mini alinipa shilingi elfu mbili ili nisiseme kuwa yeye ndiye aliyezindua mbinu ya kumfuta kazi mme wangu.

Muue! Muue! Mrushe mbugani.

*(Mkurugenzi anafika katika gari lake. Wananyamaza)*

Yepi yanayotendeka hapa?

Hedimasta lazima afe kwa udhalimu wake.
Ametukandamiza vya kutosha.

Kumwua Mwalimu Mkuu hakutoleta manufaa yoyote.

Mabadiliko! Mabadiliko!

Sikizeni. Nilielezwa haya yote. Hata kabla ya kifo cha mwalimu nilikuwa nimeamua kumshusha cheo Mwalimu Mkuu na mahala pake nikamweka…

Mwalimu wa sarakasi?

Najua unasema hayo kwa sababu bwanangu ame…. *(analia)*

(*Akitoa barua*) Soma barua hii.

mu 2 Umepandishwa cheo kuwa kiongozi wa Jungu Kuu la Elimu baada ya utafiti na majadiliano kabambe.

Na kwa kuwa hayupo……..

unzi Tumrushe Hedimasta mbugani. (*Wanamshika juujuu. Anaingia mwenye pikipiki. Amembeba mwalimu wa 1. wote wanashangaa*)

mu 2 (*Kwa mshangao*) Ulisema amefariki.

ki La, alinituma kuwaeleza kwamba mgonjwa ameaga dunia.

Mgonjwa yupi?

imu 1 Tusker! Mbwa wangu.

Tusker?

imu 1 Ndio mbwa wangu aligongwa na gari nilipokuwa nikielekea kwake Bi. Mkurugenzi. (*Mkewe anakimbia kumkumbatia*)

Na shati lako?

imu 1 Nililivua ili kumfungia Tusker majeraha yake. Haya nielezeni. Mkutano huu ni wa nini?
Kufutwa kwangu kazini?

a Hata. Mkutano ni wa kukupa madaraka. Wewe ndiwe kiongozi katika Jungu Kuu la Elimu. Hii barua. Chukua! Chukua! *(Mwalimu anasita kuchukua barua)*

e Pokea barua! Pokea barua!
(*Anapokea barua*)

a Umepata cheo. Wewe ndiwe Mwalimu Mkuu.

e Mwalimu wa sarakazi. Mwalimu wa sarakazi ndiye mwalimu mkuu wa Jungu la Elimu. **NA HILO NDILO TUZO AZIZI**

*** MWISHO ***

Kiambatisho 3b

[redacted]

# MAJUTO

## MUHTASARI

NI TAMTHILIA INAYOZUNGUMZIA JINSI NDULI UKIMWI ULIVYOTANDA NA KUDHIISHA JAMII BILA YA KUJALI INSAAFU, CHEO WALA JINSIA

## WAHUSIKA

| | |
|---|---|
| MAJUTO: | SHULIN CHUBA |
| BABA MAJUTO: | MOFFAT MABULA NZING'U |
| MAMA MAJUTO: | FATUMA ALI |
| KATIBU: | KATHLEEN NYABOLA |
| DOLA: | JACKLINE WANGARI |
| BABA DOLA | JOY FURAHA KIWANGO |
| MAMA DOLA: | SHARIFA ISLAM |
| SHAMU: | AGNES MAINA CHEGE |
| KAHINDI: | WAITHERA KIHIU |
| CHIMERA: | NANCY CHITTI |
| SHIFTA I | MOHAMMED HAMISI |
| SHIFTA II | MUTUNGA MASILA |
| MWANDISHI: | KHAMIS JOHNSON KANGANJI |
| WATAYARISHI: | KHAMIS JOHNSON KANGANJI, ATHUMAN MOHAMED AMANI. |

# ONYESHO LA KWANZA

(JUKWAANI ANAONEKANA MAJUTO AMEKAA AKIHUZUNIKA. RAFIKI YAKE, SHAMU AMBAYE NI KILEMA ANAMFARIJI)

SHAMU: Rafiki yangu majuto, sahau ni dawa ya waja. Yaliyopita si ndwele, tugange yaliyopo na yajayo. Puuza yaliyopita, turudi shule majuto.

MAJUTO: Shamu…la !

SHAMU: Majuto, fahamu yakuwa ujao ni mtihani wa mwisho wa masomo ya msingi. Sasa utaendelea kuishi hivi na majonzi mpaka lini?

MAJUTO: Milele na milele, aaamin !

SHAMU: Wakati majuto na fedha yote iliyopotea kwa miaka minane. Si haki hivyo ufanyavyo.

MAJUTO: Shamu…mimi niacha, naogopa

SHAMUU Usiogope

MAJUTO: Nakuchelea wewe heshima yako, maisha yako yasije yakaharibika kama yangu.

SHAMU: Najua wayathamini sana maisha yangu lakini utaendelea kuishi katika hili dimbwi la upweke mpaka lini? Turudi shule Majuto.

MAJUTO: La ! Haiwezekani

SHAMU: Jaribu

MAJUTO: Siwezi

SHAMU: Jikaze

MAJUTO: La ! laa! Laaa ! siwezi. Je .. Je Watu watasema nini kuhusu hali yangu hii. Fedheha tupu.

SHAMU: Si fedheha, ni hali yakilimwengu na ushujaa

MAJUTO: Sitaki ! Nimesema sitaki kabisaa !

SHAMU: Yaani ndiyo umeamua kugeuka siyo. Situlielewana kuwa utarudi shule licha ya majanga yote yaliyotokea (kimya) Majuto sinaongea na wewe !

MAJUTO: Shamu ! (kwa ghadhabu) usiibughudhi akili yangu. Yanayonisibu ni makubwa. Madhila yaliyonifuma mazito, siwezi kuyahimili….Shamu usinichukulie vibaya.. wewe bado ni rafiki yangu, lakini…ni heri tuachane (anapiga hatu kadhaa, mbali na Shamu).

SHAMU: Mimi bado nakupenda urafiki wangu kwako uko ngazi ya juu moyoni mwangu…Mbona wanifanya hivi?

MAJUTO: Hebu jaribu kunielewa kuwa mbali nawe ni mahaba makubwa kwako.

SHAMU: Hapo bado hujaniambiakitu. Mimi si duko. Usinimulike kurunzi ilhali kuna muangaza. (kwa ukali) wacha kunitia huku ukinitoa kule.. nipasulie mbarika.. kwanini ..kwanini ghafla bin-vu waghairi usuhuba wetu ..ehh! ..Ama umeshapata asiye kilema?

MAJUTO: Mimi sijapata, bali nimepatwa…Nimeangukiwa na mlelema, na hivi sasa siwezi hata kuhema.

SHAMU: (Kwa uchungu na huzuni tele) Sawa..sawa tu.. Nimeshakuelewa. (anapiga hatua kuelekea upande wa kulia wa jukwaa)…Shamu..Shamu binti Amu…huna chako tena…. Ulidhani umepata tende kumbe umepata mende…Hupendwi !…Hupendwi kwa vile wewe ni kilema.

MAJUTO: Heri wewe kilema, mimi hivi unionavyo ni zaidi ya kiselema..(akimfariji)

SHAMU: (Kwa hasira) Usinishike !

MAJUTO: Najua uamuzi wangu umekuudhi, lakini yafaa unishukuru.

SHAMU: Afadhali nitoe shukurani zangu kwa mbwa koko kuliko wewe paka shume ! (kilio cha kwikwi). Kwanini umekuwa ukinihadaa wakati huu wote. Kwanini?...Kwanini hukunipa kanuni yako toka awali?

MAJUTO: Kanuni ya sasa na awali, zote zina sahali Mpensi usilie. Ukilia waniliza. Shamu yanayonizonga ni mazito, Madhila yanayonifadhaisha, nilikuwa nimeyapiga fundo, lakini sina budi kukufungulia. Dunia... Dunia si tambarare....Tanabahi.. ukweli... ukweli uko katika fundo. Fundo limefunga fumbo (Anafungua kamba alioishika mikononi) Tazama ! Tazama nilivyozama...

SHAMU: (Kapigwa na butwaa)..Ma...Ju...To...!

MAJUTO: (Akiondoka) Kuanzia sasa usiniite tena Majuto. Niite hayati Majuto aliye hai ! sina la ziada. Kwaheri.

SHAMU: (Akimfuata) Majuto...Majuto nisikize..Majuto nisubiri, Majuto...Majuto...(Anamuandama)

## ONYESHO LA PILI

(NYUMBANI KWA BABA MAJUTO. ANATOKA NJE AKIWA NA HAMAKI TELE MKEWE ANAMUANDAMA)

BABA MAJUTO: Sitaki... Nimesema hakuna lengine la kufanya.

MAMA MAJUTO: Tafadhali mume wangu hebu jaribu kubadili huo uamuzi wako

BABA MAJUTO: Sikiliza mama Majuto, kikosa mwaka na ruza, silimi vuli kachekwa.

MAMA MAJUTO: Lakini si ungemsamehe tu...

BABA MAJUTO: (anamkatiza) Mwanamke ! Mbona umekwenda chagagana ngangandu asemehewe. Inaonekana unafurahia yaliyomfika Majuto sio.

MAMA MAJUTO: (kwa upole) Mume wangu, yafaa ufahamu ya kuwa mwana wetu tu anaugua, na si yeye aliyependa iwe hivyo.

BABA MAJUTO: Samli ya Pemba haimpati mtu macho, huo ni mwiba wa kujichoma kila mwenda mbizi nchi kavu huchunuwa usowe.

MAMA MAJUTO: Yataka ufahamu haya yote ni majaaliwa.

BABA MAJUTO: Haya si majaaliwa huku ni kulaaniwa.

MAMA MAJUTO: Mume wangu hebu punguza hamaki. Jaribu kufikiria uamuzi wako kwa mara ya pili.

BABA MAJUTO (Kwa bezo) Mara ya kwanza nilifikiria nikaamua siwezi.. mara ya pili nasema siwezi kabisa.

MAMA MAJUTO: Lakini Majuto ni mwanao !

BABA MAJUTO: (STIHIZAI) Kuanzia leo si mwanangu tena, nimekuuzia wewe. Utanilipa polepole, na ukishindwa, nitakusamehe !

MAMA MAJUTO: Hebu wacha kukufuru

BABA MAJUTO: Kwanza huyo Majuto yuko wapi? Majuto (Anaita) Majuto !

MAJUTO: Naam baba (akitokeza)

BABA MAJUTO: (Akimkejeli) Aaha.. Majuto mwanangu mzuri.. Mwanangu wa pekee. Uliyeniletea tuhuma na shahada maadal – basar..(Kwa

hasira) kafunganye kila kilicho chako na nyumba hii uione paa…Hizo shahada zako za ulanisi na usherati, katafute pa kuziweka.

MAMA MAJUTO: Baba Majuto !!!

BABA MAJUTO: Kimya!

MAJUTO: (Kwa unyenyekevu) Baba, najua nimekosa. Najuwa nimekuletea izara katika wizara yako. Yaliyonikumba ni aibu kubwa kwako kama waziri wa afya… lakini ewe babangu mzazi nisamehe.

MAMA MAJUTO: Baba Majuto, Mwana akinyelea paja halikatwi

BABA MAJUTO: Mimi sitolikata paja, nitaukata mguu mzima ili iwe funzo kwa watoto wengine wenye tabia chafu kama yake.

MAMA MAJUTO: Mume wangu jaribu kupima maji na unga.

BABA MAJUTO: Huwo unga kula wewe, mlafi mkubwa. (kwa Majuto) majuto nimesema niondokee machoni mwangu. Kila ninapozidi kuona hicho kijuso chako cha mbuzi nahisi kutapika. (Majuto anaingia ndani).

MAMA MAJUTO: Mume wangu sasa hivyo wajengaa..

BABA MAJUTO: (Anamkatiza) Nabomoa, navunja, navuruga kabisaaa!

MAMA MAJUTO: Lakini mbona hutaki kunisikiza?

BABA MAJUTO: Uamuzi wangu ni 'alpha' na 'omega.' 'I am the head of this house'.

MAMA MAJUTO: (Akasikitika) Watu wakisikia jambo hili hawataweza kuamini.

BABA MAJUTO: Muuuh… Nitakapotembea uchi ndiyo watu wataamini kuwa mimi ni mwanaume na nusu. Siwezi kukubali kuona hadhi na heshima yangu ikishushwa na kutiwa dosari na kitinyango cha binadamu kama huyu. (Majuto anatokeza).

MAJUTO: Baba hebu nisikize.. yaliyonipata ni kama ajali, na ajali haina kinga.

BABA MAJUTO: Nami na kufukuza nikijuwa hakuna wa kunipinga.

MAJUTO: Lakini sikufanya kwa makusudi.

BABA MAJUTO: Najua vyema huitwi sudi waitwa majuto, lakini hapa kwangu sitokidhia kujimbi kozi, toka!

MAJUTO: Kweli wewe ni babangu wa kunizaa!

BABA MAJUTO: Mimi ni babako wa kukufukuza, nimesema utoke, ningurumapo unyauke kisha, pheeww..u-ya-yu-ke!

MAJUTO: Baba nakusihi unis….

BABA MAJUTO: Wanipotezea wakati wangu

MAMA MAJUTO: Mbona umnyama jinsi hiyo, huna hata hisia za kibinadamu?

BABA MAJUTO: Sina hata za yule beberu aliyetiwa jandoni.

MAJUTO: Mimi ni mwanao usinitupe. Nakuomba… nakusihi…niko miguuni mwako.

MAMA MAJUTO: Nakupigia magoti.. mume wangu….mwandani wangu, muhisani wangu.. (baba Majuto anawaepuka polepole. Mama Majuto anasimama pole na kumuenua mwanawe) …Majuto mwanangu, lisilobudi hutendwa.

BABA MAJUTO: Nami sina budi kulitenda.

MAMA MAJUTO: Ni heri uende…nakuombea kila la heri

MAJUTO: Siwezi kuamini ..kama babangu…babangu mzazi aweza kunifukuza…Damu yake!

MAMA MAJUTO: (Akimsindikiza) Majuto mwanangu, twende.. twende nikusafirishe hadi tamati usiyoijuwa.

BABA MAJUTO: (Kwa ukali) Mama Majuto! Piga hatua moja tu zaidi, nawe nyumba hii utaiona paa.

MAMA MAJUTO: (Kwa kilio) Ah Baba Majuto mbona watu fanyia ukatili kiasi hichi (kwa Majuto) Majuto mwanangu…

MAJUTO: Mama…tafadhali niwache niende…wewe kaa na baba kwa utulivu. Sitaki kuwatenganisha baadaye nikawa nuksani kitatange.. na idumu ndo-a- ye- nu.

BABA MAJUTO: Nawe yadumu maradhi yako. Buriani Bon-viyajz .(polepole Majuto anatoka na mizigo yake. Mama anabaki machozi churu churu)

MAMA MAJUTO: Siwezi (kwa kilio) siwezi kuamini kama wewe …waweza kufanya kitendo cha kinyama kama hiki.

BABA MAJUTO: (akimfuatia) Basi utaamini siku ile nitakapotenda kitendo cha kibinadamu cha kukufukuza hata wewe!

MAMA MAJUTO: Yani wewe waweza kumfukuza mwanao hivi hivi..(kwa uchungu) Hata mshipa wa wasiwasi usikupige? Wewe ubinadamuu…u..?

BABA MAJUTO (anamkatisa) Ni kitu nusu…nguva!

MAAMA MAJUTO: Ama kweli, dunia imebadilika. Ulimwengu… ulimwengu umegeuka.

BABA MAJUTO: Haya na wewe geuka, ona njia ya ndani. Sitaki kusikia vilio hapa… matanga yamekwisha (mama anaingia ndani)

BABA MAJUTO: (Anajisemea akiwa pekee) Hebu jaribu kufikiria ehh. Kweli jambo hililaingia akilini? Waziri mzima wa Afya, aingiwe na doa, dosari. Jambo … jambo litakuwa limezua mambo. (Kitendo kifuatacho ni fikra kichwani mwa baba Majuto. Wauzaji majarida wanaonekana wakiuza majarida yasemayo:-
:Taifa Leo – Binti ya Waziri augua ukimwi.
:Daily Zefhe – Shame! Minister's Daughter has Aids.
(baba majuto anachanganyikiwa, anahangaika akijaribu kuwazima wasiuze. mara anazinduka kwa hamaki…)

BABA MAJUTO: 'Non-Sense!!!'
(Mara wafanyikazi wawili wanaingia mbio..)

WOTE: Naaaaam Baba! Umetuita ! (Lafudhi ya kishamba)

BABA MAJUTO: Nyinyi mwaitwa non-sence? (kimya) Nawauliza siku hizi mumesilimishwa mwaitwa non-sense?

CHIMERA: La baba! Mimi naitwa Chimera Jogolo

KAMINDI: Na mimi naitwa kahindi Jogolo

WOTE Na Bhemlaa !

BABA MAJUTO: Sasa ?

KAHINDI: Wajua mzee sisi hivi utuonavyo hatujapata mishahara yetu.

BABA MAJUTO: Kwani nyie hamjui njia ya msalani

KAHINDI: Siyo hivyo Mzee, ni mushihara

WOTE: Pesa zehu !

BABA MAJUTO: Nyinyi akili zenu ni timamu? ….(Akiwaandama) Nawauliza humu vichwani mwenu kuna akili au uji wa wimbi? Hamuoni hii zahma

niliyo nayo, kisha nyinyi mwaja (Akiwaiga) Babbah hatujjahpata mushihara wetu. Puuuzz…

KAHINDI: A ! Usitutusi Mzee, sisi bwana twakwambia wazi, usipotulipa mshihara wetu, tena wa miezi miwili…

WOTE: Hino kazi fundaigomea ! (Wanarudi ndani).

BABA MAJUTO: (Kwa ukali) Malizeni kazi kwanza kisha ndio mugome. Mabegube wakubwa, wasiojuwa tafauti mbingu, ardhi and sayari. Ngoja niwasikie eti wamegoma, watanitambua. (anaita) Mama Majuto, Mama Majuto!….

MAMA MAJUTO: Labeik.

BABA MAJUTO: Hebu nipatie koti langu

MAMA MAJUTO: Koti? !! yaani leo utavaa koti na kaunda suti.

BABA MAJUTO: (Anagutuka) A!! (Anatoka)

MAMA MAJUTO: (Akibakia pekee) Makubwa haya. (anaingia ndani)

## ONYESHO LA TATU

HAPA NI KATIKA OFISI KUU YA WAZARA YA AFYA. KATIBU MKUU ANAONEKANA AKIONGE KWA SIMU.

KATIBU: Yes…Yess.. Ndio. Hapa ni Afya House… Yaah, eti?…si nimekwambia hapa ni makao makuu ya wazara ya Afya..Waziri? Hajaingia bado…Mimi sitaki kujua saa ngapi, nimekwambia hajawazili! Mambo yake ya kinyumbani mimi siyajui, 'after all' sikuajiriwa kama jasusi. (mara waziri anawasili). Subiri ndiye huyo anaingia. (Kwa waziri) Boss…simu yako.

BABA MAJUTO: Simu yangu iko nyumbani

KATIBU: Kuna mtu anataka kuongea na wewe.

BABA MAJUTO: (Anasimama) ni nani?

KATIBU: Mwandishi wa habari

BABA MAJUTO: Anataka nini?

KATIBU: Nafikiri ni kuhusu mwanayo Majuto.

BABA MAJUTO: Mambo ya majuto, sitaki kuyasikia hapa ofisini mwangu.

KATIBU: Boss, hawa waandishi wa habari wamekuwa wakinisumbu toka asubuhi, kila wakati simu ni NGRRR NGREEEE. Licha ya hayo, jana usiku pia walikuwa hapa, tena inaonekana sio waandishi wa hapa pekee, hata wale wa nje.

BABA MAJUTO: Wawe wanje, ndani hata kuzimu, sitaongea nao, nimesema sitaki.

KATIBU: (Kashangaa) Lakini hivyo ufanyavyo sivyo.

BABA MAJUTO: Hebu nikabidhi hiyo simu. (Anaipokea) "Minister speaking…I have nothing to tell, nothing to discuss with you and nothing to comment on! Good day !!".

KATIBU: (Akizidi kushangaa) lakini hivyo ufanyavyo sibyo. Si sawa kabisa… Ni heri uongee nao ujue wana yapi ya kukuuliza kusudi uondoe dukuduku na tashwishi zilizoko kama hubna ukweli….

BABA MAJUTO: (Akikatiza ghafla) ukweli…? Ukweli gani? Hakuna ukweli wowote.

| | |
|---|---|
| KATIBU: | Wacha kuupa moyo wako faraja. Piga moyo konde, onana na hawa waandishi wa habari, uwaeleze kama mwanao anaugua uki... |
| BABA MAJUTO: | Tosha ! (kwa hamaki) ushauri wako umevuka mpaka. Habari za Majuto kuwa anaugua hazikuhusu ndewe wala sikio. Ikiwa tayari, umeshapulizwa sumu baridi na hao waandishi wa habari, basi juwa ya kuwa hapa umefika ukingoni...(Akimuandama, Guu-Bandika, Guu-Bandua). Wewe ni katibu ! "You are just a mere female permanent secretary in this office !!" |
| KATIBU: | (Kwa hamaki) wacha kuniripukia ! (Anapoa Ghafla) Aaah samahani... samahani sana Boss... lakini yataka ufahamu mimi ndiye nimayesumbuliwa na hao waandishi. Na ni wajibu wangu kukupa ushauri. |
| BABA MAJUTO: | Ushauri wa kikazi "madam P.S." Wakinyumbani 'No' sitaki kuona sura za hao mburukenge wanaojiita waandishi wa habari...Habari...Habari gani wanazoziandika na ni unafiki na uchochezi mtupu. |
| KATIBU: | (Akienua mabega) Upendavyo..lakini kaa ukijuwa, uji wa moto haupozwi kwa ucha ya ulimi, hata ujifiche wapi hawa mapaparazi watakupata, na siku hiyo, chete kitakuwa kimeingia nyoka. |
| BABA MAJUTO: | Nyoka ni porini, sio hapa ofisini...tena nataka ifahamike ya kuwa, sina mwana aitwaye Majuto. (katibu anashangaa) na wajibu wangu si baba Majuto, bali waziri wa afya. "Full Stop." (ANAONDOKA. KATIBU ANAMFUATA NYUMA NA MSHANGAO). |

## <u>ONYESHO LA NNE</u>

(ONYESHO LINAANZA NA NDOTO. MAMA ANAOTA NI MGENI WA HESHIMA NA ANAWAKABIDHI/ANAWATUZA WANAFUNZI SHAHADA ZAO, LAKINI MWANAWE MAJUTO ANAONEKA KABANWA NA KUTESWA NA MARADHI MPAKA ANASHINDWA KUPOKEA SHAHADA. MAMA ANAJARIBU KUMSAIDIA LAKINI WAPI).

| | |
|---|---|
| MAMA MAJUTO: | Majuto...Majuto...mwanangu... Majuto....(Anaita lakini majuto anapotea polepole). |
| BABA MAJUTO: | (Anaingia ghafla. Ndoto inakatika) Mama majuto... Mama Majuto! Usipochunga utapagawa. Wafanya nini hapa, waomba Mungu? |
| MAMA MAJUTO: | (Kwa ufidhuli) Naomba shetani ! |
| BABA MAJUTO: | Ei, mwanamke.. hasira zako za usingizi usiniletee mimi. |
| MAMA MAJUTO: | Mimi sina hasira, nina uchungu. Uchungu wa mwanangu... Kwanini...Kwanini ulimfukuza? |
| BABA MAJUTO: | Nilimfukuza kwa sababu alikuwa kiraka kibovu katika nguo mpya. |
| MAMA MAJUTO: | Wewe ni mzazi wa aina gani usiye na huruma na damu yako... ama kweli mwanaume, hajui uchungu wa uzazi ni nini. |
| BABA MAJUTO: | Mimi hata uchungu wa ukunga siufahamu. |

MAMA MAJUTO: Baba Majuto ! yaani umethamini cheo sana kuliko mwanao... Hakika wewe ni hayawani, ni mnyama kuliko mnyama mwenyewe.

BABA MAJUTO: Tosha ! Mwanamke, sitokubali unipande kichwani. Hapa ulipokika komelea papo hapo... Majuto alinivua nguo, akanibakisha hivi, were wataka kunivua nini?

MAMA MAJUTO: Mimi nitakuvua....

BABA MAJUTO: (Anamkatiza) ...U-skuti...kama sakatal jabal. (kimya) kama una huzuni sama na mwanaon njia hiyo mfuate.

MAMA MAJUTO: Mimi ni mamake mzazi...nitamfuata! Wewe kaa na cheo chako cha uwaziri wa afya, lakini fahamu ya kuwa Majuto...Majuto ni mjukuu.

BABA MAJUTO: Majuto si mjukuu, Majuto ni mwanangu. Naliweliwalo...(Mama Majuto anaingia ndani na kutoka huku kabeba mizigo yake) Mama Majuto...Mama Majuto...usiniambia watoka.

MAMA MAJUTO: Sitwakwambia...nakuonyesha...(anatoka).

BABA MAJUTO: Mama Majuto...(akimfuata) Mama Majuto... (Amebaki pekee)...Mashaka gani haya yanayoniandama...kazi yaenda mrama...familia nayo inazama...Aaaa! (anakurupuka kuelekea ndani

## ONYESHO LA TANO

HAPA NI MTAA FULANI KATIKA SHEHEMU FULANI KATIKA MKOA WAPWANI. MSICHANA MDOGO NA MAMAKE WANAZOZANA. MAMA ANAMCHAPA MWANAWE......

DOLA: (CHWA) Basi mama..... Basi mamaa... Sifanyi tena... sifanyi tena mama....

MAMA DOLA: (AKIPUMUA) Yaani wewe, mwana mdogo.. Mdogo.. Hata hujavunja ungo. Ushajua mambo ya ki-utu uzima (ANAMCHAPA)

DOLA: Basi mamaa....Basi mama sifanyi tena...Sifanyi tena (ANAMUACHA)... Haki Ya mungu sifanyi tena...Sifanyi tena.

MAMA DOLA: Utafanya tena?

DOLA: Sifanyi tena...Haki ya Mungu naramba mchanga.

MAMA DOLA: Eti !...Waramba mchanga !...Halafu ukishikwa na minyoo... nani atakupeleka hospitali... Kumbe wewe huna adabu hata za kuvalia nguo (anachapa mfululizo...) Baradhuli, sulisuli mkubwa ! (ANAPOZIDI KUMVHAPA...BABAKE ANAINGIA AKITOKA UVUVINI)

BABA DOLA: Kuna nini...Kuna nini. Mbona kelele zimezidi...Dola amefanya nini, mbona unamtandika utadhani tonabari.

MAMA DOLA: Huyu ni makhuluku tabu, keeshazoea adhabu. Punda haendi ila kwa fimbo. (AKITAKA KUMCHAPA LAKINI- ANAZUIWA NA BABA). Unabahati pepo wangu wa kinyamwezi hunipandi siku kama ya leo lakini we ! ungenitambua.

BABA DOLA: Bibic, mafarakano haya yote yameletwa na nini?

| | |
|---|---|
| MAMA DOLA: | Muulize huyo bintiyo eti. Umri huu aliwo nao tayari kesha jua kuinika kinu cha kutwangia. |
| BABA DOLA: | Swadakta Mwanagu |
| MAMA DOLA: | (KWA MSHANGAO HAMAKI) Swadakta?! Swadakta za nini. Yaani mambo aliyo fanya yamekufurahisha? |
| BABA DOLA: | Sasa kwa nini nisifurahie. Mwanangu ameshajua… Kuinuka kinu. Baadaye atajua kutwanga au kupepeta nafaka. |
| MAMA DOLA: | Baba Dola! Yaani wajifanya huelewi kiswahili? Ngoja nikutoe taka masikioni. Dola bintiyo kesha aanza kujifunza kukwea minazi na kugema. |
| BABA DOLA: | (MSHANGAO) Mambo haya yote, Dola mwanangu kajifunza kwa usiku mmoja tu! Mashalla!. |
| MAMA DOLA: | (AKISTAAJABU) Mashallah ???Aghstafiruu… Mashaka haya mwana mjake kuvaa ngua mwaka. Mashallah ni za nini? (ANAPIGAKOFI) Mtume na asimame!….haya, mtwae huyo mtlailshamsi wako, umvike nishani ya dhahabu, kwa hayo aliyofanya, akiisha gemwa barabar, ndipo utaelewa, maana ya tabia chafu. |
| BABA DOLA: | Tabia charu! |
| MAMA DOLA: | Tabia dafu (AKIELEKEA NDANI) |
| BABA DOLA: | Mama Dola…Mama Dola (AKIMZUILIA) Hebu subiri kidogo wajua mimi mpaka sasa sijaelewa sawa. Hebu nitoe gizani… Kwani Doala, amefanya nini hasa, kikubwa. |
| MAMA DOLA: | Dola hakufanya lolote, hili ni vice versa. Nimemfumania kule kichorochoroni, na yule kizuka wa mzee Juma kitwana wakitafunana midomo! |
| BABA DOLA: | Wakitafunana midomo?… Na huko ndio kufanya nini? |
| MAMA DOLA: | Si huko ni kupigana busu? Mdomo bin mdomo. |
| BABA DOLA: | (ANASHTUKA) Lahaulah! Huyu, huyu Dola wangu? |
| MAMA DOLA: | Hizo hozo Dola Zako. Kwani ni zipi zingine ni hizo hizo. |
| BABA DOLA: | Suhana Enh!…Mwana huyu, hana haya, wala hajui vibaya (KESHA PADWA NA MORI) Nipe mimi huo ufito, nimfunze alifisomwavyo. (ANAMFUKUZA MBIO-DOLA ANACHURUPUKANA KUTOROKA). Umekimbia sio? Utaona…Mwenda tenzi na omo, marejeo ni ngamani… Hapo ndipo utakapojua kilichomtoa kanga manyoya mtazame… ananuka kwapa ! |
| | (ANAPOGEUKA ANAMUONA MAMA MAJUTO ANAINGIA) Unafanleik!… Akimbiapo shetani – yuwazuka subiani.. |
| MAMA MAJUTO : | Habari za asubuhi shemegi? |
| BABA MAJUTO: | Habari za asubuhi, kamuulize jogoo. |
| MAMA MAJUTO: | (KIMYA KIDOGO) Mimi nimekuja. |
| BABA DOLA: | Nakuona umekuja, lakini kitu kinachonishangaza ni kuwa .. umeelekezwa, umeagizwa ama umetumwa kwangu ! |
| MAMA MAJUTO: | Nimekuja kumtizama mwanangu. |
| BABA DOLA: | Ulisikia hapa ni 'maternity' au 'Nursery school'. |
| MAMA MAJUTO: | Siyo hivyo shemegi. Milipata fununu kuwa amehamia hapa. |
| BABA DOLA: | Eeeh ! Naona hapa ni "boarding and lodging". |

| | |
|---|---|
| MAMA MAJUTO: | Shemegi, mbona hutaki kunielewa? |
| BABA DOLA: | Mimi sielewi wala sisikizi wanawake. |
| MAMA MAJUTO: | Shemegi ! |
| BABA DOLA: | (Kwa ghadhabu..)Shemegi – Shemegi gani ? Mimi sasa nimekuwa shemegi kwa vile muko matatani? Jahazi lenu linazama sasa ndio….Shemegi, Shemegi nisike hapa, shemegi nishike kiuno. Ama kweli, wasohaya wana mji wao. Yaani, tayari umesahau … hukumbuki…. |

## REHESHI I

| | |
|---|---|
| | Baba Majuto anaonekana akicheza Golf. |
| BABA MAJUTO: | Kaka, mimi naona maji yamezidi unga….siwezi kulea jogoo, kuku na kifaranga chake. Kwa hivyo itakubidi wewe na familia yako muondoke. Nyinyi ni kama marobota yasiyo na thamani. |
| BABA DOLA: | Lakini kaka si-ungeli- tulifadhihapa jijini halafu… |
| BABA MAJUTO: | (anatoa Mobile phone) Kahidi Jogoloo…lete hiyo mizigo iliyo ndani ya bandali ya unga. |
| BABA DOLA: | Kaka….wewe ni wakunifanya hivi kama ambaye hatukutoka tumbo moja… |
| MAMA MAJUTO: | Haha ! mulitoka tumbo moja, lakini wakati mbalimbali kwa hivyo hamuna budi kuwa mbali mbali…. |
| BABA MAJUTO: | Kama mbingu na ardhi. |
| KAHINDI: | Haya, mamsatubuh. Mizigo ndiyo hii. |
| BABA MAJUTO: | Wapeleka katika kitu cha gari la moshi |
| BABA DOLA: | Kaka yaani wanifukuza kikweli—kweli |
| BABA MAJUTO: | Astala-vista (akiondoka) rejeshi inakwisha. |
| MAMA MAJUTO: | Shemegi, yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. |
| BABA DOLA: | (Kwa hamaki) yajayo !…wewe wayaweza yajayo… Nakuuliza, waweza kuyahimili yajayo ? (kimya) Basi yajayo ni haya (kwa sauti ya juu) Toka…toka nyumbani mwangu (anatengeneza kapu lake. Anapomtazama mama Majuto bado hajaondoka)…Ala ! wewe ni nyani wa aina gani usiye elewa maana ya neno toka.. toka! |
| MAMA MAJUTO: | Shemegi, hebu punguza hamaki, hasiwa ni hasara. |
| BABA DOLA: | Hasira si hasara, ni mshahara. Mshahara wa uovu na unyama mlionitendea wewe na mumeo…Ikiwa ni mwanao, kweli alikuwa hapa. Tukamuhifadhi, tukamuuguza kwa hali na mali. Maradhi yaliponzidia tukampeleka hospitali – Coast General …Nadhani umeshajua alipo mwanao sio? ….Haya…anza ! toka !. |
| MAMA MAJUTO: | Shemegi si… |
| BABA DOLA: | Toka..Toka Kabla sijateremsha kiyama hapa…Tokaa..Toka ! (Mama Dola anatokeza kashikilia upawa). |
| MAMA DOLA: | Haya kuna nini, mbona nasikia fujo. |
| BABA DOLA: | Kwani wewe ni G.S.U., usikiapo fujo tu ushajitokeza na rungu lako. |
| MAMA DOLA: | Mmm..mimi najua hizo ni hasira za kukosa samaki uvuvini. |

BABA DOLA: Mwanamke uskinikumbushe kisirani cha uvuvuni, ama nitakuvua wewe.

MAMA DOLA: Basi…Basi yeshe. Yamekwisha (mara anamuona mama Majuto) Mama Majuto, mbona umejikita hivyo kama mlingoti? Ingia ndani.

BABA DOLA: A…Aa…Aaa..! Hapahapa ! Humo ndani aiingie, kunanuka vumba na huyu ni bibi ya waziri. Tena waziri wa afya.

MAMA DOLA: Sasa…Tuongee hapahapa nje? Makubwa basi.

BABA DOLA: Humo ndani nimekutangaza hali ya hatari, yaani majensi kwa lugha ya kimambo 'dangerous'.

MAMA DOLA: Baba Dola, yaani hiyo hali ya hatari umeitangaza kwa mama Majuto tu, mbona Majuto hukumtangazia hiya majansi?

BABA DOLA: Mke wangu yafaa uwelewe aliyotufukuza sio majuto, bali ni wazazi wake. Huyu hapa aliwa mmoja wao. Isitoshe Majuto ni ngonjwa na yeye ni mtoto mdogo, ni sawa na malaika wa Mungu.

MAMA DOLA: Na huyu hapa

BABA DOLA: Huyu ni malaika wa….

MAMA DOLA: (Anamkatiza) Malaika wa Shetani siyo? Hebu mume wangu piga audhubilahi umlani shetani. (akimshika). Yanayamsibu Majuto ni yetu sote nasi ni kama wazazi wake. Kw hivyo hasira za kale zitupilie mbali.

BABA DOLA: Lakini mke wangu hawa walitufuku…

MAMA DOLA: (Anamkatiza) Naelewa…naelewa, lakini yaliyopita yamepita tusahau. (Akizidi kumbebeleza) Tofauti zetu za kale kuzitupilie mbali.

BABA DOLA: Lakini walitufu….

MAMA DOLA: Aaah mumem wangu…wasamehe…wasamehe..ehh. Darling….

BABA DOLA: Wanawake (akiwaameshawishika) Mnaweza kuingia, hali ya hatari imeondolewa. (anaenda kutoa bidhaa zake)

## ONYESHO LA SITA

(Majuto aliyedhoofika anaonekana akilalamika huku kajifunga kitanzi akitaka kujinyonga)

MAJUTO: Majuto yaliyonifika sina wa kunisaidia. Adhabu ninayoipata siwezi kusimulia..sina mimi wa sinani, sina hata wa kunipa maji..(kwa uchungu) Ewe Mola, kwanini kunipiga kipigo hiki? Kwani ukanitweka kinamasi hiki?…(huku akilia) hawapo watu, walio maamuma wa shetani, waliouoga kwa tui la ui wanaofaa chungu hiki?…. Majuto, nimeteseka vya kutosha …Mola, nimedhiika vya kutosha…Ichukue roho yangu mie ni radhi, sina kinyongo…pokea nafsi yangu, uiweke mahali ifaapo (anarusha kamba juu kutaka kujinyonga…shamu anatokeza..)

SHAMU: Majuto !! Majuto rafiki yangu mpenzi… bona wataka kutoa uhai wako?

MAJUTO: Shamu..tafadhali, nakuomba, niwache peke yangu.

SHAMU: Majuto, usihini uhai wako bure. Katu si suluhisho. Muombe Kahari akufungulie njia.

| | |
|---|---|
| MAJUTO: | Sina haja ya kuomba, njia yangu iwazi, yanishubiri mie tu… Shamu… Ulimwengu huu simo tena hesabuni…(kwa ukali na uchungu) Yanini nizidi kudhiika, yanini? |
| SHAMU: | Majuto…Majuto nitazame…niangalie (kimya). Mimi nikilema mbona sijakata tamaa na maisha ….Mimi sijakutupa, wakati wote nimekuwa nawe, nimekuuguza… Mbona wanitoa shukurani? |
| MAJUTO: | (Kwa kulia) mimi sitoi mtu yeyote shukurani lakini, sioni kama nina manufaa. Sifai kitu humu duniani..Mimi ni mzigo. (wakati huu baba Majuto alikuwa akipanda jumwaani polepole). |
| WOTE: | Wewe si mzigo. |
| BABA MAJUTO: | Wewe si mzigo. |
| MAJUTO: | (Akimgeukia kwa ghadhabu) Wataka nini, watafuta nini hapa? |
| BABA MAJUTO: | (Kwa upole) Majuto mwanangu…. |
| MAJUTO: | (Anamkatiza kwa sauti ya juu) Abadan ! mimi si mwanao. Sikuwa, sijawa na sitokuwa. Siye wewe uliyenikana, ukanifukuza, ki-umbwa, ki-uguruwe nithili ya mbwa msikitini…siye wewe?!! Kul-naam !! |
| BABA MAJUTO: | Kitendo changu najua kilikuwa cha kinyama. Hakika, sikustahili kufanya hivyo.. |
| MAJUTO: | (Akimkatiza) Na kuwanini ukafanya hivyo? |
| SHAMU: | Majuto, maji yakishamwagika hayazoleki |
| MAJUTO: | Niwacheni nitimize azimio langu. Sina na wala sitaki muhali na mtu. Mwani…ehh (anawatazama) kwani nikifa kuna hasara gani? ..(akisisitiza). Kuna hasara gani kwenu…Dhoruba inayonidhalilisha tayari imenikinaisha…Kibwebwe, sina budi kutiteremsha…Mauti kuyakabili. (anarusha kitanzi kutaka kujinyonga mara mama Majuto na Baba Dola wanaingia) |
| WOTE: | Majuto !!! |
| MAJUTO: | (Kwa kuudhika) Aaak, mbona hamuishi kuniandama kama mtama..kitambo mlinipiga teke, nikawa niko pweke…mbona sasa umyo-unyo ehh! Mimi ni mtengwa. |
| MAMA MAJUTO: | Wewe si mtengwa. |
| BABA MAJUTO: | Mishale yote najua imeelekezwa kwangu. Vitendo vyangu vilikuwa vyenye ukatili usio muthili. Majuto, nimejuta vya kutosha Maisha yangu yote yametawaliwa na majuto… Majuto ya vitendo, majuto ya nafsi. Mke wangu…kaka, najuta…nimejuta…Tafadhalini musiniache. Nizidi kujuta. |
| MAJUTO: | Bado hujajuta. Mwanzo wa ngoma ni lele, mwisho… mwishowe hujiri kelele. Jitimai linaloni fadhaisha ni usiku wa kiza kwenu. Sikupenda kwangu …. Sikupenda kwangu kuwa hivi !! |

## <u>REJESHI II</u>

| | |
|---|---|
| | (Wakiwa safarini, gari linaegeshwa kwa mda ili aboria wajisaidie. Baadaye dereva anakama usukani) |
| DEREVA: | Mshaingia nyote sio ? … Haya tunaondoka. (Ghafla gari linasimamishwa na magaidi, mashifta) |
| SHIFTA I: | (Anaamrisha) Gila mtu chini. Nyote nashuga jinni…waria sharore…laagdon (tafsiri: - Sharore mjasiri, kusanya pesa). |

SHIFTA II: Nyoote sasa nafuta amri ya amiri

SHIFTA I: Haya walimu yote nakaa kibande hii. Wanafunzi kibande ile. Walimu yote kuja mbele… nyinyi taruka gamba.

ABIRIA WOTE: Kamba ! (wanaelekezwa bunduki, wote kinya).

MAJUTO: Hili haliwezekani. Haliwezekani kabisa. Hawa walimu ni swawa na mama zetu. Hiyo si haki. Si haki kabisa.

SHAMU: Si haki kabisa. Ndiyo haiwezekani.Patazuka kivumbi leo hapa. (Anapigwa risasi ya mguu)

SHIFTA I: Haki?…wewe najua haki? Ngoja sisi nafundisha wewe haki…kina mama yoote sisi nasamehea…wasichana yote, kiongozwa na binti haki…..taruga gamba.

SHIFTA II: Sodoxo – sodoxo ( Tafsiri:- haraka – haraka ) (Majuto ananajisiwa kisha mashifta wanatoweka.

## REJESHI INAMALIZIKA

BABA MAJUTO: Majuto mwanangu, mbona hukutueleza kutoka awali …utengano, mvunjiko wa jamii…yote haya hayangejiri.

MAMA DOLA: Jamani, mavi ya kale hayanuki.. yaliyopita…

MAMA MAJUTO: Yamepita. Tuunganeni ili….

MAJUTO: (Anamkatiza) Hatuwezi kuungana! Kabda nyinyi…mimi katu! Niwachemi nipunzishe roho yangu…Ukatili na unyama nilio fanyiwa, ni dondo ndugu moyoni wangu.

MAMA MAJUTO: Mwanangu Majuto,…yaani mimi nimetoka nitokako nikushuhudie ukitoa uhai wako?

MAJUTO: Mama, lakivunda halina ubani.

BABA MAJUTO: Majuto usijiue. Jamani ongeeni naye. Kaka…mama Majuto kwa matendo yangu.. Najua nilikosa…Najua mimi ndiye chanzo cha kimamasi hiki…Lakini njoo, mikono yangu iwazi.

MAJUTO: LA!

SHAMU: Majuto usituweke katika taharuki..njoo, sote tuko nawe.

BABA DOLA: Jumuika nasi..yakale tumeyazika katika kaburi la sahau..Tazama…Huu ni mwamko mpya wa jitimai.(wanashikana mikono).

MAJUTO: Najua nyote mwanithamini lakini utandu ulio ninasa haunasuliki !

WOTE: Majuto njoo…

MAJUTO: Siwezi

WOTE: Jaribu…

MAJUTO: Si-we-zi…

WOTE: Tuko nawe…..
(popole anashuka, jamii inafurahika. Anamkumbatia Shamu, mamake, Shangazie na Ami. Baba anakufa moyo anaondoka..)

MAJUTO: Baba ! (wanakumbatiana)…

## TAMATI.

## Kiambatisho 3c

# MONALISA

*Na MASINDE W.K.E. WENCESLAUSE.*

**WAHUSIKA**

| | | |
|---|---|---|
| Monalisa | - | Msichana Mdogo |
| Luseka | - | Babake Monalisa |
| Tina | - | Mamake Monalisa |
| Timothy | - | Mwandani wa Monalisa na wa Darsa Moja. |
| Walimu Mkuu | - | |
| Mhazili | - | |
| Mlinzi | - | |
| Malaika | - | |
| Kasisi | - | |
| Chansela | - | |
| Ziraili | - | |
| Hakimu (Kortini) | - | |
| Christabel | - | Dadake Tina |
| Mlinzi (Askari) | - | |
| Hadhira | - | |

**MUHTASARI.**

Mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Kwa majanga, maovu na mateso, jitihada haiondoi kudura. Monalisa ni mchezo unaohimiza na kuthibitisha mada kuwa wema hukithiri ui.

Utangulizi.

Muziki wa kuongoa unasikika kutoa taswira ya wahaka mara pazia linafunguliwa. Mandhari ni ya kufikirika. Kuna lango lililotengenezwa kwa mifupa ya binadamu. Ni siku ya kutuzwa shahada za digrii. Tina na mwanaye Monalisa wanaingia.

Tina : Mfungulie mwanangu lango. Amegaagaa na upwa hata akatwaa shahada ya digrii. Mbona wambagua? Fungua lango hili.

Hadhira : (Kutoka kwa watazamaji) Fungua lango. Fungueni.

Sauti I : Nachelea kufungua lango jua la kuangaza limebanwa na

mawingu meusi ya tanzia.

Hadhira : Mawingu mazito ya tanzia.

Tina : Tutafanyaje?

Hadhira : Tutafanyaje?

Sauti 2 : Torokeni sasa. Timkeni wasichana, msikabiliwe. (Wasichana wanatimuka mbio huku wachache wakinaswa na viwakilishi vya taasubi za kiume)

Tina : Lione janajike la kiafrika limekabwa mtegoni mwa maangamizo. Binadamu amepigwa kumbo. Huruma na ueledi wa wanawake umerushwa chungu bovu ndungu zanguni. Tutaketi na kushuhudia wasichana wetu Wakielekea jongomeo? Wakati ni leo namsema kesho ni mwongo. W aamuzi w atukufu nawaamrishi kutaliki k alamu na majalada kwa kuwa kita cha wanadada kimeanza na mwanangu Monalisa ndiye rubani.

(Watu wanatoka Monalisa anabaki ameshika tama)

***(TAMATI YA UTANGULIZI)***

Tina : Luseka, mbona wanizonga!

Luseka : Nitamwoa mwanamke mwingine. Labda kutoka kwake nitapata jana dume wa kurithi mali yangu; ng'ombe wangu na shamba langu. Mwana wa kiume wa kuwa *ngao* yangu wakati wa janga. Nataka kijana wa kiume Tina- kwa kuwa boma bila *jogoo* ni sawa na kiza bila nuru........ mwanamme bila mwana wa kiume ni sawa na ng'ombe aliyefinywa maksai.

Tina : Lakini huwezi ukamwoa mwanamke mwingine Luseka. Kumbuka ulisema kuwa mapenzi hayagawanywi hasa kwa mke mwenza.

Luseka : Huo ulikuwa wakati ule-kwa sasa majani chai yamenawiri na damu yangu i moto. Nitachuna majani chai na kumwoa mke wa pili. Basi maongeo kuhusu elimu kwisha! forget! Monalisa, wanielewa. Finished!

Monalisa : Lakini baba elimu ndio ufunguo wa maisha hasa katika karne hii. Bila ufunguo huu maisha hayapo tena. Natumai kusoma niwe rubani.

Tina : Mimi mamako nitakupa ari na motisha. Lo! Ndoto yangu ni kumwona Monalisa rubani. Apaaye kwa ndege mufti na murua. Shabash!

Monalisa : Lazima niende shule baba. Sina budi kwenda.

Luseka : Na nimesisitiza kwamba huendi.

Monalisa : Lazima nitakwenda. (Anamzaba kofi)

Monalisa : Nitateseka hadi lini minyororoni mwa taasubi za kiume? Nitadunishwa hadi lini? Ndoto zangu mama, ndoto za kukwea daraja la elimu. Nimejitahidi mama kufanya yote niwezayo. Ili nivuke daraja hili. Fauka ya hayo, nimedhulumiwa na kuwekwa na kuzikwa katika kaburi la sahau.

Tina : Simama mwanangu. Simama ufute machozi ya kumbukumbu za siku za mateso na majonzi. Leo, mama, utaenda shuleni usikate tamaa.

Monalisa : Pesa tutazipata wapi, huku taasubi za kiume zimembana mwanamke na kumtumbukiza ufukarani?

Tina : Ng'ombe yule niliyenunuliwa na kundi la kina mama, nitamwuza.

Monalisa : Hiyo itagharamia tu asilimia hamsini ya pesa zote zinazohitajika.

Monalisa : Baba w e! M atokeo ya mtihani y ametangazwa n a nimepata alama A katika masomo yote – Hivyo nimepata nafasi katika shule bora ya taifa – Utubora!

Luseka : Umemaliza kusema?

Tina : Wamzungumziaje mwanao? Hufurahii matokeo haya. Amejitahidi mno - b asi n awe jitahidi u pate k usoma-labda siku moja atatuzoea kutoka kwenye janga hili la ufukara.

Luseka : Janga la ufukara? Wanitusi mie? Mimi Luseka waniita fakiri?

Monalisa : Basi mpeleke shuleni.

Luseka : Si lazima kusoma ili upate maisha mazuri siku za usoni. Mimi sikupata kuona hata paa la shule. Hili halijanizuia kupata mali. Nina shamba la majani chai na hekta sitini za ardhi. Fauka ya hayo, jumba langu la fahari limejengwa kwa mawe.

Tina : Hebu mkumbuke dadangu Kristabeli.

Luseka : Huyo ni Kristabeli, mimi ni Luseka.

Monalisa : Nami ni Monalisa ambaye alufunzwa kwamba kumfunza msichana ni kama kufunza taifa zima.

Luseka : Kumfunza mvulana kweli ni sawa na kulifunza taifa zima, lakini kumfunza msichana ni kama kunyunyuzia maji

shamba la jirani.

Monalisa : Lakini baba.

Luseka : Toka! Nasema toka! (Anatoka akilia)

Tina : Mbona wamfanyia hayo yote?

Luseka : Wewe ndiwe uliyeshinikiza taka hizo zote akilini mwake.

Tina : Lakini bado ni mtoto bwanangu – mtoto mwalimwali – mbona humfunzi kama kwamba ni mwanao?

Luseka : Huyu! Si mwanangu huyu.

Tina : Luseka!

Luseka : Ni kweli – nakana – wasichana wote ni wa mama na wavulana wote ni wa baba. Kama kweli wataka kunizalia basi na awe wa kiume. Hapo ndipo itajulikana kwamba we Tina si tasa.

Tina : Lo! Kumbukumbu za siku ile nilipoamua kuolewa nawe zanipa huzuni mno. (Anaingia Kasisi. Rejeshi ya siku ya harusi).

Kasisi : Mungu awabariki, katika ndoa yenu. Katika ndoa yenu Yesu Kristo awe tegemeo lenu kwa upendo na umoja kwa kuwa anasema njooni enyi mlio na taabu nami nitawapa burudani. Ndugu zangu, kila kitu ambacho Mungu amekiweka pamoja.....

Umati : Hakuna anayeweza kutenganisha.

Kasisi : Basi nawatangaza Luseka na Tina kuwa mme na mke. Basi enendeni mkaijaze ardhi kama mchanga wa bahari. Amina (vigelegele).

Luseka : Na hapo nakumbuka mdundo wa msondo ngoma.... Nami nikawa sogora.

Tina : Nami nikasakata rumba ya uzazi. Nitasahau vipi uchungu wa uzazi niliouhisi! Bado nakumbuka Luseka! Uchungu wa

mwana aujuaye ni mzazi. Ah! Naumwa! Naumwa! Siwezi kustahimili zaidi... ah! (Anaigiza kuzaliwa kwa mwana. Vifijo)

Tina : Huyu hapa mme wangu. Toto jike nitamwita.

Sauti 1 : Kristabeli...

Sauti 2 : Winnie.....

Sauti 3 : Brenda.....

Sauti 4 : Sara....

Sauti 5 : Monalisa....

Tina : Ndio, Monalisa, ni jina mwafaka.

Luseka : (Akimtazama) Nilitarajia mvulana Tina. Si hiki kunyangarika jike. (Tina analia huku Luseka akijongolea mifupa iliyo taashira ya taasubi ya kiume.

Tina : Hata kama humtaki Monalisa, uliahidi kunipenda kwa mema na mabaya, ugonjwa na afya. Unakana?

Luseka : Kawaida za ulimwengu. Zinapinga pendekezo lako kwa kuwa mapenzi hupukutika wakati wa kiangazi. Tizama anga, Tina! Tizama taa za barabarani. Ni rangi gani? Ni kijani kibichi, basi toka uende zako.

Tina : Sitoki!

Luseka : Utatoka....

Tina : Nimedinda!

Luseka : Utatoka

Tina : La! Sitoki

Luseka : Mimi ndiyc kichwa cha boma hili na nimesema utatoka.

Tina : Sitatoka Luseka? Sitakaidi imani yangu kwa uhai au mauti.

Luseka : Lakini wewe ni kama ardhi butu ambayo haitatoa mavuno tena.

Tina : Lakini teknolojia ya kisasa yasema kuwa ardhi yaweza kutoa mazao ikitunzwa vizuri.

Luseka : Haiwezekani. Mali ghafi imeporwa kwa mmomonyoko na kuangamizwa kabisa.

Tina : Koma kunitusi bozi wewe!

Luseka : Waniita bozibozi?

Tina : Naam... na hata najilaani kwa kuhusiana nawe...wewe ni nduli...... ziraili!

Luseka : (Anamzaba kofi. Tina anaanguka chini) namwona huyo leo ataimbia wimbo wa tanzia (akitoka kwa haraka).

(Shuleni, paliojitenga, anaingia Monalisa.... Anaangalia huku na huko kasha anaita.)

Monalisa : Timmo! Timmo!
(Timothy anaingia kwa bashasha)

Timothy : Monalisa

Monalisa : (Wanakumbatiana) Oh Timothy.

Timothy : Nilijua kwamba hungenidanganya. Hata katika hatari.

Monalisa : Ningekudanganya vipi huku umenitanda akilini hasa wakati huu wa valentino. Huoni umande unavyometa meta kana kwamba ni vigae vya vioo vilivyopasuka.

Timothy : Matamshi yako yanaweza kumtoa nyoka pangoni Monalisa. Najihisi kama kibogoyo aliyeota meno. Ningekuwa ndege ningepuruka.

Monalisa : Lakini huna mabawa.

Timothy : *Wewe ndio mabawa yangu* Monalisa. Najiona nikiruka

angani bila ya tahadhari yoyote hata ya jua linalochoma. Maneno yako ni kama ganga ganga ya mganga. Kwa ajili yako naweza hata kujitoma baharini. Hata iwe na urefu upi. Mkono wako mwororo unaponigusa, hunifanya kuhisi joto mwilini.

Monalisa : *Usichomeke bwana* - siwezi kuhimili maisha bila wewe.

Timothy : Siwezo kulala Monalisa pasipo wewe, umenitanda akilini.

Monalisa : Uongo! Wewe hulala kama gogo la mti!

Timothy : Moyo wangu *umekoma kupiga kwa sababu* yako.

Monalisa : Mbona basi ungali hai? Ungekuwa maiti.
Timothy : Wanipenda kweli Monalisa? Monalisa wanipenda?

Monalisa : (Akisonga karibu naye)
Naam nakupenda.

Timothy : Basi nipe mkono wa ndoa – na tucheze ngoma za kitamaduni. Ngoma za busara.
(Wanatokea Mwalimu Mkuu na naibu wake.)

Principal : Flonina! Flonina! (Anaingia mhazili)

Mhazili : Naam!

Mw. Mkuu : Hao wanafunzi bado wako hapo nje.

Mhazili : Naam.

Mw. Mkuu : Waelekeze ndani
(Timothy na Monalisa waingia)

Sasa tega sikio! Halmashauri ya shule imefanya uamuzi wake. Kabla naibu wangu kukueleza uamuzi wetu, lazima ufahamu kwamba tumechukizwa sana nanyi. Hasa wewe Monalisa. Njoo hapa! Piga magoti! Wewe ni msichana mwerevu sana. Sielewi kwa nini umekubali kundanganywa. Mwalimu endelea!

Naibu : Timotheo Kiprono!

Timotheo : Naam Mwalimu.

D/H/M : Utakuwa topasi juma lote. Upate hamsa wa ishirini (viboko sita) ndipo urudi darasani. Wewe Monalisa, umekufuru na fauka ya hayo, umetolewa mzigo wa kuwa mwanafunzi katika shule hii. Funganya virago na shule hii uione paa.

Monalisa : Haiwezekani Mwalimu.

Principal : Yote yawezekana. Na yamewezekana shule hii imekupiga teke.

Monalisa : Lakini mwalimu hukumbuki faida yangu hapa skulini. Yale niliyofanya. Zawadi nilizoleta shuleni kwa umahiri wangu katika uigizaji. Niwieni radhi.

D/H/M : Nani atamruhusu kuku kukaa na vifaranga. Huoni kwamba watajifunza kutaga mayai?

Monalisa : Nisamehe mwalimu. Natumai umeokoka, thibitisha uokovu wako leo. Nipe ruhusa niendelee na masomo yangu.

D/H/M : Mlinzi! Mlinzi! Huyu kiruka njia...eeh. Nisifumbue macho nimwone hapa.

Monalisa : Lahaula labda ni ndoto hii. Ole wangu nithibitishie kwamba ninaota na kuwa punde tu nitakuwa macho. Naona maisha yangu yakiporomoka. Matarajio yangu yanafifia maisha yangu ya usoni yanatokomea.

(Nyumbani kwake Luseka anaigia Tina)

Tina : (Amepigwa na butwaa) Monalisa! Habari ya shule?

Monalisa : Je! Utanisamehe mama? Nimekukosea!
Nimekupaka tope na hadhi na heshima zako nimezitupa.

Tina : Mwana we! Umepagawa?

Monalisa : Nimekupaka masizi. Nimekuwa dubwasha la maangamizi usinishike. Tina... mimi sifai kuwa bintiyo.

Tina : Mbona huna haya ya kuniita jina?

Monalisa : Sifai kuitwa mwanao. Nastahili kubobea katika ufu. Kashfa na maangamizi yameninyoshea mikono.

Tina : Monaliza! Shida ni nini?

Monalisa : Hapa mama, waraka kutoka shuleni.

Tina : (Akifungua...) waraka... wa nini? (Anasoma... mshangao). Eti! La haiwezekeni. La! Monalisa wewe mkembe. Kifaranga tu, utafuatana vipi na majogoo.

Tina : Kazi hiyo ni ya hawa wanawake. Hawa watembaeao Koinange. Hawa makware.

Monalisa : Nisamehe mama... ni shetani.... Alinifanya kuwa mbuyu wake... kwa ukembe wangu alininasa.

Tina : Nitakusamehe vipi Monalisa?...
Mimi nimekusetiri, nimekufunza utubora. Mbona wanikosea heshima? Nilitarajia kuwa utapita mtihani... uniletee shahada nitundike ukutani. Sasa hivi shahada umejitundika mwenyewe!

Luseka : Ni vioja gani hapa? Mbona nyuso zenu ni kaa vinyesi vya ngombe kichinjioni? Monalisa! Umekuwa bubu? Nyumba yangu mmeibadili kuwa matanga .... Machozi yenu hata yataleta mafuriko hapa tusombwe hadi ziwani.

Tina : Luseka! Mwanetu amefukuzwa shule.

Luseka : Eti! Ni mja mzito?

Monalisa : Nisamehe baba! Nisamehe!

Tina : Msamehe Luseka! Msamehe!

Malaika : Msamehe Luseka kwa kuwa Bibilia yasema msamehe mara sabini mara saba!

Ziraili : Wasemaje Luseka! Wakumbushe miaka minne iliyopita.

Luseka : Tina! Wakumbuka miaka minne iliyopita papa hapa?

Tina : Ndio! Nakumbuka bwana.

Ziraili : Ulimwambiaje?

Luseka : Nilikwambiaje?

Tina : Kuwa kumwelimisha msichana ni kama kunyunyizia shamba la jirani maji.

Ziraili : Waona astahili kufa huyo.

Tina : Lakini msamehe bwana, alighafilika.

Monalisa : Nisamahe baba!

Tina : Msamehe Luseka. Huyu ni mwanao. Yuastahili msamaha.

Ziraili : Hili ni kosa kubwa. Yuastahili adabu. Mwadhibu Luseka.

Luseka : Nimsamehe nani? Amekashifu familia yangu... lazima nimwue. Nipe bunduki... Leo utaende jongomeo (akitoa bunduki).

Tina : La! Luseka. Msamehe! Usimuwe La!

Monalisa : Aacha aniue mama... Baba niue. Acha niwe kafara kwa wasichana wengine... niue sasa hivi... acha nitolewe kafara kwa ajili ya vijana wa baadaye.

Tina : Monalisa.

Monalisa : Acha nife mama! Acha nife...

Monalisa : Niue!

Luseka : Huyu ana nini? Kiburi eeh!

Ziraili : Anakupumbaza na kudumaza matakwa yako. Muuwe; (anamlenga Monalisa. Tina anaingilia kati kwa ghafla. Anapigwa kwa risasi).

Monalisa : Mama! Mbona umekubali kutolewa kafara? Ungeniacha mimi nife. Usife mama. Usiniache mama. Luseka umefanya nini sasa? (Luseka anamszaba kofi. Analia huku watu wanakusanyika kama katika matanga. Daktari anaingia na kuashiria kwamba, Tina ameaga dunia. Monalisa naye ameovya. Monalisa anaamka na kuelekezwa kwa maiti yake Tina. Akilia...)

Monalisa : Mama; mbona umeniacha? Ulinisaidia nilipoumwa au nilipochokozwa na wenzangu. Nilipofanya mtihani tulisherehekea nawe. Hakuna mwingine kama wewe. (Wimbo - hakuna mwingine kama wewe unasikika) kwaheri mama, kwaheri, kwaheri.

Kisha nitashuka na kuwasaidia kupanda ngazi ya elimu. Nitakuwa macho ya vipofu. Masikio ya viziwi, ndimi za mababu na miguu ya walemavu. Hata hivyo tushirikiane pamoja ili tupiganie uhuru wa wanawake. Mungu awabariki. Mungu bariki ndoto zetu.

(Wimbo wa mapinduzi huku Monalisa akiteremka hadhirani kuashiria kwenda shuleni. Wanawake wanimba wakitoka jukwaani. Wimbo unahinikiza kisha wafifia. Tina anabaki akiwaza, Luseka anaingia.

Luseka : (Akiita) Tina! .... Bibi weeh!

Tina : Naam mme wangu.

Luseka : Ewe mwizi usipobadilisha mienendo yako wewe, nitakusukuma kwa wazazi wako wakupe wasia. Wanielewa?

Tina : Waniita mwizi mie?

Luseka : Naam. Miaka minne iliyopita, wewe na kile kisichana chako nilifanyaa njama na kumuuza ng'ombe wangu.

Tina : Ng'ombe huyo alikuwa wangu nilimnunua kutokana na ridhaa ya chama chetu cha wanawake.

Luseka : Tangu lini mke akamiliki mali? Na kwa kuwa wewe umekuwa ni wangu, ngombe wako ni wangu, sufuria yako ni

yangu, mali yako yote ni yangu.

Tina : Hapo ni kusema....?

Monalisa : Ni halali.

(Watu wanarudia)

Lady 1 : Bwana Luseka harambee itaendelea. Mimi natoa shilingi elfu tano ya karo. (Vigelegele)

Luseka : Fyata ulimi wako! Harambee hii ikiendelea basi mimi sijashuhudia ukali wa kisu. (Watu wanalalamika)
Harambee hii haitaendelea!

Crowd : Eee!

Luseka : Wee!

Lady 1 : Harambee itaendelea.
Mchango wangu ni viatu.

Lady 4 : Mimi sina chochote ila kufuli na ufunguo. Mwanangu, vifaa vyako vitatuzwa na ufunguo huu pia unaonyesha ufanisi wa siku za usoni.

Tina : Lahaula! Ninafuraha iliyoje kushuhudia siku hii? Sina budi kuwapa pongezi chungu nzima kwa mliyoyatenda. Lakini kwa kuwa ninyi ni kina mama mwaelewa hisia zangu. Basi Monalisa mwanangu umejionea mwenyewe. Basi natumai utaenda shuleni. Jikite kitabuni ili uweze kupata namna ya kuchuma *ghawazi.*
(Vigelegele aongeapo Monalisa)

Monalisa : Ninafuraha si haba. Nawashukuruni nyote. Nawahakikishia kuwa nitaenda shuleni kwa madhumuni ya kuwatoa katika umaskini na maangamizi, unyama na ukatili. Nitaendelea kukwea.

Luseka : Fyata ulimi! Mara ngapi nimekueleza kuwa ni dhambi nzito kudakulia mwanamme aongeapo? Ni nani aliyemwoa mwenzake? Mimi? Wewe?

Tina : Mimi ni mwanamke ndio, lakini nataka uelewe kuwa hata nami nina haki katika boma hili.

Luseka : Eti!

Tina : Naam! Nina haki sawa na yako. Usithubutu tema kunitusi na kunipinda kama gania la mtama
La! Ni haramu!
(watu wanaingia)

Crows : La! La! La! Si halali

Luseka : Mpango gani huu? (anamzaba kofi).
Tina njoo hapa.
Mbona unamea pembe? (mlio wa ngoma).

Tina : Mbona nisimee pembe. Kwani wewe waniona jiwe, au dubwasha lisilo uhai? Jamani, mbona mwawatesa wanawake? Hamwezi mkaelewa?

Kasisi : Ndugu zanguni. Dada yetu ametuacha. Hivyo tuelewe kuwa Tina alikuwa na roho iliyotakasika na kwa hivyo ataende mbinguni. Tina simama na uende kwa Muumba wako. (Wanaingia malaika.... Picha ya Yesu inaonekama. Tina anasimama na kuisongea. Wanaamini kwamba ameenda mbinguni – kortini. Watetesi nje ya korti.

Watetesi : Fungua mlango. Tunataka kusikiza kesi.

Walinzi : Korti imejaa. Sitaruhusu haya hata kidogo.

Afisa : Utetesi huu ni haramu.

Watetesi : Ni halali muuaji lazima afe x 3

Walinzi : Kimya! Na tawanyikeni kabla ya sheria kuwaandama.

Watetezi : La!

Walinzi : Tawanyikeni.

Watetesi : La!

Afisa : Haya wote wanaanguka kisha wanasimama huku mmoja wao akiongea.

Watetesi : Mheshimiwa ninazungumza kwa niaba ya hawa ambao wameumia dhidi ya taasubi ya kiume. Naomba korti sheria na haki imhukumu ili liwe funzo kwa wote.

Hakimu : Monalisa Luseka, una lolote la kusema!

Monalisa : Ndio mheshimiwa. Moyo wangu unaumia, nalia kwa kuwa mama alimwoa huyu nyamaume.

Luseka : Napinga mheshimiwa mbona ananikashifu?

Hakimu : Kimya!

Monalisa : Nilikuwa na rafiki mmoja tu hapa duniani. Mamangu ambaye sasa ni mfu. Yeye ndiye aliyekuwa wa kuninusuru. Nitamtegemea nani ilhali mumewe ni mamba mlafi mwenye *njaa*. Oh! Mamangu! Mamangu mpenzi!

Hakimu : Philip Luseka, una malilio?

Luseka : Mheshimiwa! Tina nami tumepitia makuu. Nilimpenda sana. Lakini uamuzi ni wa korti.

Hakimu : Wenzangu, tumfanyeje afiriti huyu?

Hadhira : Mchome! Mchome! Mchome!...

Hakimu : Basi Philip Luseka umepatikana na .....

Hadhira : Hatia!

Haakimu : Ya mauaji na kwa hiyo atahukumiwa kutupwa kwenye moto wa jahanamu. (Wote wanasherehekea kwa vivijo na nderemo) anapelekwa motoni
(Daraja linaletwa)

Na wee mwanangu, vuka daraja la elimu.

Hadhira : *Vuka daraja Monalisa, vuka.*

Monalisa : Lakini mheshimiwa, kuna moto mvunguni naogopa.

Hakimu : Wewe ndiwe matumaini yetu Monalisa….

Hadhira : Tizameni upande ule mwingine wenzanguni kuna elimu.

Sauti I : Kuna mwangaza

Sauti II : Kuna uhuru wenzangu, uhuru.

Hakimu : Ndio vuka daraja Monalisa rudi shuleni.

Hadhira : Ndio tuongoze Monalisa tuongoze

Monalisa : Lakini Mheshimiwa…

Hakimu : Wewe ndiwe tumaini letu, mwokozi wetu.

Monalisa : (Akilia) Naungua mheshimiwa nisaidie….

Hadhira : (Wanamhimiza kuvuka daraja).

Monalisa : Nimefaulu! Nimefaulu!
(Vigelegele)

Chansela : Kwa uwezo niliotunikiwa na chuo kikuu nakupa shahada na kukuruhusu kuhudumu.
(Monalisa anavalishwa magwanda ya kufusu)

Monalisa : Na kwa kuwa nimefaulu nataka tusherehekee usawa wote.
Mko tayari?

Hadhira : Ndio.

Monalisa : Mko tayari?

Hadhira : Ndio.

Monalisa : Tazama
(Anawaonyesha matunda ya usawa)

Hadhira : Upendo amani haki na utangamano.

Hakimu : Tumeweza ndugu zanguni.
Tumefaulu! Aliyetuongoza ni nani?

Hadhira : Monalisa!

Hakimu : Nani?

Hadhura Monalisa.
(Wote wanaonyesha furaha. Wimbo unaanza polepole kisha wahinikiza wote wanaonyesha mapenzi kwa wenzao. Wanainama huku pazia zikifungwa pole pole.)

## Kiambatisho 3d

### VISOSAUTI

*NA OTIENO NYANGLA NA MASINDE W.K.E. WENCESLAUSE.*

*(Huku pazia zikiwa bado zimefungwa.... Kikundi cha watoto wafananao na wakimbizi wanasimama kutoka miongoni mwa watazamaji huku kukiwa na mdundo wa ngoma pazia zinafunguliwa polepole kuonyesha mpango usiodhihirika jukwaani.... Wimbo wa maombolezo unaoambatana na zana za muziki unaanzwa kuimbwa au wale watoto wanaweza kuimba-nyuso zao za maombolezo – zilizoparara na nguo zilizochanika zinadhihirisha hali yao....*

*Wanatembea polepole kwa unyonge hadi kukwaani na kuchukua nafasi zao pale.... Wimbo huo unafifia polepole huku wakianza kulia)*

Charity : (Akimsemeza Purity) Je, ilikuwa ni lazima utulete mbali hivi kwa mawra nyingine? Kuhaisha machungu ya siku zetu za awali zinazozua masikitiko makubwa..... Najihisi kulia.... Najihisi niikatekate niwe vipande vipande nikomeshe uhai wangu. Ubinadamu wetu.... Maisha yetu yaliyokuwa mazuri.... Maisha yaliyovuma kwa uhai kama miti hii iliyo tulivu .... Iliyojaa amani na kufanana na maji safi yanayopita.... Lakini kama kimbunga kikali kilichojiri kwa mshindo mkuu na kuvuma upande wetu na kuarisha kama jinamizi na kuvuruga yale mazuri mapya tuliyokuwa tukiyapenda...

Hubu tazama bahati ilivyotufifisha hadi tukawa vifefe... Waridi zilizonyauka malafi ya majibwa, mbweha na tai ambao kwa shauku wanasubiri kule msituni na kuhariri upeovu. Sisi tumedharauliwa na kudhulumiwa.

Watoto : Tulieni...wanadamu tulieni
Sikilizeni.
Silikizeni wimbo wetu
Wimbo wa waliohasirika
Na nyoyo zilizosumbuliwa
Nyoyo zinazosafiri ardhi nzima zikiwa na uchovu zikitafuta.
Zikipekua
Zikiangalia
Shamba la Edeni lililopotea
Shamba la Edeni

Linalozua kilio cha furaha
Inayofufua uzuri
Katika ulimwengu uliokwanguriwa.
*(Watazamaji watajulishwa kuhusu mchezo huu kwa ufupi na onyesho litafifia kuelekea kwenye uwanja wa hospitali.)*
Haya yatadhihirishwa na kufika kwa daktari mahali pale).

Daktari : Watoto, ni lipi mlitafutalo kwenye lango la hospitali?

Purity : Tuko hapa kumwona mgonjwa

Daktari : Mnataka kumwona mgonjwa katika hospitali hii?

Watoto : Ndio daktari, twataka kumwona aliyewasha miale ya masumbufu yaliyogagia ndoto zetu, matumaini yetu na yote tuliyoyatazamia.

Charity : Ndugu, dada zangu, kwa huruma za Mwenyezi Mungu nawaombeni kwa mara nyingine tena mniepushe na machungu ya kuyatia macho yangu kwenye kiwiliwili cha ibilisi yule .

Purity : Charity! Charity! Charity! Je, lazima tuyapitie haya machungu tena?

Charity : Haya, naomba msamaha.

Purity : Haya daktari, tafadhali turuhusu tumuone mgonjwa wetu.

Daktari : Mgonjwa mnayetaka kumwona aitwaje?

Watoto : Susana Kositale

Purity : Yu ndani?

Daktari : Kwa vyovyote vile.

Purity : Na hali yake ikoje?

Watoto : Ndio Daktari.... Tafadhali twambie hali yake ikoje?

Daktari : Si nzuri

Watoto : Si nzuri?

Daktari : Ndio wanangu. Ni mbaya. Mbaya mno. Inasikitisha. Nadhani mnafahamu alihusika katika ajali mbaya katika mgodi wake na kutokana nayo baadhi ya viungo viake vya ndani vilidhurika kama mnavyoyaona katika picha hii ya Eksirei figo zake zote zimedhurika. Amekuwa katika mtambo wa kusafisha damu kwa miezi miwili na ikiwa hatutampata atakayejitolea kumpa figo basi yaelekea tutampoteza.

Purity : Hii itachukua muda gani?

Daktari : Figo zinazooza sharti zitolewe katika muda wa masaa saba.

Watoto : Masaa saba?

Daktari : Lau sivyo… basi atakufa.

Watoto : La hasha!

Charity : Acha afe kifo cha uchungu kama kile alichowafanya wazazi wangu wafe.

Purity : Charity kibaya nawe?

Charity : Kila kitu ni kibaya Purity …. Sielewi ni vipi wewe dadangu miongoni mwa watu wengine wote unaweza kumhurumia huyu mwanamke chatu aliyetuingiza katika visa vya ajabu visivyosimulika.

Purity : Charity, hatustahili kujitawisha katika hayo ya jana yanayoaibisha… Daktari kuna uwezekano wa kumwona mgonjwa?

Daktari : Kwa vyovyote vile (akiita) Muuguzi! Muuguzi!
(Muuguzi anaingia)

Muuguzi : Labeka, Daktari.

Daktari : Watoto hawa wangependa kumwona. Bi Susana, mgonjwa wa figo. Tafadhali kamletea huku.
(Muuguzi anaondoka)

Daktari : Ni vizuri kuwa umekuja...mwanamke mwenyewe amekuwa pweke... hakuna aliyekuja kumtembelea tangu aletwe hapa miezi minne iliyopita. Kumpata mtoaji wa figo limekuwa jambo gumu.

*(Muuguzi anaingia akimsukuma Susana kwenye kiti cha gurudumu).*

Muuguzi : Ndiye huyu hapa... huenda mmeona kuwa hawezi kuzungumza. Hii ni kwa sababu amepoteza uwezo wake wa kuzungumza... kwa kweli muonavyo yu katika hali ya hatari.

Purity : Kumpa figo mpya, kutabadilisha chochote? Kwangu naona haiwezekani kumtoa katika hali yake ya sasa.

Daktari : La, figo mpya itampa uhai. Kwangu, uhai ni muhimu kushinda kitu chochote kile na kumbuka kuwa tuna muda usiozidi saa saba kwa kuwa hali yake ni mahututi na isiyo thabiti-inadhoofika dakika baada ya dakika.

Purity : Daktari?

Daktari : Naam, mwanangu.

Purity : Nina swali.

Daktari : Endelea mwanangu.

Purity : Tafadhali niruhusu nimpe figo yangu.

Daktari : Ungali bado mdogo mno. Kumpa figo yako lazima uwe na zaidi ya miaka kumi na mitano. Waama, damu yako lazima ikubaliane na damu yake.

Purity : Damu yake i katika kikundi kipi?

Daktari : Ni moja isiyopatikana kwa urahisi... Ana damu aina ya O-(negativu)

Purity : Mungu kweli u mwema. Charity!

Charity : Ni nini?

Purity : Wewe una damu aina ya "O-" na pia una umri uliozidi miaka kumi na mitano.

Daktari : Je, ni hivyo?

Purity : Ndio daktari… tafadhali Charity msaidie… mpe figo yako uokoe maisha yake.

Charity : Purity umepagawa?

Purity : Nimekuwaje?

Charity : Je, unasemaje?

Purity : Sisemi Charity bila nakuomba dadangu mpendwa… Tafadhali mpe uhai… mwilini mwako mna pumzi yake ya uhai… tafadhali kuwa na huruma, na mpulizie pumzi kidogo ndani yake.

Charity : Mimi simpatii yangu! Huo ndio uamuzi wangu wa mwisho!

Purity : Lakini atakufa.

Daktari : Kwa muda wa saa sita.

Watoto : Acha afe na aenda ahera.

Purity : Nini? Hata nyinyi Magarita, Josephat, Dennis? La hasha!

Purity : Ndugu na dada zangu… Lazima ujistawishe na kujikuza katika kusameheana. Kulipiza kisasi katika utukufu wake usiofaa kutatuongezea tu uchungu zaidi na mateso.

Charity : Huyu mwanamke ni shetani aliye na umbo la binadamu na hastahili huruma bali laana, hastahili kuishi bali kifo.

Watoto : (Kwa huzuni).
Muue, mchome, msulubishe….

Daktari : Kimia! Msisahau kuwa humu ni hospitalini. Kwani hamuoni kuwa mnavuruga amani na utulivu wa wagonjwa wengine? Acha Charity ajiamulie mwenyewe.

Daktari : Tuna saa tatu zaidi la sivyo ataaga dunia!

Purity : Tafadhali Charity!

Charity : Dadangu Purity... Mbona unakwepa ukweli wa mambo? Mbona unanitia majaribuni hadi kwenye kifo changu.... Mwangaza wa maisha yetu ni giza. Susanna, hapa alitupatia yote ambayo hatukuyataka maishani nami kama dadako mkubwa sitakubali kamwe ombi lako la kuturejesha kwenye maisha yetu yaliyopita. Jiondoe kwenye maisha yetu yaliyopita ili tuonyeshe hawa watu aliyotufanyia huyu shetani .... Njoo dada... njoo... Nyinyi wengine ondokeni kwani hamna jukumu lolote la kutenda katika sehemu hii ya maisha yetu yaliyopita... njoo dadangu ... andamana nami katika maisha yetu yaliyopita.

Purity : Tutawezaje kushiriki katika maisha yetu yaliyopita huku mametu amefunikwa katika kaburi hili lilofungwa?

Charity : Acha ngoma ipigwe ili afufuke kwani tuko katika ukale.
(Mama anaondoka kaburini)
Ondoa haya magwanda ya mazishi ili tuyashirike haya ya ukale huu usioepukika.
(Wimbo wa msiba.... Mama anaoondoa nguo zake za maziko na kuwa muhusika halisi. Anaanza kushiriki katika mchezo wa kuigiza).

Prisilla : Charity! Ni saa ngapi? Chukua mkoba wako na uende shuleni?

Charity : (Anaingia) Lakini mama....

Prisilla : Ni nini tena? Kwani ni lazima uwe na kisingizio kila mara wakati wa kuenda shule ufikapo?

Charity : Sio hivyo mama.

Priscilla : Basi ni nini?

Charity : Ni sare yangu ya shule.

Priscilla : Ina nini?

Charity : Ni fupi mno hata kamisi yangu yaonekana, wale watoto wengine watanicheka.

Priscilla : Hilo lisikutie wasiwasi mwanangu…. Nitahakikisha kwamba umepata sare mpya mwaka utakapoanza… kwani hivi sasa nenda shuleni upesi… kwaheri!

Charity : Purity njoo twende. Kwaheri mama!
(Wote wanaondoka kuelekea shuleni)
(Prisilla anaimba huku akipalilia kaburi la mumewe… Anaingia mkemwenza Susanna)

Susanna : Prisilla! Acha unachofanya! Nimekuonya mara ngapi usipalilie kaburi hilo? Inanikumbusha mengi machungu kuhusu kifo cha mume wangu mpendwa.

Priscilla : Alikuwa mumeo mpendwa au mchukiwa…. Kaburi hili liko katika shamba langu na hivyo basi nitafanya chochote nipendacho – nalo.

Susanna : Mambo yanakupita mwenzangu

Priscilla : Una maana gani?

Susanna : Shamba hili ni langu.

Priscilla : La hasha.

Susanna : Ni langu… hebu angalia hati hii mpya ya kulimiliki. Kwa hivi sasa ninamiliki yote yaliyokuwa ya marehemu Mathayo.

Priscilla : Hebu mwangalie huyu shetani…. Huyu mwana haramu…. Huyu sokwe!

Susanna : Acha kunitusi wewe mjinga!

Priscilla : Ungewezaje kufanya haya? Ulipanga ukapata malipo yake yote ya bima na hivi sasa umenyakua shamba lake…. Ni kipi ulimwenguni unachotaka kwangu? Ni ubaya gani niliyokufanyia wewe muuaji?

Susanna : Unaniita muuaji?

Priscilla : Najilaani kwa kuyafahamu haya huku ikiwa imechelewa sana. Nani asiyejua kuwa ulimuua mume wangu… ulimwaga mafuta kwenye chumba chake cha kulala na kuwasha moto. Hukujali mapenzi yake kwako. Macho yako madogo ya mwewe , yasiyo sawa yalifuata hazina ya almasi katika ardhi hii… sasa una vyote…. Kwa nini huwezi kuachana nami katika matambara yangu ya umaskini ili niwalee wanangu waliofiwa na babao?

Susanna : Lakini hii ni ardhi yangu na ninataka uondoke.

Priscilla : Utaitaje mali hii tuliyotolea jasho mimi na mume wangu kuinunua kuwa yako?

Susanna : Mambo huenda yanakupita mwenzangu. Hebu tazama hili agizo la mahakama linalosema uondoke toka shamba hili mara moja.

Susanna : Unawezaje kuniamuru niondoke kwenye shamba la marehemu mume wangu? Zaidi ya hayo kaburi lake bado linanihitaji. Ni jukumu na wajibu wangu mkewe wa kwanza kulitunza kwa makini ili nisikasirishe mzimu wake. Sita cheza wivu wa mshindo wa ngoma isiyofaa sitashiriki ewe mjinga.

Susanna : Waniita mjinga.

Priscilla : Ndio! Wewe ni mjinga mtegemea wazimu! Hayawani! Mnyonya damu!

Susanna : (Akihamaki) Wewe!
*(Anamsongea Priscilla wanashikana… Susanna anashika shingo la Priscilla… anamnyonga…. Anaanguka na kuzirai. Charity anaingia.)*

Charity : Acha unachofanya!

Susanna : Wafanya nini hapa wakati huu? Unastahili kuwa shuleni.

Charity : Umemfanyaje mamangu? Umemfanyaje mamangu?

Charity : Amka mama! Amka!

Susanna : Nyamaza ewe mbwa mwehu! Ondoka hapa.

Charity : Utakosaje ubinadaamu? Sitaondoka hapa bali nitabaki na mamangu mpendwa. Ikiwa wataka kumwua basi utaniua kwanza!

Susanna : Charity, tafadhali niheshimu kwa kuondoka.

Charity : Mimi siendi popote. Sitaruhusu kifo kinipokonye mamangu kutoka kwenye ulinzi wangu.

Susanna : Ninakuamuru aondoke kwani nimehamaki na niko tayari kutekeleza oparesheni nambari mbili.

Charity : Na oparesheni numbari moja ilikuwa ipi?

Susanna : Oparesheni Mathayo out! Nipishe!

Charity : Sibanduki!
(Anaingia Konstatino!)
Mshike huyo mbwa Mzuie
(Konstatino anamshika… zaingia nguvu zinazoashiria kifo)

Charity : La, tafadhali mwache, la! Laa…..
(*Huku Susanna anapomnyonga Priscilla... viwakilishi vya kifo wakati uo huo vinatoa dhoruba yao na kuondoka. Wanaingia malaika wakiwa na utukufu na kuvia roho yake Priscilla)*

Mbona umenifanyia haya Susanna! Umemuua mamangu aliye joto na nguvu za maisha yangu.

Susanna : Hicho ni kielelezo tu cha kipindi kipya Charity.
Mlio mdogo, kubofya kidogo tu hapa na pale na mpangilio wote utajitokeza kwenye ubongo wako!

(Wimbo wa maombolezo – wasikika kwa umbali… wanaingia watu waliomo fikirani mwa Charity).

Charity : La! La! Ninaweza kuwaona wachimba kaburi!

Susanna : Wachimba kaburi? Vema basi hebu songesha kidude hicho na ubofye mara mbili ili uone matukio! (Mlio wa ngoma)

Charity : La mama, tafadhali usiniache!

Susanna : Jivu kwa jivu na vumbi kwenye vumbi. Wafu watawazika wafu! Priscilla kaburini mwako nenda!
*(Priscilla anasimama na kuelekea kaburini mwake. Anapozikwa kunakuwa na wimbo wa maaombolezi. Wengine wanaondoka huku Charity anatembea kuelekea kaburi huku akiwa na s hada l a m aua.... A naliweka k wenye k aburi h uku umati wa watu ukiingia na hali ikiwa ya matanga. Ni katika hali hii Charity anapozidiwa na majonzi na kuanza maombolezi)*

Charity : Mama.... Mama. Mbona umetuacha. Tazama wingu jeusi la mauti linafuni... iliyo ndani yako na bila kutarajiwa linazua uwazi wa kina katika moyo wako. Ni neno mama nililotamka kwanza; ni mama ndiye niliyemwita nilipoanguka na kuumiza goti langu, ni mama niliyemwita wakati watoto wenzangu waliponichezea shere. Ni nani nitakayemwita sasa kwa kuwa umeenda? Nani? Niko pekee mama. Ni peke yangu.

*(Mlio wa ngoma. Mbinu rejeshi hospitalini.)*

Charity : Hiyo ni sehemu tu ya yale niliyopitia wenzangu.... Kushuhudia uhai wa wazazi wangu ukihitimishwa na mkono wa mwanamke huyu aliye na mwenendo usiokuwa wa kawaida... Baada ya haya yote je, ni haki kupofushwa na kumpa mwanamke huyu nafasi ya kuishi?

Watoto : Vipi? Haiweszekani

Purity : Lakini tafadhali elewa.

Watoto : Aelewe nini!

Purity : Maisha ya mwanamke huyu yako mikononi mwako....

Watoto : Yako nawe dadangu... mbona waonea fahari ulipizaji kisasi?

Charity : Dadangu... sijawahi kwamini katika ulipizaji kisasi hata hivyo siwezi kumsamehe aliyekatiza maisha ya wazazi wangu. Purity unakumbuka ndoto zangu na matarajio?

Purity : Nakumbuka kila kitu Charity. Nakumbuka vizuri jinsi ulivyonuia kusoma na kuwa daktari.

Charity : Ndiyo, lilikuwa kusudi langu kusoma na kuwa daktari wakati huo nilifikiri kuwa ningepata uwezo wa kuwakomboa watu wangu kutoka kwenye minyororo ya magonjwa iliwavamia kama nzige wanavyovamia mimea iliyo kijani kibichi... Nakumbuka nilivyoweka kifo cha wazazi wangu nyuma nikaenda shule na kufanya bidii kwa sababu hiyo moja. Sikujua kamwe kuwa nilikuwa ninaandaa ukumbi tu kwa yale mabaya yaliyofuatilia.
Purity, tuko shuleni kwa hivi sasa.

Purity : Nini? Lakini siwezi kuelewa.

Charity : Haraka. Gonga kengele waite wanafunzi kwenye gwaride naibu wa mwalimu mkuu atatangaza matokeo ya mtihani wa mwigo leo hii.

*(Umati wa watu kwa utaratibu unafumkana onyesho linapogeuka na kuwa gwaride shuleni. Purity anagonga kengele... Wanafunzi wengine wanaingia. Naibu wa mwalimu mkuu anawahutubia wanafunzi.)*

Naibu W.M : Hamjambo wanafunzi.

Watoto : Hatujambo.

Naibu W.M : Nina furaha kuwa tangaazia kuwa matokeo ya mtihani wa mwigo ya mkoa yaliofanywa na wasichana wa darasa la nane yametoka.... Wakati huu shule yetu haikuweza tu kuibuka ya kwanza bali pia kuchangia wanafuzi watatu bora zaidi katika mkoa (mashangilio). Hivyo basi, ninamwalika mwalimu mkuu bibi Kiwanuka awakabidhi zawadi wasichana hao watatu.

*(Mwalimu mkuu asonga mbele)*

Katika nafasi ya tatu alikuwa Patricia Karuga (mashangilio anapopokea zawadi yake) katika nafasi ya pili tuna Elerlyne Nomzana (vigelegele) na msichana bora zaidi katika shule yetu na mkoa mzima kwa jumla si mwingine ila ni Charity

Kositale.
(Mashagilio yanakuwa mazito zaidi Charity anapopokea zawadi yake.... Mwalimu mkuu baadaye anahutubia shule)

Mwalimu/M : Hamjambo wanafunzi.

Watoto : Hatujambo bibi Kiwanuka

Mwalimu/M : Aah! Hamna furaha? Hamjambo kwa mara nyingine

Watoto : Hatujambo Bibi Kiwanuka (kwa sauti zaidi)

Mwalimu/M : Hiyo ni afadhali. Nina furaha mno asubuhi ya leo. Kwanza kabisa, lazima tumshukuru Mungu kwa mema yote aliyotendea shule hii.... Wasichana hawa watatu wametuletea furaha kuu siyo tu shuleni bali kwa wanawake wote. Basi waliyoyafanya wasichana hawa yamedhihirisha kwa kina dada wapewapo nafasi watakuwa bora zaidi kuliko wavulana kwa njia nyingi. Wasichana hawa wa kipekee wamedhihirisha wazi kuwa uwezo wa mwanawake unazidi kutia fora. Wameibuka washindi miongoni mwa wavulana wengi katika mkoa mzima hivyo basi chochote awezacho mume, mke aweza kufanya hata vema zaidi.

Watoto : Vema zaidi mabibi na mabwana chochote awazacho kufanya mume mke anaweza kufanya hata vema zaidi.

Mwalimu/M : Sawa kabisa. Wale wazazi wanaowaondoa mabinti zao shuleni wana funzo kuu kuiga kutoka kwa wasichana hawa watatu. Nawataka nyinyi wasichana mfanye kazi kwa bidii ili siku za usoni muwe mawakili, madaktari, wahandisi, mahakimu na hata wanasiasa. Tunataka tuwe na rais mwanamke siku moja au haiwezekani?

Watoto : Inawezekana.

Mwalimu/M : Sawa kabisa, kwa hivi sasa fumkaneni mwende madarasani mwenu lakini kumbukeni yale yote niliyosema asubuhi ya leo. Sote tuna nafasi ikiwa tutafanya kazi kwa bidii. Nawatakieni siku njema.

Watoto : Hata nawe pia Bibi Kiwanuka
*(Wimbo.... Wimbo wa maombi watoto wanapoondoka.*

*Wasimamizi wa shule nao pia wanafumkana huku onyesho linajifia hadi kwenye nyumba ya Susanna)*

Susanna : (Aingia na kuita)
Konstatino! Konstatino!
(Aingia Konstatino)

Konstatino : Lebeka bibiye.

Sisanna : Ulionana na wakili wangu?

Konstatino : Nilimkuta akisubiri tayari

Susanna : Ameshakamilisha kushughulikia urithishaji?

Konstatino : La bibiye

Susanna : Atathubutuje? Mbona uchelewesha mambo?

Konstatino : Bibiye, kuna stakabadhi moja inayohitaji sahihi ya marehemu mke mwenzio

Susanna : Lakini anaelewa vyema kuwa Priscilla aliend jongomeo. Anamtaraji aondolewe kwenye kaburi ili atiyeidhini kwenye stakabadhi? (Anaita) Konstatino!

Konstatino : Labeka bibye.
(Anaingia Charity kisirisiri)

Susanna : Nilimuua Mathayo, nilimuua Priscilla na kwa hivyo, kisheria nastahili kuwa mumilika wa mali yake.

Konstatino : Wakili asema kuwa hiki kinaweza tu kufanyika ikiwa Charity atakubali kutia hiyo stakabadhi sahihi kwa niaba ya marehemu mamake.

Susanna : Lakini Charity ni msichana mdogo wa miaka kumi na mitano. Ana uwezo gani wa kisheria kuhusiana na jambo hili?

Konstatino : Sheria bibiye.... Sheria ni mtambo usioleweka wenye umbo lisilodhihirika. Inatulazimu kutekeleza itakavyo.

Susanna : Utulivu wangu unazidi kutoweka

Konstatino : Kwa hivyo nifanyeje?

Susanna : Mtafute Charity. Lazima alazimishwe kutia sahihi stakabadhi hiyo mara moja.

Charity : (Ambaye amekuwa pale kwa kitambo kirefu). Utapata sahihi yangu nikiwa maiti.

Konstatino : (Ameghutuka) Nini? Charity? Kwani ni wewe?

Charity : Yaagize macho yako yakujibu.

Susanna : Charity. Wafanya nini hapa?

Charity : Hii ni mali ya babangu na ninaweza kuwa popote nipendapo wakati wowote nipendao?

Konstatino : Wewe, chunga ulimi wako… la sivyo utakatwa uwe kimo kinachofaa.

Susanna : Sawa kabisa. Sasa unaweza kutia sahihi yako kwenye stakabadhi hii?

Charity : Hilo litafanyika tu nikiwa mfu. Kwani unadhani mimi ni mjinga kiasi gani hata nitie sahihi stakabadhi zotakazotwaa mali ya marehemu. Babangu aliyotolea jasho. Nitawezaje kumkabidhi muuwaji wake mali yake!

Susanna : Mimi si muuwaji.

Konstatino : Bibiye huyu ni mwanamke mwenye fikira pevu na tabia isiyo dosari. Usimharibie sifa zake.

Charity : Lakini uliyanena mwenyewe…. Nimeyasikia hayo mwenyewe kwa masikio yangu na kama unataka kukana, kanda hii ya sauti itakuwa shahidi wangu katika mahakama ya sheria.

Konstatino : Wewe, leta hiyo kanda ya kunasia sauti mara moja au nitakuua.

Charity : Unaweza kuniua… unaweza kunitesa na kuudhuru mwili wangu lakini moyo wangu na roho zitabaki thabiti katika

pambano langu la kutafuta haki.

Susanna : Ni kipi kibaya na huyu msichana?

Konstatino : Mambo yamekwenda mrama bibiye. Itabidi tufanye hima la sivyo tumekwisha.
(Anaondoka Konstatino)

Susanna : Tazama hapa mwanangu....

Charity : Nani wako? Usiniite mwanao kwa kuwa huwezi hata kwa sekunde moja kuwa mamangu. Ulipanga kifo cha babangu. Yeye ndiye aliyekuwa tegemeo letu kwa riziki na kwa kifo chake starehe na furaha ya jamii ilififia. Isitoshe, ulipiga hatua na kumuua mamangu yule mke aliyenizaa. Ulijiingiza katika maisha ya babangu kwa kishindo. Kama nzi aliyevutiwa na harufu ya kinyesi cha binadamu alijiingiza katika mtego wako wa unafiki. Tamaa yako ilikuwa ni shamba lake kwa kuwa ulifahamu vyema kuwa katika ardhi yenyewe kulikuwa na almasi. Kwa nini umetutesa hivi? Ni hatia gani tuliyotenda hata kustahili mateso haya? Wewe ni mtu mla watu. Nataraji hutafanikiwa kabla ya kumalizana nami. (Anaingia Konstatino huku amemshika Purity mateka... Ana upanga aliyouinua kwenye mkono wake wa kulia.

Susanna : Sasa maisha ya dadako yamo hatarini. Yote yanategemea uamuzi wako kumwona akifa au akiendelea kuwa hai... Utatupa ukanda huo na kutia sahihi stakabadhi kwa ajili ya uhai wake au utataka kumwona akifa!

Konstatino : Fanya uamuzi mpendwa wangu. Hatuna wakati.

Purity : Dadangu... usiache waniue. (akilia) Tafadhali wape wanachotaka ili unusuru maisha yangu.... Sitaki kufa!

Charity : Lakini wataendelea kunawiri kutokana na damu ya wasio na hatia dilini? Ni hadi lini binadamu atazidi kiviszia jasho na sulubu ya binadamu mwenziwe.... Sitawapa wanachoitisha. Hata hivyo nitamwomba Mungu akupe nguvu. Nitajenga kuta za mawe kukinga kaburi lako kutokana na upepo na mvua. Nitaziweka safi utakapokufa.

Konstatino : (Akihamaki) Nyamaza!

Susanna : Hiki ni kiburi cha namna gani?

Konstatino : Kiburi cha madharau kwa wakubwa wako, kisa kisichosimulika cha upinzani. (akiita) Bibiye!

Susanna : Naam Konstatino.

Konstatino : Niruhusu na nitalipuka kama bomu na kuyanyosha mambo hapa.

Susanna : Ruhusa umepewa.

Purity : Charity tafadhali? Usiache waniuwe! Tafadhali Charity! Tafadhali.

Charity : Sitatishwa na viumbe potovu na wasio na hata chembe cha utu.

Konstatino : Charity... nitahesabu hadi tatu na ikiwa kufikia tatu hutakuwa umetimiza matakwa yetu basi nitampiga fafako dharuba la kifo mchoni mwako.

Susanna : (Akicheka) Charity mpira upo uwanjani mwako.

Konstatino : Moja!

Purity : La hasha Charity! La!

Susanna : Dadako anakuomba.

Charity : Nyamaza wewe hayawani, wewe shetani! Wewe kiumbe duni!

Konstatino : Mbili.

Charity : Konstatino, ni fahari ipi unayoiona unapowanyanyasa wanyonge.

Purity : La hasa! La! Tafadhali usiniuwe.... Mama mwambie asiniuwe.

Susanna : Mimi si mamako… mabaki ya mifupa ya mamako yanavunda katika kaburi lile. Konstatino!

Konstatino : Tatu!

Purity : Hivyo basi nitakufa? Charity niokowe.

Susanna : Mpige!
(Moyowe yanasikika Konstatino anapoinua upanga wake tayari kwa mpigo… Charity anakimbilia kumzuia… katika ghasia zinazofuata Susanna anaunyaka ukanda…mapambano yanafuata kati yake na Charity waking'ang'ania ukanda…. Anawaita walinzi).

Susanna : Walinzi! Walinzi!
(Walinzi wanaingia… wanakamata Charity na Purity)

Konstatino : Aa bibiye, tumenusurika kidogo tu.

Susanna : (Akiwaagiza walinzi) Wafunge. Watafahamu leo k uwa s ina mafuta kwenye mifupa yangu.
(Charity anafungwa)

Susanna : Nipe upanga huo
(Anafanya hivyo)

Nitawachinja mmoja baada ya mwingine kama kuku.
Nitawaomba kwa heshima ikiwa kuna yeyote asiye shujaa kamili kuondoka.
(Anamsongela Charity na yu tayari kutekeleza anayoitisha kufanya)

Purity : Achana na dadangu! Kwani huridhiki kuwa uliwauwa wazazi wangu. Achana na Charity… mbingu na ikuhukumu… Acha mbingu i kuhukumu ikiwa u tagusa hata u nywele wake… n a upate kuhukumiwa!

Susanna : Nyamaza!

Purity : Nitanyamazaje huku Mungu amenipa kipawa cha kuzungumza?

Charity : Amina! Huo ndiyo moyo dada… Huo ndio moyo. (Mayowe

yahinikiza hewani anapoanza kwa utaratibu na makini wamchinja Charity)

Konstatino : Bibiye.

Susanna : Ni nini Konstatino.

Konstatino : Utamuua.

Susanna : Lakini ni sharti afe Konstatino huyu mjinga anafahamu mengi mno lazima afe au sisi tutakufa...

Konstatino : Lakini bibiye nina wazo bora zaidi.

Susanna : Nini?

Konstatino : Afadhali tuwatoe kama manokoa kwa kampuni msituni.

Susanna : Lakini huyu msichana anafahamu mengi mno... ni lazima afe.

Konstatino : Ni sharti atakufa.

Susanna : Vipi?

Konstatino : Bibiye, nitamwagiza mkuu wa kazi pale amweke kwenye mstari wa mbele. Hapo nina hakika nguvu zake hazitaweza kutustahimili kazi hiyo ngumu.

Susanna : Waondoe kutoka hapa.

Konstatino : Ahsante bibiye.

Charity : Susanna... umedhuru na kunajisi maisha yetu ya siku za usoni... huenda tanaondoka lakini kwa uwezo wake Maulana huenda tukanusurika... tutarudi siku moja na kutetemesha tambuzi lako.

(Onyesho linalioendelea jukwaani linafifia hadi kwenye majengo ya mgodi. Wale watoto wanatokea jukwaani na kuanza kufanya kazi... wanaonekana ni wanyonge na wachovu.... Filimbi inapigwa na kiongozi... Bafe anaingia pamoja na Charity na Purity ... wanaonekana wameparara na

ni wanyonge... Kobra anawahutubia wale watoto).

Mwanajeshi : Ninafurahi jinsi mulivyoendelea na kazi. Ni kwa ajali hii ndipo ninatangaza kuwa pishi lenu litaongezwa kwa asilimia mbili (kimya) Kwani hamna furaha? Basi kitapunguzwa kwa asilimia tatu.

Mtoto 1 : Lakini bwana......

Bafe : Fyata ulimi! Wewe ndiwe unastahili kuwa wa mwisho kuzungumza. Kielelezo chema cha uzao kati ya sokwe na nguchiro aliyetumbishwa usiku wa manane. Lazima kuwa ulipokuja hapa ulikuwa mseto wa ngozi na mifupa.

Charity : Hivyo sivyo unavyostahili kumtendea mtoto! Kwani huoni kuwa mikono iliyotuumba ndiyo ile ile iliyokuumba wewe?

Kobra : (Akimpiga kofi) Wewe ni nani kuzungumza nami? Viumbe kama hawawezi kutoka kwa Mungu lakini wameundwa kwenye karakana zilizokuwa na vifaa duni.

Mtoto 2 : (Akizungumza kuhusu Charity) Na hawa ni nani Bwana?

Kobra : Wenzenu wapya. Kwa pamoja mtaabiri gari hili la moshi la jasho na sulubu hadi kifo kitakapowachukua huku mkiwa vigofu tu.

Purity : Lakini huu ni ukatili!

Kobra : Hakuna dhuluma mahali kazi inapotekelezwa walaumu Adamu na Hawa sasa fumukeni kwa chakula chenu cha mchana ambacho ni spesheli kabisa leo hii.

Wote : Chakula spesheli!

Kobra : Ndiyo

Mtoto 2 : Ni nini bwana?

Kobra : Mtalishwa kwa mchanganyiko wa kumbekumbe waliokaangwa na viazi vilivyookwa.
(Watoto wanashangilia)

Tuwanyikeni hawa makurutu wataungana nanyi baada ya kufahamishwa jinsi kazi inavyotekelezwa (filimbi inapigwa.... watoto wanafumkana. Bafe anatembea kumwelekea Charity akionyesha shauku) hakuna awezaye kukosa kukubali kuwa hili ni embe tamu na lenye umbo zuri. (Akajaribu kumgusa)

Charity : Wewe!

Purity : Usimguse dadangu kwa mikono yako michafu.

Kobra : Nitamfanyia lolote nitakaloamua kwa njia yoyote ninayodhani ni sawa. Nyinyi ni mali yangu na mtacheza ngoma yangu kwa uamuzi wangu na mapendeleo yangu.

Charity : Lakini tumefanya nini kustahili haya?

Purity : Nyinyi ni watoto wa utawala dhalimu.

Charity : Kwani utawala wako ni wa haki inayozidi kuibuka? Ule unaofurahia kuyadhuru maisha yetu machanga. Huu ndio uongozi wa kibadala unaolipa bara hili...? Ambapo watoto wanahasiriwa na kuteswa hadi kifo wewe si wengine bali ni tui mwenye pupa ya pesa! Waoga wa hali ya juu! Mmesaliti nia yetu ya ukombozi na kuhasiri ardhi yetu.... Maadui! Wasaliti wapumbavu! (Bafe anampiga kofi Charity anyeanguka akilia... Purity anamweelekea upesi kumfariji)

Purity : A Charity... mapigano ya misuli na miemeso ya ari nafasi yetu ya kuweza kuendelea kuishi... mapambano haya ni ya Mungu.

Charity : La, tafadhali nyamaza... Niambie Mungu huyo wako yuko wapi. Ni Mungu yupi atakayeruhusu watoto wasiokuwa na hatia kuweza k uyapitia haya y ote makubwa n a v isanga vya kutisha katika maisha yao. Kwani huyo Mungu wako ni kipofu! Ni kiziwi kiasi kwamba hawezi kusikiza kilio cha mayatima wawili walio kwenye mateso makuu?

Purity : Usinene mambo kama hayo Charity hebu tutazame msalaba huu kwa utulivu; wa moyo na amani...kumbuka kuwa mama alitushawishi kila mara tuweke imani yetu kwa Mungu.

Charity : Namna yeye na baba walivyofanya. Kwa hivi sasa si wamekufa? Nijibu.... Kuna haya gani kumshukuru Mungu ambaye hasikii maombi na malalamiko ya watu wake... kuna sababu gani?

Kobra : Nyamazeni nyinyi wawili (anapiga makofi) leta chuma (chuma kilicho kwenye mkebe wa makaa yaliyo moto kinaletwa na wale wasimamizi wengine) fanyeni kazi.

Charity : Kazi gani?

Kobra : Wana jeshi wetu wote lazima watambulike kwa nyota katika mkono wao wa kushoto.

Charity : Kutiwa alama.... Kwani sisi ni ng'ombe... mtatekeleza tu kifono mwangu.

Kobra : (Wanapomshika) Niache; niache... niache nyinyi wauaji! Nyinyi mashetani (anazidiwa nguvu)

Purity : Ni nini maana ya kuwekwa alama.

Kobra/bate : Ni oparesheni isiyokuwa na dhara lolote hata hivyo ina umuhimu mkubwa. (Wanashika hicho chuma... mlio wa ngoma unasikika anapoanza kazi mwilini mwake Charity ambaye anapiga yowe linalofunga masikio) Waona (anamwambia Charity) Ni rahisi mno.

Purity : Tafadhali bwana usinifanyie haya, siwezi kustahimili huo uchungu.

Bafe/Kobra : Mwombe Mungu wako ajitokeza na kukookoa.

Charity : (Huku akiendelea kulia) La! Huwezi kumfanyia....

Huwezi!

Bafe/Kobra : Na ni nani atanikomesha.

Charity : Nakutafadhalisha bwana yeye ni mnyonge; moyo wake hafifu atazidiwa na huo uchungu. Maiti ina manufaa gani kwako? Ni furaha gani uipatayo kutoka kwa wafungwa waliobaki magofu ya watu. Nakuomba tafadhali... kwa jina la Mungu,

mhurumie dadangu .... Atakufa.

Bafe/Kobra : Si Mungu wako wala wewe atakayenifanya nibadili nia yangu.

Charity : Lakini ya mnyonge na shaifu. Tafadhali elewa.

Bafe/Kobra : Unaniomba niwe mbaguzi? Siwezi kuwa na vipimo viwili tofauti? Mimi ni kiongozi aliye na msimamo thabiti na hivyo basi sina ubaguzi.

Charity : La, asiye na hisia zozote!

Kobra/Bafe : Asiye na doa! (Dosari)

Charity : Asiye na heshima! Asiyeweza kubadili mwendo wake mbovu! Aletaye aibu isiyoelezeka. (Anapigwa kofi na kuanguka akipiga mayowe)

Bafe/Kobra : Hakuna mwanamke anayeweza kumtusi komanda shupavu. Mkamate huyu msichana mdogo. (Wanamkamata Purity)

Charity : La! Tafadhali bwana! Nakuomba unusuru maisha yake... Ni yeye tu niliye naye.... Utakatifu alio nao hunipa maana maishani. Hapa... (Akivuta mkono wa pili wa nguo) acha nichukuwe alama ya pili kwa niaba yake dadangu lakini usimuuwe na hicho kifaa.

Bafe : Kwa nini kwa ghafla unageuza msimamo wako wa ujeuri kuwa ombi lenye kutia huruma ya kujiuzulu? Haki isisemwe tu bali lazima ionekane ikitekelezwa. Huo ndio msimamo wetu? Mashetani.

Charity : Lakini ni haki ya nani? Haki ya nani inayokubali mauwaji ya watoto wasiokuwa na nguvu za kujitetea kwa jina la pesa.

Bafe : Haki yangu! Upendo wangu! Leta chuma nambari mia saba na nne. (Chuma kinaletwa)

Charity : La! Niweke alama mara nyingine lakini mwache dadangu... la laaaaaa!
(Kuweka alama kunafanywa kwa Purity ambaye anapiga

yowe na kuaguka kana kwamba amekufa... Charity wakati uo huo anakimbilia upande wake anajaribu kumtikisa) Purity! Purity! Amka Purity amka (kimya... mlio wa ngoma) umemua... umemua dadangu (anaanza kuomboleza) watu.... Tazameni walichomfanyia dadangu... tazameni... kwani kuna hatia kuwa hai? Kwa kuwa hai tumehukumiwa kufa kifo chenye mateso makubwa... kwa kuwa hai tumenyimwa haki ya upendo wa familia yetu... maisha si kitu kingine bali ni wimbo wenye kuleta huzuni kubwa.... Ndoto ile inayochukiza... hadithi isiyofurahisha. Alikuwa na umri wa miaka minane tu lakini wamechomoa moyo wake.... Wamemua bure dadangu mcha Mungu... lakini Mungu yu wapi, yuko wapi? Dadangu amekufa.... Nawe umenyamaza wanadamu hebu tazameni hiki kikwamizi ambacho ni picha ya fikira za binadamu... maisha yetu yanapitia kwenye kimo kifupi cha kifo... hebu tazama waliyomtendea Purity... tazama huu unyama uliofanyiwa kizazi hiki kipya... tulikuwa na ndoto sote tulikuwa na matumaini ya kile tulichotaka kuwa katika maisha.

Mtoto 1 : Nilitaka niwe mhandisi ili niongoze nchi yangu kwenye njia za ufanisi.

Mtoto 2 : Nilitaka niwe wakili ili nipiganie utekelezaji wa haki

Mtoto 3 : Ilikuwa ndoto yangu kuwa mwalimu ili niwape vijana wadogo maadili ya maisha mema.

Watoto : Tulitarajia maisha mema ya siku za usoni... yaliyojaa amani, upendo na maelewano!

Charity : Mbona mnanitazama kwa macho hayo? Mbona mwaamsha ndoto za matarajio na matumaini yangu? Mimi pia nilikuwa na ndoto. Ndoto yangu ilikuwa ni kuipanda ngazi hii ya ufanisi na kuwa daktari!

(Mashangilio anapopokea koti la daktari na stetoskopi). Nilikuwa baada ya hayo nirudi na kuwashughulikia kimatibabu wanyonge waliombukizwa na magonjwa.... Nilikuwa na matumaini ya kushiriki kwenye mwito wa amani katika bara letu lililohasirika. Hata hivyo, sauti hizo tumepokonywa. (Mlio wa ngoma... mayowe). Na hivyo basi ndoto zangu mbaya imehasirika ikiwa bado changa na

kukoma. (Mlio wa ngoma... mayowe.... Koti na stoteskopi zinachukuliwa) nimeachwa bila matumaini yoyote, bila msingi wowote na bila maana... watoto wamedunishwa kuwa fungu la sauti isiyo maana. (anaanza kulia... mlio wa ngoma onyesha linaporejelea uhalisi kutoka kwenye ndoto)

Nitawezaje kusahau mateso hayo yote? La, sitaweza kwa kuwa kumbukumbu za uovu huo unaochukiza mara kwa mara hurudi kama picha katika fikira yangu.

Daktari : Susanna hapa una dakika ishirini tu za kuishi.

Purity : Kwani tuliishi kwa nini ikiwa hatuwezi kutumia maisha yetu aliyotupa Mungu kwa maisha ya mtoto mwingine wa Mungu... Charity.... Ndugu na dada.... Uamuzi wa kubadili shamba lililomwagikiwa damu inatutegemea leo hii.... Watoto watakaoishi bada yetu watatuzamaje... kama watu walionawiri kwenye ulipizaji kisasi kama watu waliokuwa na uhai kwenye upumuo wao na hawakuweza kuwapumulia waliokuwa wakifa fadhili... mamangu alikuita Fadhila! Iliyo na maana ya 'awapao walio na haja.... Mkono unaookoa'. Utamtazama akiomboleza katika kaburi lake anapokanyagia mbali ndoto kwako? Utafanya hivyo? Ndugu tumsihi Fadhili (Charity) ampe huyu mwanamke uhai.... Kifo chake kisijiandikishe katika siku zetu za usoni... katika mioyo na fikira zetu.

Charity : Siku za usoni zina ahadi gani kwetu ikiwa misingi yake imejengwa.

Fadhili : Katika ardhi isiyothabiti na siku za nyuma zilizochanika? Nitawezaje kufuta kutoka kwenye benki ya mawazo yangu yaliyosumbuliwa na sauti ya kishetani ya Kobra akitupa amri? (Anaingia Kobra/Befa)

Kobra/Befa : Muda umemalizika. Rudini kazini (watoto wanasimama polepole). Nilisema haraka! (Anamchapa mmoja anamcharaza mmoja viboko)

Mtoto : Lakini tuna njaa! Tunahisi njaa. Tafadhali Bwana mkubwa Bafe. Tupe chakula!

Wote : Tuna njaa! Tuna kui! Tunaomba utuachie uhai?

Charity : Tuhurumie. Tuokoe Befa.

Kobra/Bafe : Mimi si masihi aliyeulisha umati kwa samaki na mkate.

Charity : Tuhurumie Befa.

Wote : Macho yetu yamechoswa na kulia.
Macho yetu yako katika ghasia vurugu.
Siku baadaa ya siku
Mioyo yetu inamea majonzi?

Tunanyosha mikono yetu iliyooza na kutoa harufu mbaya kwa majuto makuu
Tukiomba
Tukitumaini
Tukisihi
na kutumai

Charity : Lakini tokeo
Linalosusha hadhi binadamu
Hakuna mkono unaonuia
Kutoa
Hakuna moyo aliojitolea
Kifariji.

Watoto : Kuna uchungu kwenye ubinadamu
Kuna uchungu kwenye mioyo yetu
Kuna uchungu kwenye roho zetu
Kuna uchungu kwenye mawazo yetu
Kuna uchungu
Kuna uchungu pote pote

Fadhili : Lakini uchungu huo haupo kwake Kobra?

Charity : Uchungu huo haupo katika mawazo ya jamii?

Matumbo yafananayo na mitungi. Tupe uhai Kobra….

Tupe chakula… chakula…. Chakula!

Wote :

Tazameni ya njaa yawaumiza jinsi giza limezavyo mchana

Kobra :

Ndiyo!

Wote :

Nyuso zenu bikira sina chumvichumvi na inayonata kwa

Kobra : linalovunda kutoka na udhalilishaji wa kiuchumi.

Wote : Ndiyo!

Bafe : Mataumbo yenu yalia kwa jinamizo la njaa.

Wote : Ndiyo!

Kobra : Na chakula mtupatie! (Watoto wanashangilia) Basi chimbeni handaki ikiwa mnahitaji chakula kwa kuwa msingi lazima uwekwe kabla ya kutua jua. Ikiwa hamtafanya hivyo basi mtalishwa kwa chakula spesheli cha njaa na ukame.

Wote : Uuui

Charity : Lakini tutafanyaje kazi na matumbo yasiyokuwa na chochote? Mingurumo ya tumbo zetu imenea chembe zilizosalia miilini mwetu.

Kobra : Nimesema hakuna kazi, hakuna chakula. Chakula hutoka na kibaba cha kazi ngumu.

Chaity : Lakini bwana Kobra, tutawezaje kufanya kazi na matumbo yasiyokuwa na chochote na kiu? Hata gari linahitaji petroli ili kukimbia. Sauti zetu zimekuwa chungu kwa ukavu. Ndimi zetu zimetoneshwa kwa kiu.

Kobra : Ziloweshe kwa mate yenu.

Charity : Lakini mate yenu pia ni makavu! Lakini ukame wa uchungu uliozidi na njaa umechimeka kuwa jivu. Jivu lenye sumu.

Wote : Matumbo yetu si chochote ila tu ni dimbwi la jivu.

Charity : Hebu mtazame huyu msichana mdogo aliyedidimishwa kama fungu la mifupa inayochakata. Ndiye yule Befa (dalili za njaa zinapojitokeza)
Naweza kuona sura mbaya ya njaa na ukame ikijikusanya katika wingu la anga yenye huzuni na kuangamiza. (msichana

mchanga aanza kuhema)
Oh! Laaaa! Befa kwa nini huweszi kumwokoa mtoto huyu mkembe kutoka kwa kivuli lacha mauti? Maisha yake yamo mikononi mwako Befa na kama huwezi kumfanyia hisani, basi mfanyie Mungu!

Kobra : Ni Mungu atoaye na kuchukua na mapenzi yake yatimizwe.

Charity : Huwezi kusema hivyo Befa! Tazama! Yu karibu kufa, tafadhali mwokoe.

Kobra : Jivu kwa jivu.

Charity : Tafadhali Mungu, muhurumie. Usimruhusu kufa tafadhali. Mnusuru.

Kobra : Uvumbi kwa vumbi.

Charity : Befa! (anafikiri).

Wote : Tafadhali bwana!

Kobra : Ni Mungu aliyetupa, mwache amchukue.
(Ishara zaumiza. Watoto wanalilia na kuanguka mtoto alipofariki. Zaraili waliingia na kuchukua ya mtoto mfu. Wengine walia kwa kwi kwi mtoto huyo anapotolewa)

Kobra/Befa : Sasa rudi kazini (kimya). Nilisema turudi kazini!

Charity : Sasa hatuwezi! Tutadhaliliwa kwa muda gani chini vitatangi vya pingu za ukatili?

Wote : Kwa muda gani?

Charity : Tutakaa tu na kutazama ndugu zetu wakifa machoni petu.

Wote : La!

Charity : Tutakaa?

Wote : La!

Charity : Tutakaa?

Wote : La!

Charity : Befa, muda wako umekwisha! Siku nenda siku rudi umetulisha makombo ya udhalimu. Walakini, leo hizi akili zetu na juhudi zetu zimezinduliwa na fahamu ngeni. Utambuzi mpya unaoleta maumivu….

Wote : Katika sahani ya mavune!

Befa : Oh! Mwaweza kunyamaza!

Charity : Waweza kutuua Befa. Waweza kututesa. Waweza kuvunja nyoyo zetu dhalali kwa muda mrefu lakini huwezi, narudia huwezi kudidimiza miale ya ari nyoyoni mwetu.
(Watoto washangilia)

Befa : Sifurahii mfanyacho na msinifanye kujutia hatua yangu.

Charity : Twaweza kuwa wachanga, Befa. Twaweza kuwa wanyonge lakini tusiozuilika na tulio na azma katika kiu chetu cha (haki) kudai haki.

Watoto : Tuna nguvu!

Befa : Nawaamuru kutawanyika na kurudi kazini sasa!

Charity : Hatuendi popote!

Befa : (Aita) Askari! Askari! Askari!
(Askari waingia na mijeledi)

Charity : Mwaweza kututisha na vifaa hivyo vya maangamizi, lakini nyoyo na roho zetu zitabaki imara na zenye maazimio katika juhudi za kupigania haki zetu (vigelegele)

Befa : (Anakiasirika) Huu ni ukaisi gani! Shambulia!

(Mayowe watoto wanaposhuka jukwaani kukimbilia maisha yao. Askari wanafuata unyounyo. Watoto wachache wajikwaa huku wangine wakwepa… Ziraili waingia na kwa dhahania wachukua roho za waliokufa, yaliyopita yanapojipenyeza kuwa uhalisia.)

Charity : Purity, nawezaje kusahau mateso hayo yote? La siwezi. Nimeshaamua na sasa naondoka, kwa vile sina nafasi katika maisha ya mwanamke huyu.
(Charity ashukia ukumbini)

Daktari : Dakika nane zaidi…

Purity : Dadangu Charity… kabla hujatoka ningetakea uamue kumpa huyu mama uhai na ubaki dadangu ama umwache afe na nitaenda naye.

Charity : Dadangu mbona wanifanya kufutia haya yote?

Daktari : Dakika tano zaidi.

Purity : Charity! Toa uamuzi wako.

Watoto : Ndio Charity! Toa uamuzi wako! Tangaza msimamo wako!
(Ngoma… kichagizo cha muziki chasikika chini kwa chini)

Charity : Dadangu Purity, haikuwa kwa mapenzi yangu nifanye hivi bali kwa sababu ya mapenzi yangu kwako na kwa Mungu yanavuka kiwango cha mapenzi yangu kwa maisha.

Daktari : Dakika moja zaidi kwa Susanna kuishi.
(Susanna aanza kukohoa kwa kuhema Charity atoa ndani yake mfano wa figo na kumpa Daktari akisema…)

Charity : Nitampa mwanamke huyu figo yangu niliyopewa na Mungu. Kudhihirisha mikakati na sabanu za kujitolea kwetu kufa.

(Vigelegele Daktari anapompa Susanna aliyekaribia kufa mfano wa figo na ambaye anawewesuka na kuwa hai… ngoma yalia anaposimama polepole kwa msaada wa fimbo kutoka kitini na kutembea kuelekea kwa watoto).

Susanna : Charity, mbona hukuniacha nife! Naona fedheha kuishi.
Hapa….
(Waingia wasichana wanaoashiria utajiri)

Yote niliyochukua kwako
Fedha

Ardhi
Almasi
Vichukue, uvitumie kurekebishia maisha yako yaliyochanganyikiwa na kutatizika.

Ni kwa bahati mbaya kwamba siwezi kuwapa uhai wazazi wako tena. Kwangu, ni mwanamke aliyetahayuri kwa vitendo vyake. Nilikotoka na pole kwa yote. Kwaheri wanangu.
(Aanza kulia anapoanza kuondoka)

Charity : La! Sitakubali kuenda kujitosa kwenye taya ya mauti kwa vile hiyo itasaliti moyo wetu wa upatanishi tuliopata kwa taabu. Njoo Susanna, njoo tusaidiane kujenga maisha yetu ambayo tayari yameharibika.

Susanna : Lakini…

Charity : Hamna wakati wa lakini.
Tutakupa nafasi nyingine ya kuwa mama yetu.

Watoto : Lakini utuahidi kuwa wakati huu utakuwa mama mwema.

Susanna : Oh! Nitafanyaje mpaka mniamini tena?

(Wote wakumbatiana…
Wakiwa kwa furaha.
Mlio wa ngoma wasikika… moyo waingia).

Charity : Mwana wa Afrika!
Wewe ambaye mashavu yako bikira yamenajisiwa
Kwa machozi potovu mororo ya ujamaa uliooza
Inuka…
Inuka kutoka kwa dhoruba kali ya maangamizi na kujiunga na (wengine) kusherehekea majilio ya uhuru wako.
Tazama ndani yake waona nini?

Sauti : Juhudi zetu! Haki zetu! Utukufu wetu! Hakuna salubu ya watoto tena!
Hakuna ukandamizaji tena!
Hakuna tusi ya watoto tena!
(Vigelegele)

Charity : Mwana wa Afrika! Sasa uko huru!

(Vigelegele kwa sauti ya juu
Wote waanza kumba wimbo
Mmoja upatanishi (PTO)
Ni wakati huu ambapo pazia zinafungika polepole).